# JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA

## UDONDOZI KUTOKA KITABU: JAWAAHIRU AL-HIKMAH LI 'SH-SHABAAB


## KIMEANDIKWA NA: MUHAMMAD REYSHAHRI

### KIMETARJUMIWA: HEMEDI LUBUMBA SELEMANI

**KIMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: HAJAT PILI RAJAB**


### NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho, Jawaahiru 'Al-Hikmah li 'sh-Shabaab, ambacho tumekifupisha na kukiita: (JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA).

Kwa hakika kitabu hiki kinazungumzia maadili ya vijana kwa mtazamo wa Kiislamu. Kama tujuavyo, Uislamu ni dini na mfumo kamili wa maisha, kwa hiyo, haukuacha chochote kinachomhusu mwanadamu katika maisha yake ya hapa duniani na ya kesho Akhera.

Mwandishi wa kitabu hiki amejaribu kwa uwezo wake kuwakumbusha vijana juu ya wajibu wao katika jamii na kuwarejesha katika maadili mema. Na katika kuikamilisha kazi yake hii amerejea sana kwenye mafunzo ya Uislamu ambayo chimbuko lake ni Qur'ani na Sunna. Hivyo basi, huu ni mwongozo halisi kwa vijana unaolenga kuwaokoa katika harakati zao za maisha na hatimaye wawe ni wenye kufuzu kesho Akhera.

Sisi tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu ambapo vijana wengi wamejitumbukiza katika mambo yenye kuangamiza maisha yao kwa kuacha utamaduni wao bora wa Kiislamu na kuiga tamaduni potofu, fasiki na fisadi za watu wa Magharibi (wazungu). Watu wenye busara huiga mambo mazuri na huwaachia wenyewe yale machafu, lakini kwa vijana wetu sivyo, wamepupia sana katika kuiga kama kima kila jambo karihifu la watu wa Magharibi. Hivyo kitabu hiki kitakuwa ni mwongozo mzuri kwa vijana wetu wa Kiislamu na hata wasio Waislamu.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Hemedi Lubumba Selemani kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni mwanga kwa wasomaji wetu na kuzidisha upeo wao wa elimu ya dini ni ya jamii.

## DIBAJI

Bismilahi Rahman Rahim. Rehema na amani zimwendee Mtukufu wa Daraja Mtume Muhammad **(s.a.w.w)**, yeye na kizazi chake watoharifu maasumina (a.s). Bila shaka kipindi cha ujana ndio fursa muhimu inayompa mwanadamu uwezo wa kutimiza vipaji na uwezo binafsi, kama ambavyo vijana ni haz- ina kubwa yenye thamani ndani ya jamii mbalimbali za wanadamu. Kuanzia hapa ndipo maendeleo yote ya nchi yoyote ile yakategemea jinsi vipaji vya vijana vitakavyotunzwa, na jinsi watakavyoelimishwa na vipaji vyao kukuzwa. Kwa ajili hiyo daima wanaharakati, viongozi wa kidini na wa kisiasa wametilia sana umuhimu wa harakati za vijana ndani ya zama zote za historia ya mwanadamu. Katika zama zetu hizi za maendelelo ya sayansi na teknolojia, upande mmoja tunakuta kitendo cha vijana kukusanya maalumati na maarifa mbal- imbali kimesaidia sana katika kuleta maendeleo ya kielimu na kiteknolo- jia. Upande mwingine ni kuwa watu wa manufaa na wafanyabiashara wenye masilahi binafsi ya kisiasa na kiuchumi katika ulimwengu huu, wamejiandaa kutumia fursa hii kwa lengo la kutumia vibaya vipaji vya vijana kuliko zamani, hivyo ndio maana suala la vijana limekuwa na umuhimu sana leo kuliko hapo kabla. Bila shaka kipindi hiki cha ujana ndio ardhi munasibu yenye rutuba safi na mbolea bora ya kuweza kuhifadhi mbegu bora na hatimaye kuotesha mazao endelevu kwa ajili ya leo na kesho, kwani ndio kipindi ambacho Mwenyezi Mungu amekipa sifa ya nguvu na uwezo wa kila kitu, kiasi kwamba ubora na ufanisi upatikanao ndani ya kipindi hiki hauwezi kupatikana nje ya kipindi hiki. Mwenyezi Mungu asema:

Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuumbeni katika udhaifu, na baada ya udhaifu akafanya nguvu, kisha baada ya nguvu akaufanya udhaifu na uzee, huumba apendavyo, naye ni Mjuzi Mwenye uwezo." (Surat Rum: 54).

Kisha akasema tena: "Yeye ndiye aliyekuumbeni kwa udongo, kisha kwa manii, kisha kwa pande la damu, halafu akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha ili mpate nguvu zenu kamili, kisha (akakuacheni) muwe wazee, na wengine wenu hufishwa kabla (ya uzee) na ili mfikie muda uliowek- wa, na ili mpate kufahamu." (Surat Muumin / Ghafir: 67). Ni dhahiri Aya zilizotangulia zimeonyesha thamani ya ujana na matarajio endelevu kutoka ndani ya kipindi hicho ambacho Imam Jafar As-Sadiq (a.s) amekiwekea kikomo kwa kusema: "**Mtu akizidi miaka thelathini basi ameshakuwa mzee, na akizidi arubaini basi tayari keshakuwa kikongwe**."[1]

Japokuwa katika zama zetu hizi kila taifa au kundi hujiwekea mwanzo na kikomo cha ujana, lakini hakuna anayeepuka umri huo uliotajwa na Imam Jafar (a.s), na hivyo naweza kusema kuwa lengo si umri, bali lengo ni jinsi gani mwanadamu ndani ya maisha yake anaweza kutumia vizuri kipindi chake chote cha uwezo na nguvu zenye ufanisi na ubora, kipindi ambacho bila shaka ndio kipindi cha ujana. Sijaona msiba mkubwa katika nchi zetu za kiafrika na hasa Tanzania kama msiba huu wa vijana kutokujali kabisa kipindi chao hiki, lakini linaloshangaza zaidi ni kuona wazee ambao ni

1. Biharul-An'war, Juz. 75. Uk. 253.

waathirika wa mafunzo ya ujana jinsi gani wameshindwa kabisa kuwaandaa watoto wao kwa ajili ya kipindi hiki chenye thamani. Kutokana na uzembe huo wa wazee vijana wengi wameshindwa kujua thamani ya ujana wao, na hivyo kusababisha baadhi ya hasara za kijamii za kujitakia ikiwemo, ujinga, viongozi mbum- bumbu, ufisadi, utumiaji wa madawa ya kulevya, ulevi, ushoga, ukahaba, ubakaji, ujambazi, ufukara, umaskini, maradhi na mengine mengi yanay- ochangiwa sana na kitendo cha vijana wa zamani kutowaandalia mazingi- ra vijana wa sasa. Uisilamu unatambua thamani ya ujana na athari zake za kiroho na kimwili hadi kimaada, ndipo Imam Ali (a.s) akasema: "**Hakika moyo wa kijana ni sawa na ardhi tupu, chochote kitakachotupwa hapo hukikubali**." Hapo Imam akataka vijana wapandikizwe maadili mema na mtazamo sahihi ili maadui wa ubinadamu wasiweze kutumia fursa hiyo kupanda mbegu zenye sumu kwa jamii. Mtume **(s.a.w.w)** alijali sana kuwasomesha na kuwalea vijana, hivyo jiwe lake la kwanza alilolitaka katika msingi wa Uislamu lilikuwa ni vijana, na hivyo ndivyo ilivyokuwa, na kijana wa kwanza akiwa ni Ali (a.s) ambaye kwa ujana wake aliusimamisha Uislamu, ndipo Mtume **(s.a.w.w)** akawausia sahaba zake:

"**Nawausia kheri kwa vijana, kwani hakika wao ni wenye vifua vyepesi, Mwenyezi Mungu alinituma niwe mbashiri na muonyaji, vijana wakaniunga mkono, na wazee wakanipinga**."

Na kwa msingi huu Imam Jafar As-Sadiq (a.s) akamuusia Abu Jafar Al-Ahwal akimuomba kuwasambazia vijana elimu na maarifa ya Ahlul-Bait (a.s) ili waweze kuharakisha kuelekea kwenye kila la kheri, akasema: "**Shikamana na vijana, kwani hakika wao ndio wepesi kuelekea katika kila kheri**." Na hivyo kauli hii ya Imam inaelekeza na kuwajibisha majukumu kwa walezi, wazazi, viongozi wa kidini na kisiasa, wanaharakati na vion- gozi wa jamii. Mwenyezi Mungu anawapenda sana vijana, na ndio maana wafuasi shu- pavu, makini na waaminifu walikuwa ni vijana, au kwa kauli nyingine ni kuwa Manabii na Mawasii wakiwemo Maimamu wetu (a.s) walikuwa ni sehemu ya vijana. Basi Kitabu hiki ni sehemu nyingine ya mwongozo wa Mwenyezi Mungu na upendo Wake kwa vijana wote na hasa wa kizazi hiki ambacho kimezungukwa na kila aina ya mitego ya ufisadi, uovu na uasi.

# JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA

# SEHEMU YA KWANZA

## NAFASI YA KIPINDI CHA UJANA KATIKA USTAWI

### 1- KIPINDI CHA USTAWI WA MAISHA

Thamani ya ujana: Mwenyezi Mungu asema: "Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuumbeni katika udhaifu, na baada ya udhaifu akafanya nguvu, kisha baada ya nguvu akaufanya udhaifu na uzee, huumba apendavyo, naye ni Mjuzi Mwenye uwezo." (Surat Rum: 54).

Akasema tena: "Yeye ndiye aliyekuumbeni kwa udongo, kisha kwa manii, kisha kwa pande la damu, halafu akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha ili mpate nguvu zenu kamili, kisha (akakuacheni) muwe wazee, na wengine wenu hufishwa kabla (ya uzee) na ili mfikie muda uliowekwa, na ili mpate kufahamu." (Surat Muumin/ Ghafir: 67).

Imam Ali (a.s) amesema:

**"Vitu vinne thamani yake hakuna anayeijua ila watu wa namna nne:**

**(a) Hakuna anayejua thamani ya ujana ila wazee.**

**(b) Hakuna anayejua thamani ya afya ila mwenye maradhi.**

**(c) Hakuna anayejua thamani ya siha ila mgonjwa.**

**(d) Hakuna anayejua thamani ya uhai ila wafu."**[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hakuna anayejua thamani ya vitu viwili ila yule aliyevikosa: Ujana na afya.**"[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Vitu viwili lau macho mawili yatavililia kwa machozi ya damu mpaka yadondoke, bado hayatafikia uzito wake: Kupitwa na ujana na kuwakosa vipenzi.**"[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ujana waniliza umenitoka, natamani ujana ungenirudia. Lau ujana ungekuwa unauzwa kwa lolote, basi hakika ningempa muuzaji atakacho. Lakini ujana unapoondoka kuupata ni kazi.**"[4]

### KUNUFAIKA NA FURSA YA UJANA

Mwenyezi Mungu asema: "Na utafute makazi ya Akhera yale aliyokupa Mwenyezi Mungu wala usisahau sehemu yako ya dunia." (Surat Al-Qasas: 77).

Akasema tena: "Na humo watapiga makelele: Mola wetu Mlezi! Tutoe (Motoni) tutafanya vitendo vizuri visivyokuwa vile tulivyokuwa tukifanya! Je, hatukukupeni umri (mwingi) akumbuke mwenye kukumbuka, na alikufikieni mwonyaji, basi onjeni, na hakuna msaidizi kwa ajili ya madhalimu." (Surat Faatir: 37).

---

1. Al-Mawaidh Al-Adadiyyah Uk. 218.
2. Ghurarul-Hikam: Hadith ya 5764.
3. Ad-Daywan Al-Mansuub ilal-Imam Ali (a.s) Uk. 100.
4. Ad-Daywan Al-Mansuub ilal-Imam Ali (a.s) Uk. 206.

**Mtume wa Mwenyezi Mungu** (s.a.w.w) **amesema: "Ewe Ali! Vitumie vitu vinne ipasanyo kabla hujafikwa na vinne:**

**(a) Ujana wako kabla ya utu uzima wako.**

**(b) Siha yako kabla ya ugonjwa wako.**

**(c) Utajiri wako kabla ya ufakiri wako.**

**(d) Uhai wako kabla ya kifo chako."**[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mja ajiandalie matumizi ya akhera yake kutoka kwenye dunia yake, na ya kifo chake toka kwenye uhai wake, na ya uzee wake toka kwenye ujana wake, kwani dunia imeumbwa kwa ajili yenu na nyinyi mmeumbwa kwa ajili ya Akhera.**"[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Enyi watu! Hakika mna dira zitazameni dira zenu na hakika nyinyi mna kikomo tazameni kikomo chenu, kwani hakika muumini yupo baina ya vitu viwili vyenye kuogopesha: Siku iliyopita ambayo hajui Mwenyezi Mungu atamuhukumia nini humo, na siku iliyobakia hajui nini Mwenyezi Mungu atamtendea humo. Basi mja achukue toka ndani ya nafsi yake kwa ajili ya nafsi yake, na toka ndani ya dunia yake kwa ajili ya akhera yake, na toka ndani ya ujana wake kwa ajili ya uzee wake, na toka ndani ya siha yake kwa ajili ya ugonjwa wake na toka ndani ya uhai wake kwa ajili ya kifo chake. Naapa kwa Ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake kuwa baada ya mauti hakuna mkemewaji, wala baada ya dunia hakuna nyumba ila pepo au moto**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mambo ni rehani ya wakati wake.**"[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Harakisheni kutumia fursa kabla haijakuwa chungu**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Dunia iko karibu mno na uondokaji, na uzee uko karibu mno na ujana.**"[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hakukitendea kabisa haki kifo yule anayeian- daa kesho kwa ajili yake.**"[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Itumieni fursa ya kheri, kwani bila shaka yenyewe hupita mpito wa mawinguni.**"[8]

Imam Ali (a.s) amesema kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: "Wala usisahau sehemu yako ya dunia" (Surat Al-Qasas: 77) "**Usisahau siha yako, nguvu zako, faragha yako, ujana wako na fungu lako kuvitumia katika kuitafuta Akhera.**"[9]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: "Je, hatukukupeni umri (mwingi) akumbuke mwenye kukumbuka, na

---

1. Man la yahdhuruhul-Faqih Juz. 4 Uk. 35, Hadithi ya 5762. Al-Khiswal Uk. 239, Hadithi ya 85.
2.Tanbihul-Khawatir, Juz. 1, Uk. 131.
3. Aalamud-Diin, Uk. 333.
4. Awali Al-Laaly, Juz. 1, Uk. 293, Hadithi ya 180.
5. Nahjul-Balagha, barua ya 31.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 9689.
7. Al-Kafiy Juz. 3, Uk. 259, Hadithi ya 30.
8. Ghurarul-Hikam, Hadithi ya 2501.
9. Al-Amaali cha As-Suduq Uk. 299, hadithi ya 336.

alikufikieni mwonyaji, basi onjeni, na hakuna msaidizi kwa ajili ya madhalimu" (Surat Faatir: 37) "Ni kumfokea kijana wa miaka kumi na nane."[1]

Imepokewa ndani ya kitabu Tanbihul-Khawatir kuwa: "Nabii Issa [(a.s)] alikuwa awakutapo vijana huwaambia: "**Ni mazao mangapi hayajafikia mavuno." Na akiwakuta wazee huwaambia: "Mazao yakishafikia (mavuno) huwa hakuna linalongojewa ila kuvunwa.**"[2]

## HAZINA YA SIKU

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "Siku ya Kiyama mja atafunguliwa hazina ishirini na nne, sawa na idadi ya saa za usiku na mchana za kila siku kwa idadi ya siku za umri wake, atakuta hazina moja imejaa nuru na furaha, basi atakapoishuhudia ataichukua kwa fura- ha ambayo lau wakigaiwa watu wa motoni basi inawashtua kwa kuwaondolea hisia za machungu ya moto. Na hiyo ndio ile saa aliyomtii ndani yake Mola wake. Kisha atafunguliwa hazina nyingine, ataiona ikiwa na giza kali lenye kutisha, basi atakapoishuhudia ataichukua kwa uoga na mdhazaiko, kiasi kwamba lau wakigaiwa watu wa peponi neema Zake zitakuwa chungu kwao. Hiyo ndio ile saa aliyomuasi ndani yake Mola wake. Kisha atafunguliwa hazina nyingine na kuona ikiwa tupu haina kinachom- furahisha wala kumchukiza, hiyo ndiyo ile saa aliyolala ndani yake au kujishughulisha na jambo la halali la kidunia, hapo ataichukua kwa hasara na majuto kwa kupitwa na saa hiyo, kwani alikuwa anaweza kuijaza mema yasiyohesabika. Na hii ndio kauli ya Mwenyezi Mungu: "Hiyo ni siku ya khasara" (Surat Taghabun: 9)[3]

## JUHUDI ZA DHATI KATIKA NJIA YA MAENDELEO

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Dunia ni saa moja, hivyo ifanyeni utii.**"[4]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Zitakayelingana sawia siku zake mbili basi kala hasara. Utakayekuwa mwisho wa siku zake ni mbaya basi ni mwenye kulaaniwa. Asiyejua nyongeza yoyote ndani ya nafsi yake basi yuko karibu mno na upungufu. Na atakayekuwa karibu mno na upungufu basi kifo kwake ni bora kuliko uhai**."[5] Kutathmini siku za ujana: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "Hautanyanyuka unyayo wa mja mbele ya Mola wake siku ya Kiyama mpaka aulizwe kuhusu mambo matano:

(a) Umri wake ameutumia katika kitu gani.
(b) Ujana wake ameutumia katika kitu gani.
(c) Mali yake aliipata vipi
(d) Na aliitumia vipi.
(e) Na alifanya nini kuhusu yale aliyokuwa na elimu nayo."[6]

---

1. Al-Khisal Uk. 509, hadithi ya 2.
2. Tanbihul-Khawatir Juz. 1, Uk. 37.
3. Iddatud-Daiy Uk. 103.
4. Biharul-An'war Juz. 70 Uk. 68, hadithi ya 14.
5. Al-Amaali cha As-Saduq, Uk. 766, hadithi ya 1030.
6. Sunan At-Tirmidhiy. Juz. 4, Uk. 612, hadithi ya 2416.

Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Hautanyanyuka unyayo wa mja mbele ya Mola wake siku ya Kiyama mpaka aulizwe kuhusu mambo manne:

(a)Umri wake ameutumia katika kitu gani.

(b) Ujana wake ameu- tumia katika kitu gani.

(c) Mali yake aliipata vipi.

(d) Na aliitumia vipi.

(e) Na kuhusu mapenzi yetu Ahlul-Bait."[1]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "Miongoni mwa mawaidha ya Luqman [(a.s)] kwa mwanae ni: 'Jua hakika wewe kesho utaulizwa mambo manne pindi utakaposimama mbele ya Mwenyezi Mungu:

(a) Ujana wako umeu- tumia katika kitu gani.

(b) Umri wako ameutumia katika kitu gani.

(c) Mali yako uliipata vipi.

(d) Na uliitumia vipi. Basi jiandae kwa hilo na liandalie majibu."[2]

## 2- USTAWI KATIKA KUJIJENGA

Utayarifu wa kijana katika kujijenga kiroho na kimwili: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "Nawausia kheri kwa vijana, kwani hakika wao ni wenye vifua vyepesi, Mwenyezi Mungu alinituma niwe mbashiri na muonyaji, vijana wakaniunga mkono, na wazee wakanipinga". Kisha akasoma kauli ya Mwenyezi Mungu: "Na muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu.." (Surat Yunus: 83).[3]

Imesemwa ndani ya Tafsiri Al-Qummiy kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: "Na walishangaa kwa kuwafikia mwonyaji anayetokana nao."(Surat Swad: 4):

Iliteremka Makka pindi Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alipodhihirisha Uislam, kwani makurayshi walijikusanya kwa Abu Talib na kumwambia: "Ewe Abu Talib! Bila shaka mwana wa ndugu yako kachafua ndoto zetu, katukana miungu yetu, kawaharibu vijana wetu na kavunja umoja wetu, basi ikiwa linalomsababisha kufanya hivyo ni ukata, sisi tutamkusanyia mali na kummilikisha mpaka awe mtu tajiri kuliko sisi". Basi Abu Talib akampa habari kuhusu hilo, akasema: "Wallahi lau wakiweka jua mkono wangu wa kushoto na mwezi mkono wangu wa kulia, sin- toitaka (mali hiyo)."[4]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Akili na upumbavu huendelea kumgombania mtu mpaka afikishapo miaka kumi na nane, akiifikia ndipo lenye nguvu zaidi kati ya hayo mawili hushinda.**"[5]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Ewe mwana wa ndugu yangu! Shikamana na vijana na achana na wazee.**"[6]

---

1. Al-Khisal Uk. 253, hadithi ya 125.
2. Al-Kafiy Juz. 2 Uk. 135, hadithi ya 20.
3. Shabab Quraysh, Uk. 1.
4.Tafsir Al-Qummiy, Juz. 2, Uk. 228.
5. Kanzul-Fawaid, Juz. 1 Uk. 200.
6. Alimwambia maneno haya Muhammad bin Abdullah bin Hasan (a.s). Al- Kafiy, Juz. 1, Uk. 362, hadithi ya 17.

Imepokewa ndani ya kitabu Al-Kafiy kutoka kwa Ismail bin Abdul-Khaliq amesema: "Abu Abdillah (a.s) alimwambia Abu Jafar Al-Ahwal nami nikiwa nasikia: 'Je, umekwenda Basra?' Akajibu ndio. Akasema: 'Umeonaje watu wanavyoharakisha kuingia na kulikubali jambo hili?' Akasema: 'Wallahi hakika ni wachache waliofanya hivyo, na hakika hilo ni kwa uchache.' Akasema: 'Shikamana na vijana, kwani hakika wao ni wepesi wa kuelekea kila kheri."[1]

Imepokeawa ndani ya kitabu Ilalus-Sharaiu kutoka kwa Ismail bin Al-Fadhlu Al-Hashimiy amesema: "Nilimwambia Jafar bin Muhammad (a.s), nipe habari kuhusu Yaqub (a.s) pindi wanae walipomwambia: "Ewe baba yetu! Tuombee msamaha kwa dhambi zetu, hakika sisi tulikuwa wenye makosa." Akasema: Nitakuombeeni msamaha kwa Mola wangu Mlezi, kwani Yeye ndiye Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu" (Surat Yusuf: 97-98). Akawa amechelewesha msamaha wao. Lakini Yusuf (a.s) walipomwambia: "Wakasema: Wallahi bila shaka Mwenyezi Mungu amekufadhilisha kuliko sisi, na hakika sisi tulikuwa wenye makosa. Akasema: Hakuna lawama juu yenu leo, Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwenye rehema zaidi kuliko wanaorehemu." (Surat Yusuf: 91 - 92). Akawaharakishia. Imam (a.s) akasema: 'Kwa sababu moyo wa kijana ni mwepesi kuliko moyo wa mzee, na jinai la watoto wa Yaqub lilikuwa ni dhidi ya Yusuf, na jinai yao dhidi ya Yaqub ni kwa kuwa walimfanyia jinai Yusuf, hivyo Yusuf akaharakisha kusamahe haki yake, na Yaqub akachelewesha msamaha, kwa sababu kusamehe kwake kulikuwa ni kusamehe haki ya mwingine, hivyo akachelewesha msamaha mpaka usiku wa Ijumaa."[2]

## NAFASI YA VIJANA KATIKA KUJIELIMISHA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayejifunza ujanani inakuwa kama nakshi kwenye jiwe. Na atakayejifunza ukubwani inakuwa kama kitabu juu ya maji.**"[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Jielimisheni mkingali wadogo itawanufaisheni ukubwani**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Asiyeibidisha nafsi yake udogoni basi hatopevuka kiakili ukubwani**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Upiteni ujana kwa midahalo na mijadala. Utu uzima kwa tafakari na uzee kwa ukimya**."[6]

Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "**Baba yangu mpendwa Zaynul-Abidiin alikuwa awaonapo vijana wanaotafuta elimu huwasogeza kwake na kuwaambia: "Karibuni! Ninyi ni hazina ya elimu, ninyi leo ni wadogo wa wengine, na mnakaribia kuwa wakubwa wa wengine**."[7]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Sipendi kumwona kijana miongoni mwenu ila akiwa amezama katika hali mbili: Ima msomi au mwenye**

---

1. Al-Kafiy, Juz. 8, Uk. 93, hadithi ya 66.
2. Ilalus-Sharaiu Uk. 54, hadithi ya 1.
3. An-Nawadir cha Ar-Rawandiy Uk. 132, hadithi ya 169.
4. Sharhu Nahjul-Balagha, Juz. 20, Uk. 267, hadithi ya 98.
5.Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8272.
6. Sharhu Nahjul-Balagha, Juz. 20, Uk. 285, hadithi ya 260.
7.Ad-Duru An-Nadhim fi manaqibil-Aimmatil-Lahamiym, Uk. 587.

**kujielimisha, na kama hatofanya hivyo basi kavuka mipaka, na akivuka mipaka kapoteza, na akipoteza katenda dhambi, na akitenda dhambi kaishi motoni. Naapa kwa yule aliyempa unabii Muhammad (s.a.w.w) kwa haki**."[1]

## MAFUNZO YA KIROHO

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hakika moyo wa kijana ni sawa na ardhi tupu, chochote kitachopandwa humo hukipokea, hivyo harakisha kujifunza adabu kabla moyo wako haujasusuka**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema alipokuwa akimuusia mwanae Imam Hasan (a.s): "**Na nikakusanya adabu yako ili uwe nayo ungali na umri mdogo, wenye akili, ukiwa na nia salama na nafsi safi.**"[3]

Imam Zaynul-Abidiin (a.s) amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliwakuta watu wakiinua jiwe, akawaambia: 'Kazi gani hii?' Wakamjibu: 'Tunataka kwayo tumjue ni nani mwenye nguvu kati yetu.' Akasema **(s.a.w.w)**: 'Je, niwaambieni ni nani mwenye nguvu kati yenu?' Wakasema ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema **(s.a.w.w)**: 'Mwenye nguvu kati yenu ni yule ambaye anaporidhia ridhaa yake haimwingizi katika dhambi wala batili. Anapokasirika kukasirika kwake

hakumzuii kusema haki, na anapokuwa na uwezo hatoi kisichokuwa haki."[4]

## MANABII (A.S) WALITUMWA WAKIWA VIJANA

Mwenyezi Mungu amesema: "Wakasema: Tulimsikia kijana mmoja akiwataja anaitwa Ibrahim." (Surat Anbiyai: 60).

Akasema tena: "Na alipofika (Musa) baleghe yake na akastawi, tulimpa hukumu na elimu na hivyo ndivyo tunavyowalipa watendao mema." (Surat Al- Qasas: 14).

Na amesema: "Na alipofika (Yusuf) baleghe yake, tulimpa hukumu na elimu na hivyo ndivyo tunavyowalipa watendao mema." (Surat Yusuf: 22).

Imam As-Sadiq (a.s) amesema kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu:

"Na alipofika (Musa) baleghe yake na akastawi, tulimpa hukumu na elimu": "Na alipofika (Musa) baleghe yake, yaani miaka kumi na nane. **Na akastawi, yaani alipoota ndevu.**"[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu hakumtuma Nabii yeyote ila alikuwa ni kijana.**"[6]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu hakumtuma Nabii yeyote ila alikuwa ni kijana, na msomi hakupewa elimu ila alikuwa ni kijana**."[7]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Enyi wana wa Abdul Muttalib! Hakika wallahi simjui kijana yeyote katika waarabu**

---

1. Al-Amaal cha Tus Uk. 303, hadithi ya 604.
2. Nahjul-Balagha, barua ya 31.
3. Nahjul-Balagha, barua ya 31.
4. Maanul-Akhbar Uk. 366.
5. Maanul-Akhbar, Uk. 226.
6. Kanzul-Umal, Uk. 11 Uk. 475, hadithi ya 32233.
7. Al-Firdawsu, Juz. 4, Uk. 82, hadithi ya 6254.

**aliyewaletea watu wake kitu bora kuliko nilichowaletea, kwani hakika mimi nime- waletea kheri ya dunia na Akhera**."[1]

Imam Mahdi [(a.s)] atadhihiri akiwa kijana: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwisho wa zama atasimama mtu kutoka ndani ya kizazi changu akiwa kijana mwenye uso mzuri na pua iliyochongoka, ataijaza ardhi uadilifu na usawa kama itakavyokuwa imejaa dhulma na ujeuri.**"[2]

Imam Hasan [(a.s)] amesema: "**Wa tisa kutoka katika kizazi cha ndugu yangu Husayn ni mwana wa bibi wa vijakazi, Mwenyezi Mungu atarefusha umri wake wakati wa ghaiba yake, kisha kwa uwezo wake atamdhihirisha akiwa katika sura ya ujana chini ya miaka arubaini, hilo ni ili Mwenyezi Mungu ajulikane kuwa ni Muweza juu ya kila kitu**."[3]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Lau angekuwa ametokeza Qaim basi watu wangemkanusha, kwa sababu atarejea kwao akiwa kijana aliyelingana**."[4]

Imepokewa ndani ya kitabu Kamalud-Din kutoka kwa Abu Swalti Al-Harawiy amesema: "Nilimwambia Ar-Ridha [(a.s)]: Ni zipi alama za Qaim kutoka kwenu pindi atakapodhihiri? Akasema: **'Alama yake ni kiumri awe mzee lakini ni kijana kimuonekano kiasi kwamba mtazamaji atadhania kuwa ni mtu wa miaka arubaini au chini yake**."[5]

## 3 - NAFASI YA VIJANA KATIKA SERIKALI YA

### BALOZI WA KWANZA WA MTUME (s.a.w.w) NI KIJANA

As'ad bin Zarara na Dhak'wan bin Abdu Qaysi walikuja kwa Mtume **(s.a.w.w)** Makka kabla ya kuhama kwake, na wao wawili walikuwa mabosi wa Madina, wakaingia kwa Mtume **(s.a.w.w)** wakati ambao Makka ilikuwa kipindi kigumu, wakasikiliza wito wake, kisha wakasilimu na kumwambia: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tupe mtu atakayetufunza Qur'an na kuwalingania watu katika jambo lako."[6]

Hii ilikuwa ndio mara ya kwanza Madina ambayo ilikuwa ni mji mkubwa wenye tofauti nyingi kuomba mwakilishi wa Mtume **(s.a.w.w)**, kama ambavyo ilikuwa ndio mara ya kwanza Mtume **(s.a.w.w)** kutuma mwakilishi wake rasmi nje ya Makka, hivyo ilipasa kwa ajili ya jukumu hili zito la hatari amtume mtu mwenye sifa na uwezo unaohitajika. Ndipo Mtume **(s.a.w.w)** akamteua Masw'ab bin Umayri, naye alikuwa kijana mwerevu.

Mtume **(s.a.w.w)** akampa maelekezo Masw'ab bin Umayri akiwa bado kijana kabisa na akamwamuru aende na As'ad, na Masw'ab alikuwa tayari ameshajifunza sehemu kubwa ya Qur'an.[7]

---

1. Al-Amaali cha Tus Uk. 583, hadithi ya 1206.
2. Uqad-Durar, Uk. 39.
3. Kamalud-Din Uk. 316, hadithi ya 2.
4. Biharul-An'war, Juz. 3 Uk. 301.
5. Kamalud-Din, Uk. 652, hadithi ya 12.
6. Biharul-An'war, Juz. 19, Uk. 10.
7. Biharul-An'war, Juz. 19, Uk. 10.

Akaondoka kijana huyu aliyejaa roho ya imani na ujana, akatekeleza jukumu lake na kusimamia kwa namna nzuri zaidi, haukupita muda mrefu watu wa Madina wakaukubali wito wake bila kujali tofauti zao, na hasa vijana na watoto wao, wakasilimu na Masw'ab akawaswalisha Swala ya Ijumaa, nayo ndio ya kwanza ya Ijumaa iliyoswaliwa Madina. Yeye ndiye wa kwanza aliyekusanya watu kwa ajili ya Ijumaa huko Madina, na mikononi mwake wakasilimu Asidu bin Hadhir na Saad bin Muadh. Hilo linatosha kuwa fahari na athari ndani ya Uisilamu.[1]

Imepokewa ndani ya kitabu Biharul-An'war: "**Masw'ab alifikia kwa As'ad bin Zurara, na alikuwa kila siku anatoka na kutembelea vikao vya mak- hazraji akiwalingania waingie kwenye Uislamu, na hapo vijana wanamkubali**."[2]

## GAVANA WA KWANZA WA MAKKA NI KIJANA WA MIAKA ISHIRINI NA MOJA

Baada tu ya Mtume **(s.a.w.w)** kulikomboa Jiji la Makka zikajitokeza alama za kuja vita vya Hunayni baada ya muda mfupi, hapo Mtume **(s.a.w.w)** hakuwa na jingine ila ni kuandaa jeshi lake na kulitenga nje ya Makka ili kujiandaa na mapambano. Upande mwingine alikuwa analazimika Makka ambayo punde tu ameikomboa kutoka mikononi mwa mushrikina, kuiachia gavana mwenye uwezo wa kuendesha mambo ipasavyo, na hasa ukizingatia wakati huo ilikuwa ndio kituo kikuu cha Bara la Uarabu na ndio mwelekeo wa macho ya makabila na watu wote kwa ujumla, zaidi ya hapo ni kuwa ugavana huu utazuia jaribio lolote la mushrikina la kuvunja amani na uhuru wa Makka.

Hivyo Mtume **(s.a.w.w)** akamteua kijana wa miaka ishirini na moja kwa ajili ya jukumu hili zito na la hatari, naye ni Uttab bin Usaydu, akamkabidhi na kumwandikia hati ya ugavana wake: "**Mtume (s.a.w.w) amempa ugavana Uttab bin Usaydu akiwa na umri wa miaka ishirini na moja, amempa utawala wa Makka na amemwamuru awasalishe watu. Naye ndiye gavana wa kwanza anayeswalisha jamaa Makka baada ya ukombozi wa Makka**."[3]

Kisha **(s.a.w.w)** akamwelekea Uttab na kumbainishia hatari ya jukumu hili zito akasema: "**Ewe Uttab! Unajua nimekupa utawala uwatawale kina nani? Nimekupa utawala uwatawale watu wa Mwenyezi Mungu, na laiti ningejua wana mtu mwenye kheri kuliko wewe basi ningempa awatawale.**"[4]

Katika hali ya kawaida ni lazima hati kama hii ingezua dukuduku la watu wa Makka na viongozi wao, ndipo Mtume **(s.a.w.w)** akaandika hati ndefu ili kuzuia upinzani wao, mwishoni akasema: "**Wala yeyote mwenye hoja miongoni mwenu asimwasi kwa hoja ya udogo wa umri, kwani mkubwa si mbora, bali mbora ndiye mkubwa.**"[5]

1. Usudul-Ghaba Juz. 5 Uk. 176, namba 4936.
2. Biharul-An'war, Juz. 19 Uk. 10.
3. As-Siratul-Halbiyah, Juz. 3, Uk. 104.
4. Usudul-Ghaba, Juz. 3, Uk. 549, hadithi ya 20.
5. Biharul-An'war, Juz. 21, Uk. 123, hadithi ya 20.

Uttab bin Usayd alibaki kama gavana wa Makka mpaka mwisho wa uhai wa Mtume **(s.a.w.w)**, na alitawala na kuongoza vizuri. Kiongozi wa vita vya Rum ni kijana wa miaka kumi na nane: Mtume **(s.a.w.w)** mwishoni mwa uhai wake aliandaa jeshi ili kuupiga utawala wa nchi kubwa ya Rum, wakajiunga na jeshi hili la waislamu sahaba wakubwa na watu maarufu miongoni mwa muhajirina na answari.

Na ni wazi kuwa ilikuwa inapasa jeshi hili aliweke chini ya uongozi wa viongozi wenye uwezo, hivyo akaliweka chini ya uongozi wa Usama bin Zaydi, na kipindi hicho alikuwa na umri wa miaka kumi na nane.[1]

Sahaba wakapinga uamuzi huu katika mazingira tete kama hayo,[2] wakatoa yaliyomo nyoyoni mwao na kutandaza ndimi zao kwa kusema: "Hivi kijana huyu anapewa uongozi juu ya muhajirina wa mwanzo?!!"[3] Mtume **(s.a.w.w)** alipolisikia hilo alitoka akichechemea mpaka mimbarini akiwa na ghadhabu, baada ya kumuhimidi na kumshukuru Allah akasema: "**Watu wamekosoa uteuzi wa uamiri wa Usama, na tayari walikuwa wamekosoa uteuzi wa uamiri wa baba yake kabla ya hapo, na hakika wao wawili wanafaa kabisa kwa uamiri huo, na wao wawili ni watu niwapendao sana, nawausia kheri kwa Usama**."[4]

## NAFASI YA VIJANA KATIKA SERIKALI YA IMAM WA ZAMA ZETU

1. Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Wafuasi wa Mahdi (a.s) ni vijana, hatokuwa na wazee ila kama wanja ndani ya jicho na chumvi kwenye mahitaji ya safari, na mahitaji machache mno ni chumvi**."[5]

2. Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Vijana wa Kishi'a watakuwa wamelala juu ya migongo ya mikeka yao, ghafla atawafikia Imam wao ndani ya usiku mmoja bila kutangulia ahadi, kisha wataamka wakiwa Makka.**"[6]

1. At-Tabaqatul-Kubra, Juz. 4, Uk. 66.
2. Mawsuuatul-Imam Ali bin Abi Talib, Juz. 2, Uk. 195 - 401.
3. At-Tabaqatul-Kubra, Juz. 2, Uk. 190.
4. At-Tabaqatul-Kubra, Juz. 2, Uk. 249. Sahih Bukhari, Juz. 3, Uk. 1365, hadithi ya 3524.
5. Al-Ghaybah cha Tus Uk. 476, hadithi ya 501.
6. Al-Ghaybah cha An-Nuumaniy Uk. 316, hadithi ya 11.

1

# JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA

# SEHEMU YA PILI

## SABABU ZINAZOPELEKEA USTAWI WA VIJANA

## 1- MAARIFA

### KUJIELIMISHA

Mwenyezi Mungu amesema: "Sema: Je wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua? Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu." (Surat Zumar: 9).

Amesema tena: "Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu na waliopewa elimu daraja za juu, na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayoyatenda." (Surat Mujadalah: 11).

Akasema tena: "Wala usifuate usiyo na elimu nayo, hakika masikio na macho na moyo, hivyo vyote vitaulizwa." (Surat Al-Israi: 36).

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hakuna harakati yoyote ila unahitajika uwe na maarifa nayo**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Enyi kundi la vijana! Jengeni ngome ya heshi- ma yenu kwa adabu, na dini yenu kwa elimu.**"[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mambo ya kwanza wanayopasa vijana kujifun- za ni yale ambayo pindi watakapokuwa watu wazima watayahitajia.**"[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Msiwalazimishe wanenu juu ya adabu zenu, kwani hakika wao wameumbwa kwa ajili ya zama zisizokuwa zama zenu**."[4]

### KUJITAMBUA

Mwenyezi Mungu amesema: "Na hakika tumewatukuza wanadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku katika vitu vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi wa wale tuliowaumba, kwa utukufu mkubwa." (Surat Al-Israi: 70).

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hekima bora kabisa ni mwanadamu kuitambua nafsi yake.**"[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayeitambua nafsi yake bila shaka amefikia kilele cha kila maarifa na elimu.**"[6]

---

1. Tuhaful-Uqul, Uk. 171.
2. Tarikhul-Yaaqubiy, Juz. 2, Uk. 210.
3. Sharhu Nahjul-Balagha, Juz. 20, Uk. 333, hadithi ya 817.
4. Sharhu Nahjul-Balagha, Juz. 20, Uk. 267, hadithi ya 102.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 3105.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8949.

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ujinga mkubwa ni mwanadamu kutojitambua yeye mwenyewe**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Asiyeitambua nafsi yake basi kajitenga mbali na njia ya uokovu, na kaangukia ndani ya upotovu na ujahili.**"[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Namshangaa mtu anayetambulisha na kukitafuta alichokipoteza, ilihali keshaipoteza nafsi yake na wala haitafuti**."[3] Imam Ali (a.s) amesema: "**Anayeitambua nafsi yake huipiga vita, na asiyeitambua huipuuza.**"[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayeitambua thamani ya nafsi yake hatoid- harau kwa vitu vya kupita (vya kutoweka).**"[5]

Imam Ali (a.s.) amesema: "**Atakayeitambua nafsi yake atamtambua Mola wake Mlezi.**"[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Namshangaa asiyeijua nafsi yake vipi atamtambua Mola wake Mlezi.**"[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwanadamu ameumbwa akiwa na nafsi itamkayo, akiitakasa kwa elimu na vitendo basi hufanana na johari za mwanzo wa kiini chake**"[8]

Abdalluh bin Sinan alimuuliza Imam Jafar As-Sadiq (a.s): "Je kati ya Malaika na mwanadamu ni nani bora?" Akasema: Jemedari wa waumini Ali bin Abu Talib amesema: 'Hakika Mwenyezi Mungu alimwekea Malaika akili bila matamanio, na akamwekea mnyama matamanio bila akili, na akamwekea mwanadamu vyote viwili, hivyo yule ambaye akili zake zitayashinda matamanio yake yeye ni bora kuliko Malaika. Na yule ambaye matamanio yake yataishinda akili zake yeye ni duni kuliko mnya- ma."[9]

## KUIJUA QUR'ANI TUKUFU

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayejifunza Qur'ani ujanani mwake basi itajichanganya na nyama yake na damu yake.**"[10]

Imam Ali (a.s) amesema ndani ya barua yake kwa mwanae Hasan (a.s): "**Na nikakuanza kwa kukufunza kitabu cha Mwenyezi Mungu na taawili yake, sheria za Uislamu na kanuni zake.**"[11]

Imam Jafar As-Sadiq (a.s) amesema: "**Atakayesoma Qur'ani angali kijana muumini basi Qur'ani itajichanganya na nyama yake na damu yake, na Mwenyezi Mungu atamweka pamoja na waandishi watukufu wachamungu, na Qur'ani itakuwa kinga yake siku ya Kiyama.**"[12]

---

1. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 2936.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 9034.
3. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 6266.
4. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 7855 na 7856.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8628.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 7946.
7. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 6270.
8. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5884. Biharul-An'war, Juz. 40 Uk. 165, hadithi ya 54.
9. Ilalus-Sharaiu, Uk. 4.
10. Kanzul-Ummal, Juz. 1 Uk. 532, hadithi ya 2381.
11. Nahjul-Balagha, barua ya 31.
12. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 603, hadithi ya 4.

### KUJIFUNZA DINI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Kila kitu kina nguzo, na nguzo ya dini hii ni elimu ya sharia (Fiqhi)**."[1]

Imam Al-Baqir na As-Sadiq (a.s) wamesema: "**Lau kama nikiletewa kijana yeyote miongoni mwa vijana wa Kishi'a asiyejifunza sharia basi nitamwadabisha.**"[2]

Imam Al-Baqir (a.s) alikuwa akisema: "**Jifunzeni sharia, la sivyo ninyi ni mabedui.**"[3]

Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "**Lau kama nikiletewa kijana miongoni mwa vijana wa Kishi'a hajifunzi sharia ya dini basi nitamtia machungu.**"[4]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Lau kama nikiletewa kijana miongoni mwa vijana wa Kishi'a hajifunzi sharia basi nitairekebisha adabu yake.**"[5]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Harakisheni kuwafunza vijana wenu Hadith kabla Murjia hawajawatangulia kwao.**"[6]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Sipendi kumwona kijana miongoni mwenu ila akiwa amezama katika hali mbili: Ima msomi au mwenye kujie- limisha, na kama hatofanya hivyo basi kavuka mipaka, na akivuka mipaka kapoteza, na akipoteza katenda dhambi, na akitenda dhambi kaishi motoni. Naapa kwa yule aliyempa unabii Muhammad (s.a.w.w) kwa haki.**"[7]

Kutambua kwamba elimu na imani ni mapacha: Mwenyezi Mungu amesema: "Mwenyezi Mungu na Malaika na wenye elimu, wameshuhudia kuwa hakuna aabudiwaye ila Yeye tu, ni Mwenye kusimamia uadilifu. Hakuna aabudiwaye isipokuwa Yeye tu, Mwenye nguvu, Mwenye hekima." (Surat Imraan: 18).

Akasema tena: "Na waliopewa elimu wanafahamu ya kuwa yale yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ndiyo haki, nayo huongoza kwenye njia ya Mwenye nguvu, Mwenye kusifiwa." (Surat Sabai: 6). Akasema: "Na ili wajue wale waliopewa elimu ya kwamba hiyo ni haki iliyotoka kwa Mola wako na waiamini, na zinyenyekee Kwake nyoyo zao. Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ndiye awaongozaye wale walioamini kwenye njia iliyonyooka." (Surat Al-Hajji: 54).

Imam Ali (a.s) amesema: "**Asili ya imani ni elimu.**"[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Imani na elimu ni mapacha na marafaki wawili wasiotengana.**"[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Matunda ya elimu ni kumtambua Mwenyezi Mungu.**"[10]

---

1.Biharul-An'war, Juz. 1 Uk. 216, hadithi ya 30.
2. Al-Mahasin Juz. 1 Uk. 357, hadithi ya 760.
3. Al-Mahasin Juz. 1 Uk. 357, hadithi ya 760.
4. Al-Mahasin Juz. 1 Uk. 357, hadithi ya 761.
5. Daaimul-Islam Juz. 1 Uk. 80.
6. Tahdhibul-Ahkam Juz. 8 Uk. 111, hadithi ya 381.
7. Al-Amaali cha Tus Uk. 303, hadithi ya 604.
8. Biharul-An'war, Juz. 93, Uk. 57.
9. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1785.
10.Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4586.

Imam Kadhim (a.s) alimwambia Hisham bin Al-Hakam: "**Ewe Hisham! Mwenyezi Mungu hakupeleka mitume Wake na Manabii Wake kwa waja Wake ila ni ili wawaelimishe kuhusu Mwenyezi Mungu, hivyo wenye kuwakubali vizuri ni wale wenye maarifa mazuri**."[1]

## UMUHIMU WA UDADISI

Mwenyezi Mungu anasema: "Basi waulizeni wenye ukumbusho ikiwa nyinyi hamjui." (Surat Annahli: 43).

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Elimu ni hazina na ufunguo wake ni udadisi, basi ulizeni Mwenyezi Mungu atawarehemu. Kwa hakika hulipwa watu wa namna nne: Muulizaji, mzungumzaji, msikilizaji na mwenye kuwapenda.**"[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayeuliza udogoni mwake atajibu ukubwani mwake**."[3]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema alipoulizwa na Humran bin Aayan: "**Hakika watu huangamia kwa kuwa hawaulizi**."[4]

Imepokewa kutoka kwa Imam As-Sadiq (a.s) kuwa: "Mtume **(s.a.w.w)** aliambiwa kuwa kuna mtu alipatwa na janaba akiwa na jeraha, akaamrishwa kuoga ndipo akakaukia na hatimaye akafariki." Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akasema: "**Wallahi wamemuuwa, Mwenyezi Mungu awauwe. Hakika dawa ya kushindwa ilikuwa ni kuuliza**."[5]

Imepokewa ndani ya kitabu Musnad Ahmad bin Hanbal kutoka kwa Abu Umamah amesema: "Kuna kijana alimjia Mtukufu Mtume **(s.a.w.w)** na kumwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Naomba unipe idhini ya kuzini.' Hapo watu wakamvamia na kumfokea na kumwambia: 'Nyamaza, nyamaza.' Mtume akasema: 'Msogezeni.' Basi akasogezwa karibu yake kisha akaketi. Mtume akamwambia: 'Unalipenda hilo kwa mama yako?' Kijana akasema: 'La wallahi, Mwenyezi Mungu anifanye fidia kwako!' Akasema: 'Na watu hawalipendi kwa mama zao.' Akasema: "Unalipenda hilo kwa binti yako?' Kijana akasema: "La wallahi, Mwenyezi Mungu anifanye fidia kwako! Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.'

Akasema: 'Na watu hawalipendi kwa mabinti zao.' Akasema: 'Unalipenda hilo kwa shangazi yako?' Kijana akasema: 'La wallahi, Mwenyezi Mungu anifanye fidia kwako!' Akasema: 'Na watu hawalipendi kwa shangazi zao.' Akasema: 'Unalipenda hilo kwa mama zako wadogo?' Kijana akasema: 'La wallahi, Mwenyezi Mungu anifanye fidia kwako!' Akasema: "Na watu hawalipendi kwa mama zao wadogo.' Mtume akaweka mkono juu ya bega lake na kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu! Msamehe dhambi yake, safisha moyo wake, na uhifadhi utupu wake." Basi baada ya hapo kijana hakuwa tena akifikiria hilo."

1. Al-Kafiy, Juz. 1, Uk. 16, hadithi ya 12.
2. Tuhfalul-Uqul, Uk. 41.
3. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8273.
4. Al-Kafiy, Juz. 1, Uk. 40, hadithi ya 2.
5. Al-Kafiy, Juz. 3, Uk. 68, hadithi ya 4.

## 2 - AZMA

Imam Ali (a.s) amesema: "**Lakini Mwenyezi Mungu amewapa Mitume Wake nguvu katika azma zao, na udhaifu katika kile kinachoonwa na macho yao katika hali zao**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Pambaneni na ulegevu kwa azma**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Azma na walima havikai pamoja, hakuna kiondoacho usingizi kama azma za siku, na kifutacho giza kama kukumbuka hima**."[3]

Imam Al-Kadhim (a.s) amesema katika moja ya dua zake za mwezi wa Rajab: "**Na nimejua kuwa matumizi bora ya msafiri ajaye Kwako ni azma ya utashi unaokuchagua Wewe**."[4]

### KUJITUMA

Mwenyezi Mungu asema: "Na kwamba mtu hatapata ila yale aliyoyafanya. Na kwamba amali yake itaonekana." (Surat Najmu: 39 - 40).

Na akasema tena: "Na wale wanaojitahidi kwa ajili yetu, lazima tutawaongoza kwenye njia zetu." (Surat Ankabut: 69).

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayedumu kugonga mlango ataingia**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayedumu kugonga mlango na kukazana ataingia**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "Atakayetoa juhudi za nguvu zake atafikia asili ya muradi wake."[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayekitafuta kitu kwa juhudi atakipata chote au sehemu yake.**"[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Kamwe haiwezekani kupata ufanisi kwa kujib- wetesha na urahisi.**"[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ukikumbana na jambo liingie, kwani hakika ugumu wa kujiepusha nalo ni mkubwa kuliko yale unayokhofia toka humo.**"[10]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ukiogopa ugumu wa jambo basi jitume kwalo litakuwa jepesi kwako. Na udanganye wakati kuhusu matukio yake basi yatakuwa mapesi kwako**."[11]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Zamani nilikuwa na ndugu katika dini ya Mwenyezi Mungu.alikuwa dhaifu aliyedhoofishwa, lakini juhudi zinapokuja huwa simba dume na nyoka swila**."[12]

---

1. Nahjul-Balagha, hotuba ya 192.
2. Uyunul-Hikam Wal-Mawaidh, Uk. 310, hadithi ya 5454.
3. Nahjul-Balagha, hotuba ya 241.
4. Al-Iqbal, Juz. 3 Uk. 277.
5. Kanzul-Fawaid. Juz. 1, Uk. 139.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 9160.
7. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8785.
8. Nahjul-Balagha, hekima ya 386.
9. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 10028.
10. Nahjul-Balagha, hekima ya 175.
11.Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4108.
12. Nahjul-Balagha, hekima ya 289.

## MALENGO YA JUU

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ambaye malengo yake yatakuwa ya juu basi thamani yake itaongezeka**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Kuwa mwenye malengo ya mbali pindi utafutapo**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayelikeshesha jicho la fikira zake basi atafikia asili ya lengo lake**."[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hakuna kitu kimwinuacho mtu kama lengo lake, na hakuna kimbwagacho kama matamanio yake**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Apandaye daraja za malengo basi mataifa humkweza**."[5]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Matatu humzuia mtu kutafuta yaliyo juu: Ufupi wa lengo, uchache wa mbinu na udhaifu wa mawazo**."[6]

## KUJIHESHIMU

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ijengee nafsi yako heshima kwa kujiepusha na mambo duni, hata kama yatakusukuma kwenye raghba, kwani hakuna sehemu yoyote ya dini yako na heshima yako uitowayo yenye mbadala wa thamani, hata iwaje**."[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ijengee nafsi yako heshima kwa kujiepusha na mambo duni, hata kama yatakusukuma kwenye raghba, kwani hakuna sehemu yoyote ya nafsi yako uitowayo yenye mbadala wa heshima**."[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Bora kifo kuliko udhalili, bora ufakiri kuliko ombaomba**."[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Bora ufakiri kuliko udhalili**."[10]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Atakaye heshima bila jamaa, utajiri bila mali na haiba bila utawala, basi atoke kwenye udhalili wa kumwasi Mwenyezi Mungu mpaka kwenye heshima ya kumtii**."[11]

Kujitosheleza: Imepokewa ndani ya kitabu Al-Khiswal kutoka kwa Sahlu bin Saad amesema: "**Jibril alikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na kumwambia: 'Jua hakika sharafu ya mtu ni kusimama usiku, na heshima yake ni kutokuwahitajia watu**."[12]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayejua thamani ya nafsi yake basi vitu vya kupita havitomdhalilisha**."[13]

---

1. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8320, 7161, 8784.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8320, 7161, 8784.
3. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8320, 7161, 8784.
4. Uyunul-Hikam Wal-Mawaidh Uk. 484, hadithi ya 8928.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8526.
6. Tuhaful-Uquul, Uk. 318.
7. Biharul-An'war, Juz. 77, Uk. 206.
8. Nahjul-Balagha, barua ya 31.
9. Nahjul-Balagha, hekima ya 396.
10. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 362.
11. Al-Khiswal, Uk. 160, hadithi ya 222.
12. Al-Khiswa,l Uk. 7, hadithi ya 20.
13. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8628.

Imam Ali (a.s) amesema: "**Utajiri mkubwa ni kutojali yaliyomo mikononi mwa watu.**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Udhalili ni kuwaomba watu**."[2]

Imam Zaynul-Abidina (a.s) amesema: "**Kheri yote nimeiona imekusanyika kwenye kuacha za tamaa dhidi ya yale yaliyomo mikononi mwa watu**."[3]

## MSIMAMO

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayeshikamana na msimamo basi usalama utashikamana naye**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Jueni kuwa Mwenyezi Mungu huwachukia waja wake wasio na msimamo, hivyo msiteleze nje ya haki na wilaya ya Ahlul-Baiti, kwani kwa hakika atakaeleta mbadala dhidi yetu basi kaangamia**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Shikamana na mfumo wa msimamo, kwani wenyewe utakuletea heshima na kukulinda dhidi ya lawama**."[6]

## KUMTAWAKALI MWENYEZI MUNGU

Mwenyezi Mungu amesema: "Utakapoazimia basi mtegemee Mwenyezi Mungu" (Surat Ali Imran: 159).

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayemtawakali Mwenyezi Mungu basi atamtosheleza matumizi yake na kumruzuku kwa namna asiyotarajia**."[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Yeye ndiye Ambaye atakayemtawakali humtosheleza na atakaemuomba humpa**."[8]

Imam Jawad (a.s) amesema: "**Kumtegemea Mwenyezi Mungu ni thamani ya kila ghali na ngazi ya kuelekea heshima ya juu**."[9]

Imepokewa ndani ya kitabu Kanzul Fawaid kuwa: "**Miongoni mwa hekima na usia wa Luqman (a.s) kwa mwanae ni: 'Ewe mwanangu mpendwa! Mtegemee Mwenyezi Mungu, kisha waulize watu: Je, kuna yeyote kamtegemea Mwenyezi Mungu kisha hajamwokoa?! Ewe mwanangu mpendwa! Mtawakali Mwenyezi Mungu, kisha waulize watu: Ni nani aliyemtawakali Mwenyezi Mungu kisha hajamtosheleza?!**"[10]

---

1. Nahjul-Balagha, hekima ya 342.
2. Uyunul-Hikam Wal-Mawaidh, Uk. 17, hadithi ya 11.
3. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 148, hadithi ya 3.
4. Kanzul-Fawaid, Juz. 1 Uk. 280.
5. Al-Khiswal, Uk. 626.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 6127.
7. Kanzul-Ummal, Juz. 3 Uk. 103, hadithi ya 5693.
8. Nahjul-Balagha, hotuba ya 90.
9. Ad-Durratu Al-Bahirah, Uk. 40.
10. Kanzul-Fawaid, Juz. 2, Uk. 66.

2

# JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA

## 3 - UHUSIANO NA MWENYEZI MUNGU

### THAMANI YA IBADA KATIKA KIPINDI CHA UJANA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ubora wa kijana ambaye anajishughulisha na ibada ujanani juu ya mzee ambaye anajishughulisha na ibada baada ya miaka yake kukua ni sawa na ubora wa Mitume juu ya watu wengine**."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu asema: 'Kijana mwenye kuamini kadari Yangu, mwenye kuridhia Kitabu Changu, mwenye kutosheka na riziki Yangu na mwenye kuachana na mata- manio yake kwa ajili Yangu, yeye Kwangu ni sawa na baadhi ya malaika Wangu**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika Mwenyezi Mungu humpenda kijana ambaye anaumaliza ujana wake katika kumtii Mwenyezi Mungu**."[3]

Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "**Ibrahim aliamka akaona mvi moja kwenye ndevu zake, akasema: 'Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, Ambaye amenifikisha kiwango hiki huku nikiwa sijamwasi Mwenyezi Mungu hata kidogo**."[4]

Mwenyezi Mungu hujifakharisha kupitia ibada ya kijana: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika Mwenyezi Mungu hujifakharisha kwa malaika kupitia kijana mfanya ibada, huwaambia: Mtazameni mja Wangu! Ameacha matamanio yake kwa ajili Yangu**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakuna kijana yeyote anayeacha ladha ya dunia na matamanio yake, na kuelekea kumtii Mwenyezi Mungu kwa ujana wake ila ni lazima Mwenyezi Mungu atam- pa ujira wa wasema kweli sabini na mbili**."

Kisha akasema: '**Mwenyezi Mungu husema: Ewe kijana mwenye kuacha matamanio yake kwa ajili Yangu, mwenye kuutumia ujana wake kwa ajili Yangu, wewe kwangu ni sawa na baadhi ya malaika wangu**."[6]

Imam As-Swadiq (a.s) amesema: "**Kiumbe apendwaye sana na Mwenyezi Mungu ni kijana chipukizi wa miaka aliye katika sura nzuri, ambaye ameuweka ujana wake na uzuri wake katika kumtii Mwenyezi Mungu. Huyo ndiye ambaye Mwenyezi Mungu hujifakharisha mbele ya malaika kupitia yeye kwa kuwaambia: Huyu ndiye mja Wangu kweli**."[7]

---

1. Kanzul-Ummal, Juz. 15, Uk. 776, hadithi ya 43059.
2. Kanzul-Ummal, Juz. 15, Uk. 786, hadithi ya 43107. Rejea hadithi ya 124.
3. Kanzul-Ummal, Juz. 15, Uk. 776, hadithi ya 43060.
4. Al-Kafiy, Juz. 8 Uk. 392, hadithi ya 588.
5. Kanzul-Ummal, Juz. 15, Uk. 776, hadithi ya 43057.
6. Hilyatul-Awliyai, Juz. 4 Uk. 139.
7. Iilamud-Din, Uk. 120.

## BARAKA ZA IBADA YA UJANANI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakaemwabudu Mwenyezi Mungu kwa ufanisi ujanani mwake, Mwenyezi Mungu atampa hekima ujanani**. Mwenyezi Mungu asema: "Na alipofikia baleghe yake na akastawi, tulimpa hukumu na elimu na hivyo ndivyo tunavyowalipa wenye kufanya mema." (Surat Al-Qasas: 14).

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Watu wa aina saba Mwenyezi Mungu atawafunika kwa kivuli chake siku ambayo hakuna kivuli ila kivuli Chake tu: Imam mwadilifu na kijana aliyekulia katika ibada ya Mwenyezi Mungu..**"[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Chipukizi yeyote atakayekulia katika elimu na ibada mpaka akawa mtu mzima, Mwenyezi Mungu atampa siku ya Kiyama thawabu za wasema kweli sabini**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ewe Abu Dhari! Hakuna kijana yeyoye anayeiacha dunia na matamanio yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kuumaliza ujana wake katika kumtii Mwenyezi Mungu ila ni lazima Mwenyezi Mungu atampa ujira wa wasema kweli sabini na mbili**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mbora katika umma wangu ni yule mwenye kuuponda ujana wake katika kumtii Mwenyezi Mungu, na kuitenga nafsi yake na ladha za dunia na kuifunganisha na akhera, hakika malipo yake juu ya Mwenyezi Mungu ni daraja ya juu kabisa ya Pepo**."[4]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Watu wa aina tatu Mwenyezi Mungu atawaingiza peponi bila hesabu..Imam mwadilifu, mfanyabiashara mkweli na mzee aliemaliza umri wake katika kumtii Mwenyezi Mungu**."[5]

## MAANA YA IBADA

Imepokewa ndani ya kitabu Muhjjatul-Baydhai kuwa: "**Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungun (s.a.w.w) alikuwa ameketi na sahaba zake, akam- tazama kijana shupavu mwenye nguvu ametangulia akitembea kwa juhudi, wakasema: 'Tazama huyu, kwa nini asiutumie ujana wake na ushupavu wake katika njia ya Mwenyezi Mungu?' Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: 'Msiseme hivyo, kwani ikiwa yeye anafanya juhudi kwa ajili ya nafsi yake ili aizuie isiombeombe na isiwahitajie watu, basi yeye yupo katika njia ya Mwenyezi Mungu. Na ikiwa anafanya juhudi kwa ajili ya wazazi wake wawili madhaifu au kizazi chake dhaifu ili awatosheleze na kuwatimizia mahitaji yao, basi yeye yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu. Na ikiwa anafanya juhudi**

---

1. Al-Khiswal, Uk. 343, hadithi ya 7.
2. Maniyatul-Murid, Uk. 104.
3. Al-Aamaliy cha At-Tusi Uk. 535, hadithi ya 1162.
4. Al-Mawaidh Al-Adadiyyah, Uk. 34.
5. Al-Khiswal, Uk. 80, hadithi ya 1.

**ili ajifakharishe na kujigamba kwa wingi wa mali, basi yeye yupo katika njia ya shetani**."[1]

### WASTANI KATIKA IBADA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Dini hii ni nzito, basi iingieni kwa wepesi, wala msilazimishe ibada za Mwenyezi Mungu kwa waja wa Mwenyezi Mungu, mkaja kuwa kama mpandaji aliyepanda ambaye hana safari aliyoisafiri wala mgongo alioubakisha**."[2]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Nilifanya juhudi katika ibada nami nikiwa bado kijana, ndipo baba yangu akaniambia: 'Ewe Mwanangu mpendwa! Punguza ninachokuona ukifanya, kwani hakika Mwenyezi Mungu ampendapo mja humridhia kwa kichache**."[3]

## 4 - RAFIKI MWEMA

### NAFASI YA RAFIKI MAISHANI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mtu huwa katika dini ya rafiki yake, basi mmoja wenu achunguze ni yupi anayemfanya kuwa rafiki yake**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Aliye madhubuti ni yule mwenye kupata kheri kwa urafiki wake, kwani hakika mtu hupimwa kupitia rafiki yake**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Urafiki una majuto ila kwa walio wachamungu**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Rafiki wa mtu ni dalili ya akili yake**."[7]

Imepokewa kuwa Sulayman (a.s) alisema: "**Msimhukumu mtu kwa chochote mpaka mchunguze husuhubiana na nani, kwani hakika mtu hujulikana kupitia wenzi wake na marafiki wake, na hunasibishwa kwa sahiba zake na wapambe wake**."[8]

### KUMJARIBU RAFIKI

Imam Ali (a.s) amesema: "**Kumwamini kila mtu kabla ya kumjaribu ni dalili ya kushindwa**."[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Tangulizeni majaribio na fanyeni juhudi katika uchunguzi wakati wa kuchagua ndugu, la sivyo utalazimika kufanya urafi- ki na waovu.**"[10]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Akili za watu hujaribiwa kwa mambo sita: Urafiki, muamala, utawala, kuvuliwa madaraka, utajiri na ufakiri**."[11]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Watu hawajulikani ila kwa majaribio, basi mjaribu mkeo na wanao katika ghaibu yako, rafiki yako katika msiba**

---

1. Al-Muhujjatul-Baydhai, Juz. 3, Uk. 140.
2. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 86, hadithi ya 1.
3. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 87, hadithi ya 5.
4. Al-Amal cha Tus Uk. 518, hadithi ya 1135.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 2026.
6. Biharul-An'war, Juz. 69, Uk. 237, hadithi ya 4.
7. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5088.
8. Biharul-An'war, Juz. 74 Uk. 188, hadithi ya 17.
9. Nahjul-Balagha, hekima ya 384.
10. Ghurarul-Hikam, hekima ya 6711.
11. Ghurarul-Hikam, hekima ya 5600.

**wako, mwenye ukaribu na wewe katika ukata wako na mwenye mapenzi na wewe wakati wa kutengana naye, ili ujue ni ipi nafasi yako kwao**."[1]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Msimuone mtu kuwa ni rafiki mpaka mumjaribu kwa mambo matatu: "Mghadhibishe uone ghadhabu zake je zitamtoa kwenye haki hadi kwenye batili, na wakati wa dinari na dirhamu (Dola na shilingi), na mpaka usafiri naye**."[2]

## AINA ZA MARAFIKI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Zama za mwisho kutakuwa na watu, wao ni marafiki kwa nje na maadui kwa ndani." Akaambiwa: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hiyo inakuwaje?' Akasema: 'Hiyo ni kwa kupendana wao kwa wao na kuogopana wao kwa wao.**"[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Marafiki zako ni wa aina tatu na maadui zako ni wa aina tatu: Marafiki zako ni rafiki yako, rafiki wa rafiki yako na adui wa adui yako. Na maadui zako ni adui yako, adui wa rafiki yako na rafiki wa adui yako**."[4]

Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "**Mtu mmoja huko Basra alisimama kwa kiongozi wa waumini na kumwambia: 'Ewe kiongozi wa waumini tupe habari kuhusu ndugu.' Akasema: 'Ndugu wana namna mbili: Ndugu wa kweli na ndugu wa uongo. Ama ndugu wa kweli wao ndio uwezo, rafiki, ndugu na mali. Ukiwa na imani na ndugu yako basi jitolee kwake mali yako na mwili wako, msafie nia aliyemsafia nia na mfanyie uadui aliyemfanyia uadui, mfichie siri yake na aibu yake na mdhihirishie wema. Na jua ewe muulizaji hakika wao ni wachache kuliko madini ya kibiriti chekundu. Ama ndugu wa uongo, hakika wewe utapata ladha yako (manufaa) kutoka kwao, hivyo usilikatishe hilo kutoka kwao, na wala usitafute yaliyo nyuma ya hayo kutoka katika dhamiri zao, na wape ucheshi wa uso na utamu wa ulimi kama walivyokupa**."[5]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Ndugu wana namna tatu: Mmoja ni kama chakula ambaye anahitajika kila wakati, naye ni yule mwenye akili. Wa pili ni sawa na ugonjwa naye ni yule mpumbavu. Na wa tatu ni sawa na dawa naye ni yule mwerevu**."[6]

## MARAFIKI BORA

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: "**Ndugu bora ni yule mwenye kukusaidia katika amali za Akhera**."[7]

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: "**Aliye bora kati ya ndugu zako ni yule anayekusaidia katika kumtii Mwenyezi Mungu,**

---

1. Biharul-An'war, Juz. 78, Uk. 10, hadithi 68.
2. Al-Amal cha Tus Uk. 646, hadithi ya 1339.
3. Musnad Ahmad bin Hanbal, Juz. 8, Uk. 244, hadithi ya 22116.
4. Nahjul-Balagha, hekima ya 295.
5. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 248, hadithi ya 3.
6. Tuhaful-Uquul, Uk. 323.
7. Tanbiihil-Khawatir, Juz. 2, Uk. 123.

**anayekuzuia kumwasi Mwenyezi Mungu na anayekuamuru kumridhisha**."[1]

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: "**Mbora kati ya ndugu zenu ni yule mwenye kuwazawadieni (kukujulisheni) aibu zenu**."[2]

Alipoulizwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni yupi aliye mbora kukaa naye? Akasema: "**Ni yule ambaye kumtazama kwake kunawakumbusha Mwenyezi Mungu, kuongea kwake kunawaongezea elimu na matendo yake yanawakumbusha Akhera**."[3]

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: "**Wanafunzi wa Isa walimuuliza: 'Ewe roho wa Mwenyezi Mungu, tukae na nani?' Akasema: 'Yule ambaye kumtazama kwake kunawakumbusha Mwenyezi Mungu, kuongea kwake kunawaongezea elimu, na matendo yake yanawaraghibisha Akhera**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ndugu bora ni yule aliye mchache wa hadaa katika nasaha**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ndugu bora ni yule ambaye mapenzi yake ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ubora wa kila kitu ni upya wake, na ndugu bora ni wa zamani**."[7]

Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "**Mfuate anaekuuliza ilihali akikunasihi, wala usimfuate anayekuchekesha ilihali akikuhadaa**."[8]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Shikamana na rafiki wa zamani kwani kila mpya hana ahadi na uaminifu, wala dhima na mkataba. Na chukua tahadhari sana dhidi ya yule uliye na imani naye sana, kwani watu ni maadui wa neema**."[9]

Imam Al-Askar (a.s) amesema: "**Ndugu aliye bora kwako ni yule aliyesa- hau makosa yako na akakumbuka ihsani yako kwake**."[10]

Imam Hasan (a.s) amesema: "Mtume **(s.a.w.w)** aliulizwa: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni yupi rafiki bora?' Akajibu: 'Rafiki ambaye unapomkumbuka Mwenyezi Mungu anakusaidia na unapomsahau anakukumbusha.' Wakamwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, tuonyeshe aliye mbora kwetu ili tumfanye rafiki na mtu wa kukaa naye.' Akasema: 'Ndio, yule ambaye akitazamwa Mwenyezi Mungu hukumbukwa."[11]

---

1. Tanbiihil-Khawatir, Juz. 2, Uk. 123.
2. Tanbiihil-Khawatir, Juz. 2, Uk. 123.
3. Al-Amal cha Tus Uk. 157, hadithi ya 262.
4. Tuhaful-Uqul, Uk. 44.
5. Ghurarul-Hikam, hekima ya 4987.
6. Ghurarul-Hikam, hekima ya 5017.
7. Ghurarul-Hikam, hekima ya 5089.
8. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 638, hadithi ya 2.
9. Al-Kafiy, Juz. 8, Uk. 249, hadithi ya 350.
10. Aalamud-Din, Uk. 313.
11. Al-Ikhwani cha Ibnu Abu Dunya Uk. 123, hadithi ya 42.

### HAKI YA MWENZI WAKO

Imam Zaynul-Abidina (a.s) amesema: "**Ama haki ya mwenzi wako uliyekaa naye ni uwe mpole kwake na kumfanyia insafu katika utamshi wa lafudhi. Usisimame toka ulipokaa ila kwa idhini yake, na aliyekaa kwako anaruhusiwa kusimama toka kwako bila idhini yako. Sahau makosa yake na hifadhi kheri zake na wala usimsikilizishe ila kheri**."[1]

## 5 - MAHITAJI YA HALALI NA NGUVU ZA MWILI

### NGUVU ZA MWILI ZASIFIWA

Mwenyezi Mungu amesema: "Na Nabii wao akawaambia: Hakika Mwenyezi Mungu amewawekea Taalut kuwa ni mfalme juu yenu. Wakasema: 'Atakuwaje yeye na ufalme juu yetu na sisi tuna haki zaidi ya ufalme kuliko yeye wala hakupewa wasaa wa mali?' Akasema: Hakika Mwenyezi Mungu amemchagua juu yenu na amemzidishia wasaa wa elimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu huumpa ufalme wake amtakaye na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa Mwenye kujua." (Al-Baqarah: 247).

Mwenyezi Mungu amesema tena: "Ewe Yahya! Shika Kitabu kwa nguvu, na tukampa hekima angali mtoto." (Surat Maryam: 12).

Imepokewa kutoka kwa Is'haqa bin Ammar amesema: "Nilimuuliza Abu Abdullah kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: "Chukueni tulichowapa kwa nguvu." Je ni nguvu za mwili au nguvu za roho? Akasema: '**Ni zote mbili**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ni uzuri kwa aliyesil- imu maisha yake yawe yamtosheleza na nguvu yake iwe imara**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Muumini mwenye nguvu ni bora kuliko muumini dhaifu, na katika kila kheri**."[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ndani ya sahifa ya Ibrahim mlikuwa na: 'Na mwenye akili anapokuwa hajashindwa kiakili awe na saa: Saa humo anamnong'oneza Mola wake Mlezi. Saa anaitath- mini nafsi yake. Saa humo anatafakari kuhusu ihsani aliyofanyiwa na Mwenyezi Mungu na saa anakaa faragha na kuiepusha nafsi yake na halali, kwani saa hii ni msaada wa saa zile na ni kuuimarisha moyo na kuupumzisha**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Inapasa kwa mwenye akili ikiwa kweli ana akili awe na saa nne mchana: Saa humo anamnong'oneza Mola wake Mlezi. Saa anaitathmini nafsi yake. Saa anawaen- dea wenye elimu na wanamfumbua macho katika dini yake na kumnasihi na saa anakaa faragha na kuiepusha nafsi yake na ladha miongoni mwa mambo ya dunia, yaliyo halali na jamali**."[6]

---

1. Al-Khiswal, Uk. 569.
2. Tafsirul-Ayaash, Juz. 1, Uk. 45, hadithi ya 52.
3. An-Nawadir, cha Ar-Rawandiy Uk. 90, hadithi ya 23.
4. Sahih Muslim, Juz. 4, Uk. 2052, hadithi ya 34.
5. Al-Khiswal, Uk. 525, hadithi ya 13.
6. Rawdhatul-Waaidhina, Uk. 8.

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ewe Mola Mlezi! Ewe Mola Mlezi! Vipe viun- go vyangu nguvu katika kukutumikia, na imarisha azima yangu**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Muumini ana saa tatu: Saa humo anamnong'oneza Mola wake Mlezi. Saa anatafuta maisha yake na saa anaie- pusha nafsi yake na ladha zilizo halali na jamali**."[2]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Na miongoni mwa hekima za jamaa wa Daud ilikuwa ni: Ni lazima kwa mwislamu mwenye akili awe na saa anayoimalizia kati yake na Mwenyezi Mungu kwa amali. Saa anakutana na ndugu zake anaowazunguka na wanaomzunguka katika jambo la Akhera yake. Na saa anaiepusha nafsi yake na ladha katika mambo yasiyo ya hara- mu, kwani yenyewe ndio msaada kwa saa hizo nyingine**."[3]

Imam Al-Kadhim (a.s): "**Jitahidini katika zama zenu muwe na saa nne: Saa kwa ajili ya kumnong'oneza Mwenyezi Mungu. Saa kwa ajili ya mambo ya maisha. Saa ya kushirikiana na jamaa na waaminifu ambao wanawaonyesha aibu zenu na wanawasafia nia. Na saa ya kujiepusha na ladha zenu katika mambo yasiyokuwa ya haramu**."[4]

## SABABU ZA MVUTO

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Kwa mambo matatu mwili hustawi na kuvutia: Manukato, mavazi mepesi na kuramba asali**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Manukato hufurahisha, asali hufurahisha, kutazama uoto kunafurahisha na kupanda kipando hufurahisha**."[6]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Manukato hufurahisha, asali hufurahisha, kutazama uoto kunafurahisha na kupanda kipando hufurahisha**."[7]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Furaha hupatikana katika mambo kumi: Kutembea, kupanda, kupiga mbizi majini, kutazama uoto, kula na kunywa, kumtazama mwanamke mrembo, kujamiiana, kupiga mswaki, kuosha kichwa kwa mti wa khatami huko hamamu na kuongea na wanaume**."[8]

## BURUDANI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Burudikeni na chezeni kwani mimi nachukia kuona ususuavu ndani ya dini yenu**."[9]

**Imepokewa kutoka kwa Abu Rafiu amesema: "Nilikuwa namchezesha Hasan bin Ali (a.s) kwa mchezo wa kumchenga akiwa angali mtoto, basi ninapomshika, namwambia nibebe, naye**

---

1. Misbahul-Mtahajid, Uk. 849.
2. Nahjul-Balagha, hekima ya 390.
3. Al-Kafiy, Juz. 54, Uk. 78, hadithi ya 1.
4. Tuhaful-Uquul, Uk. 409.
5. Tibun-Nabiy, Uk. 6.
6. Sahifatu Imam Ridha, Uk. 239, hadithi ya 144.
7. Uyunu Akhbar-Ridha, Juz. 2, Uk. 40, hadithi ya 126.
8. Al-Mahasin, Juz. 1, Uk. 78, hadithi ya 40.
9. Shuabul-Iman, Juz. 5, Uk. 247, hadithi ya 6542.

**ananiambia: 'Ole wako je unau- panda mgongo ambao ameubeba Mtume wa Mwenyezi Mungu?' basi hapo namwacha. Na anaponishika namwambia sikubebi kama ambavyo hukunibeba. Basi ananiambia: 'Hivi huridhii kuubeba mwili ambao kaubeba Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Basi hapo nambeba."**[1]

## MATEMBEZI

Imepokewa kutoka kwa Amru bin Hurayth amesema: "**Niliingia kwa Abu Abdillah (a.s) naye akiwa nyumbani kwa ndugu yake Abdullah bin Muhammad, nikamwambia: 'Mimi ni fidia kwako, kitu gani kilichokuleta kwenye nyumba hii?' Akasema: 'Nimekuja kutembea**."[2]

Imepokewa kutoka kwa Ibrahim bin Abu Mahmud amesema: "Ridhaa [(a.s)] alituambia: 'Ni chachandu ipi inafaa kwa chakula?' Wenzi wetu wakesema: 'Nyama.' Wengine wakasema: 'Siagi.' Na wengine wakadai: 'Maziwa.' Yeye akasema: **'Hapana! Bali ni chumvi. Tulitoka kwenda matembezini basi kijana wetu akasahau chumvi, basi huko wakatuchinjia kondoo mnono mno lakini hatukunufaika naye kwa chochote mpaka tukaondoka**."[3]

## MIZAHA

Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa anafanya mizaha lakini hasemi ila ukweli. Anas bin Malik alisema: "Amekufa Nughayru kwa Abu Umayru, naye ni mwana wa mama Sulaym." Basi Mtume **(s.a.w.w)** akawa anasema: "**Ewe Abu Umayru Tughayru amefanya nini**."[4]

Mmoja kati ya wakeze **(s.a.w.w)** alikuwa na mfanyakazi anayeitwa Anjashatah (yaani mashine ya kusagia), basi Mtume **(s.a.w.w)** akawa anamwambia: "**Ewe Anjashatah fanya urafiki na vigae**."[5]

Kuna mtu alimwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: "**Nibebe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu." Akamjibu: 'Nitakubeba juu ya mtoto wa ngamia.' Akasema: 'Nitamfanyia nini mtoto wa ngamia?' Akamjibu: 'Ngamia hazai ila mtoto wa ngamia**."[6]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimwambia mwanamke aliyekuwa kamtaja mume wake: "**Je ni yule mwenye weupe jichoni?" akasema: 'Hana weupe.' Basi alipokuja kumwambia mumewe, mume akamwambia: 'Hivi huoni kuwa weupe wa jichoni mwangu ni mkubwa kuliko weusi**."[7]

Ajuza mmoja kati ya Maanswari alisema kumwambia Mtukufu Mtume **(s.a.w.w)**: "Niombee Pepo." Mtume **(s.a.w.w)** akamwambia: "**Peponi haingii ajuza**." Basi mwanamke yule akalia, ndipo Mtume akacheka na kumwambia: "**Hivi hujasikia kauli ya Mwenyezi Mungu**: "Hakika tumewaumba (wanawake ) kwa umbo (bora). Na tukawafanya ndio kwanza wanaolewa." (Surat Al-Waqia: 35 - 36)."[8]

---

1. Basharatul-Mustafa, Uk. 140.
2. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 23, hadithi ya 14.
3. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 326, hadithi ya 7.
4. Biharul-An'war, Juz. 16, Uk. 294, hadithi ya 1.
5. Al-Manaqib cha Ibnu Shahru Ashub Juz. 1 Uk. 147.
6. Biharul-An'war, Juz. 16, Uk. 294, hadithi ya 1.
7. Biharul-An'war, Juz. 16, Uk. 294, hadithi ya 1.
8. Biharul-An'war, Juz. 16, Uk. 295, hadithi ya 1.

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimwambia ajuza wa Ashjaiyya: "**Ewe Ashjaiyyah ajuza haingii peponi**." Ndipo Bilal akamuona akilia akaenda kumwambia Mtume **(s.a.w.w)**, Mtume akasema: "**Na mweusi pia**." Basi wote wawili wakakaa wakilia. Ndipo Abbas akawaona na akaenda kumwambia Mtume **(s.a.w.w)**, Mtume akasema: "**Na mzee pia**." Kisha akawaita wote na kuwaambia: Mwenyezi Mungu atawaumba kwa uzuri kama walivyokuwa." **Na akawaambia kuwa wao wataingia Peponi wakiwa vijana wenye kung'aa kwa nuru na kuwa watu wa peponi ni weupe wenye kupakwa wanja**."[1]

Suwaybitu Al-Muhajiriyyu alimwambia Nuuman Al-Badriyyu: "Nilishe." Na alikuwa na chakula huku wakiwa safarini. Basi akamjibu: "Subiri mpaka waje jamaa." Basi wakawakuta jamaa, ndipo Suwaybitu akawaam- bia: "Mtamnunua mtumwa wangu kutoka kwangu?" wakasema: "Ndio." Akawaambia: "Yeye ni mtumwa mwenye maneno mengi, hivyo atawaam- bieni: Mimi ni muungwana, mkimsikiliza mtakuwa mmeniharibia mtumwa wangu dhidi yangu. Mnunueni kwa ngamia kumi." Basi wakaja na kutupia kamba shingoni mwake. Nuuman akasema: "Huyu anawafanyia mzaha, hakika mimi ni muungwana." Wakamwambia: "Tumeshasikia habari yako." Basi wakamchukua na kuondoka naye mpaka watu wengine walipowafuata na kumwokoa. Tangu kipindi hicho Mtume **(s.a.w.w)** akawa anacheka akumbukapo."[2]

Nuuman alimwona bedui akiwa na chupa ya asali akainunua na kuja nayo nyumbani kwa Aisha siku hiyohiyo, akamwambia ichukue, basi Mtume **(s.a.w.w)** akadhani amempa zawadi. Ghafla Nuuman na bedui wakapita mlangoni, basi bedui alipoona muda unazidi kwenda akamwambia Nuuman: "Nirudishie chupa yangu kama hujapata thamani yake." Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akawa amegundua kisa chote. Mtume akamwambia Nuuman: "Kitu gani kilichokupelekea kufanya hivi ulivyofanya?" Akajibu: "Niliona Mtume wa Mwenyezi Mungu anapenda asali na nikaona bedui ana chupa ya asali." Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu akacheka na wala hakudhihirisha kuchukizwa.[3]

## KUOGELEA NA KUTUPA MSHALE

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Burudani bora kwa muumini ni kuogelea**."[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Wafunzeni wanenu kuogelea na kutupa mshale**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Kati ya haki za mtoto kwa baba yake ni amfunze kuandika, kuogelea na kutupa mshale**."[6]

---

1. Biharul-An'war, Juz. 16, Uk. 295, hadithi ya 1.
2. Biharul-An'war, Juz. 16, Uk. 296, hadithi ya 1.
3. Biharul-An'war, Juz. 16, Uk. 296, hadithi ya 1.
4. Kanzul-Ummal, Juz. 15, Uk. 211, hadithi ya 40611.
5. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 47, hadithi ya 4.
6. Kanzul-Ummal, Juz. 16, Uk. 443, hadithi ya 455340.

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Burudani ipendwayo sana kwa Mwenyezi Mungu ni kuwashindanisha ngamia na kutupa mshale**."[1]

Imepokewa kutoka kwa Sulayman At-Tamiymiy amesema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alikuwa anafurahishwa na mtu kuwa mwoge- leaji mwenye kujua kutupa mshale**."[2]

## MIELEKA

Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alitoka siku moja kwenda Abtah, akamwona bedui akichunga kondoo na alikuwa akisifika kwa nguvu, basi bedui yule akamwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: "Je uko tayari tushindane mieleka?" Mtume **(s.a.w.w)** akamwambia: "Utanipa nini?" Akasema: "Mbuzi." Basi wakaanza miele- ka na ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akambwaga chini. Bedui akasema: "Je uko tayari turudie tena?" Akamuuliza: "Utanipa nini?" Akajibu: "Mbuzi." Basi wakaanza mieleka na Mtume akambwaga tena chini. Bedui akasema: "Nifunze Uislamu, kwani hakuna yeyote aliyewahi kunibwaga zaidi yako." Basi akamsilimisha na akamrudishia mbuzi wake.[3]

Hakika Rukana bin Abdi bin Zayd bin Hashim alikuwa na nguvu sana miongoni mwa makurayshi, ndipo siku moja wakiwa kwenye bonde lisilokuwa na kitu Mtume akamwambia: "Ewe Rukanata hivi humwogopi Mwenyezi Mungu na kukubali ninayokulingania?" Akasema: "Lau mimi ningejua kuwa ni haki basi ningekufuata."

Mtume **(s.a.w.w)** akamwambia: "**Hivi unaona ikiwa nikikubwaga utajua fika kuwa nisemayo ni haki?" Akasema: "Ndio." Basi akamwambia simama tushindane kwa mieleka. Basi Rukana akasimama na kushindana naye na hatimaye Mtume wa Mwenyezi Mungu akamshinda na kumbwaga chini. Basi wakarudia tena na Mtume akambwaga tena**.[4]

Kiongozi wa waumini alishindana mieleka na mtu mmoja na hatimaye akambwaga chini. Basi mtu yule akamwambia Ali: "Ewe kiongozi wa waumini Mwenyezi Mungu akuimarishe." Ali akamwambia: **"(Akiimarishe) Kifua chako**."[5]

## MASHINDANO

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Malaika hawashududii chochote kati ya burudani zenu ila mashindano ya ngamia na utupaji wa mishale**."[6]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mashindano ya ngamia hufurahisha**."[7]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Isma'il na Is'haq walipofikia ujana walishin- dana na hatimaye Ismail akashinda, basi Ibrahim akamchukua na**

---

1. Kanzul-Ummal Juz. 4 Uk. 344, hadithi ya 10182.
2. Ad-Durrul-Manthur, Juz. 4, Uk. 87.
3. Mustadrakul-Wasail, Juz. 14, Uk. 82, hadithi ya 16153.
4. Biharul-An'war, Juz. 16, Uk. 178, hadithi ya 19.
5. Kanzul-Ummal, Juz. 13, Uk. 130, hadithi ya 36414.
6. Al-Muujam Al-Kabir, Juz. 12, Uk. 305, hadithi ya 13474.
7. Kanzul-Ummal, Juz. 4, Uk. 344, hadithi ya 10815.

**kumuweka mapajani mwake na akamkalisha Is'haqa pembeni mwake**."[1]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu aliruhusu kushindanisha ngamia na yeye alishindanisha, na katika hilo akaweka zawadi ya wakia za madini ya fedha**."[2]

Imam Muhammadi Al-Baqir amesema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu alimshindanisha ngamia ambaye alipunguzwa uzito toka Al-Hayfau hadi msikiti wa Bani Zurayqi, na alimshindanisha kwa makole matatu ya tende, basi akampa mshindi kole, na akampa mwenye kusali kole na wa tatu kole**."[3]

Ibnu Umar amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alishindanisha kati ya ngamia, basi yule aliyekuwa amepunguzwa uzito alimshindanisha toka huko Al-Hayfau mpaka Thaniyatul-Wadai, na yule aliyekuwa hajapunguzwa uzito akamshindanisha toka Thaniyatul-Wadai mpaka msikiti wa Bani Zurayqi. Abdullah anasema: **'Siku hiyo nilikwa nikimkimbiza farasi basi nikawashinda watu na ndipo farasi wa msikiti wa Bani Zurayqi akawa sawa na mimi**."[4]

Imepokewa kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alipita na kuwakuta vijana wa kianswari wakishindana kutupa mishale, basi Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akasema: "Mimi niko kwenye kundi ambalo yumo mtoto wa Adrai." Basi kundi la pili likaacha kutupa na likasema: "Halitoshindwa kundi ambalo yumo Mtume wa Mwenyezi Mungu." Mtume akasema: "Tupeni bila shaka mimi nitatupa pamoja nanyi." Basi akatupa kwa kushiriki kwenye kila kundi dhidi ya jingine, basi hatimaye hakuna aliyeshinda. Wakaendelea kushindana wao, watoto wao hadi wajukuu zao lakini hakuna walioshinda."[5]

Abu Lubayd amesema: "Ibnu Malik aliulizwa: 'Je mlikuwa mnashindana kwa kuweka zawadi zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: **'Ndio Mtume wa Mwenyezi Mungu alismshindanisha farasi wake kwa kuweka zawadi, basi akashinda na akafurahishwa kwa hilo**."[6]

## 6 - THAMANI YA TABIA NJEMA NA MATENDO MEMA

### KUACHA MAASI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakaetoka kwenye udhalili wa kumuasi Mwenyezi Mungu hadi kwenye heshima ya kumtii Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu atamliwaza bila kuwepo mlewezeshaji na atampa auni bila mali**."[7]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mtu hawi ni mwenye uwezo wa kutenda haramu kisha akaacha kwa ajili ya kumwogopa Mwenyezi Mungu ila ni lazima Mwenyezi Mungu atampa**

1. Biharul-An'war Juz. 12, Uk. 111, hadithi ya 37..
2. Daaimul-Islam, Juz. 1, Uk. 345.
3. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 48, hadithi ya 5.
4. Musnad Ibnu Hanbal, Juz. Uk. 206, hadithi ya 4487.
5. Awali Lial, Juz. 3, Uk. 266, hadithi ya 5.
6. Awali Lial, Juz. 3, Uk. 265, hadithi ya 2.
7. Biharul-An'war, Juz. 75, Uk. 359, hadithi ya 74.

**badala hapa duniani kabla ya Akhera kwa kumpa kilicho bora kuliko hicho**."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "Itakapofika Siku ya Kiyama baadhi ya watu toka katika umma wangu Mwenyezi Mungu atawaoteshea mbawa, na hapo wataruka toka makaburini mwao mpaka Peponi, watatembea humo na kustarehe watakavyo. Basi Malaika watawaambia: Je mmeona heasabu? Watasema: Hatujaona hesabu. Watawaambia: Je mmevuka Sirat? Watasema: Hatujaiona Sirat. Watawaambia: Je mmeona Jahannam? Watasema: Hatujaona chochote. Malaika watawauliza: Ninyi ni kutoka umma wa nani? Watasema: Ni kutoka umma wa Muhammad. Watawaambia: Tunawaapisha kwa Mwenyezi Mungu, hebu tusimulieni ni amali gani mlikuwa mkiifanya duniani? Watasema: Tulikuwa na sifa mbili basi Mwenyezi Mungu kwa rehema Zake akatufikisha katika hadhi hii. Watawaambia: Ni zipi hizo? Watasema: Tulikuwa tuwapo faragha huona haya kumwasi Mwenyezi Mungu, na tunaridhia kwa kidogo tulichopewa. Basi Malaika watawaambia: Hadhi hii ni haki yenu."[2]

## TOBA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Toba ni nzuri lakini kwa vijana ni nzuri zaidi**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakuna kitu kipendwacho zaidi na Mwenyezi Mungu kama kijana mwenye kutubu. Na hakuna kitu kimchukizacho mno Mwenyezi Mungu kama mzee mwenye kuendelea ndani ya maasi**."[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu humpenda sana kijana mwenye kutubu**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu hufurahishwa sana na toba ya mja wake kuliko mgumba aliyezaa na mpotevu aliyepata na mwenye kiu aliyekata kiu**."[6]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Ukifanya kosa fanya haraka kulifuta kwa kutubia**."[7]

Abu Basir amesema: "Nilikuwa nina jirani alikuwa ni mpambe wa mtawala basi akawa amepata mali, akaandaa mabinti wanenguaji na alikuwa anawakusanya kwake anakunywa pombe na kuniudhi, basi nikam- lalamikia hilo zaidi ya mara moja lakini hakujali. Basi nilipomsisitizia hilo akaniambia: 'Ewe ndugu mimi ni mtu mwenye maradhi na wewe ni mtu mwenye afya njema, natamani lau kama ungepeleka tatizo langu kwa rafiki yako, nataraji Mwenyezi Mungu ataniokoa kupitia kwako.' Basi hilo likakaa moyoni mwangu na nilipokwenda kwa Abu Abdillah nilimuelezea hali yake, naye akaniambia: 'Utakaporejea huko Kufa atakujia basi mwambie: "Jafar bin Muhammad anasema: 'Acha uliyonayo nakudhamini

---

1. Kanzul-Ummal, Juz. 15, Uk. 787, hadithi ya 43113.
2. Biharul-An'war, Juz. 103, Uk. 25, hadithi ya 31.
3. Kanzul-Ummal, Juz. 15, Uk. 896, hadithi ya 43542.
4. Kanzul-Ummal, Juz. 4, Uk. 217, hadithi ya 10233.
5. Kanzul-Ummal, Juz. 4, Uk. 209, hadithi ya 10185.
6. Kanzul-Ummal, Juz. 4, Uk. 205, hadithi ya 10165.
7. Tuhaful-Uquul, Uk. 18.

Pepo toka kwa Mwenyezi Mungu.' Basi niliporejea Kufa alinijia akiwa miongoni mwa walionijia, nikamzuia mpaka nyumba yangu ilipobaki faragha, ndipo nikamwambia: 'Ewe ndugu yangu mimi nimekutaja mbele ya Abu Abdullah Jafar bin Muhammad As- Sadiq (a.s) akaniambia: "Utakaporejea Kufa atakujia basi mwambie: 'Jafar bin Muhammad anakwambia: 'Acha uliyonayo ninakudhamini pepo toka kwa Mwenyezi Mungu.' Amesema: Basi akalia kisha akaniambia: 'Wallahi ni kweli Abu Abdullah kakwambia haya?' Nikamwapia kuwa hakika ameniambia niliyokuwambia. Akasema: 'Inatosha na imekwisha." Baada ya siku alinitumia mtu akiniita ghafla nikamkuta nyuma ya nyumba yake akiwa uchi, akaniambia: 'Ewe Abu Basir, wallahi sijabakiwa na chochote nyumbani mwangu ila nimekitoa na nimebaki kama unionavyo. Akasema: 'Ndipo nikaenda kwa baadhi ya ndugu zetu nikakusanya kiasi kilichoweza kumvisha, kisha hazikupita siku nyingi akawa amenitumia mtu kuwa mimi ni mgonjwa njoo kunitazama. Nikawa nakwenda kwake mara kwa mara kumtibu, na hata alipofikwa na mauti nilikuwa nimekaa kwake akiwa anahangaika na nafsi yake na ndipo akazimia na kisha akazinduka na kuniambia: 'Ewe Abu Basira rafiki yako amenitekelezea ahadi aliyoahidi.' Nilipohiji nilikwenda kwa Abu Abdullah (a.s) nikamwomba ruhusa na nilipoingia yeye alianza kuniambia toka ndani ya nyum- ba huku mguu wangu mmoja ukiwa kizingitini na mwingine ukiwa nje: 'Ewe Abu Basira tumeshamtekelezea rafiki yako."[1]

Abu Nasri Bishru bin Al-Harith bin Abdu-Rahman mwenye asili ya Al-Marawaziyu aliyekuwa akiishi huko Baghdad, mwanairfani na mtawa ambaye ni mmoja wa nguzo za mfumo wa utawa. Inasemekana kuwa alikuwa mmoja wa watoto wa Marais na maafisa wa serikali, naye alikuwa kati ya watu wa anasa na miziki.

Inasemekana kuwa sababu kubwa ya kutubu kwake ni kwamba Maulana Imam Musa bin Jafar (a.s) alipita nyumbani kwake huko Baghadad akasikia miziki na sauti za nyimbo huku fujo ikitoka ndani ya nyumba hiyo, ghafla akatoka mtumwa wa kike huku mkononi akiwa na uchafu akautupa jalalani na ndipo Imam (a.s) akamwambia: "Ewe binti! Je mwenye nyumba hii ni muungwana au mtwana?" Akajibu: "Hapana ni muungwana." Imam akasema: "Umesema kweli kwani angekuwa ni mtwana basi angemuogopa bwana wake." Basi aliporejea ndani bwana wake akamwambia akiwa yuko kwenye meza ya vileo: "Kitu gani kilichokuchelewesha?" Akajibu: "Mtu mmoja ameni- ambia kadha wa kadha." Ndipo akatoka akiwa peku mpaka akamkuta maulana Al-Kadhim (a.s) akatubu mikononi mwake na kuomba msamaha na akalia mbele yake kwa kuona haya kutokana na amali zake."[2]

Imam Jafar As-Sadiq (a.s) amesema: "Kulikwa na mchamungu mmoja zama za Bani Israil alikuwa hajajichumia chochote kati ya mambo ya dunia, basi Ibilisi akapuliza mluzi na kuwakusanya askari wake kwake, akawaambia: Nani atamrubuni fulani? Mmoja akasema: Mimi nitamrubuni. Akamuuliza: Utamwendea kwa kitu gani? Akasema: Nitatumia wanawake. Akamwambia: Humuwezi, hajawahi kuwagusa wanawake. Mwingine

---

1. Al-Kafiy, Juz. 1, Uk. 474, hadithi ya 5.
2. Al-Kunniy Wal-Alqab, Juz. 2, Uk. 167.

akasema: Mimi hapa nitamrubuni. Akamuuliza: Utamwendea kwa kitu gani? Akasema: Nitatumia vileo na starehe. Akamwambia: Humuwezi, huyu harubuniwi kwa hivi. Mwingine akasema: Mimi hapa nitamrubuni. Akamuuliza: Utamwendea kwa kitu gani? Akasema: Nitatumia mema yake. Akamwambia: Nenda wewe ndiye utakayemuweza.

Basi akaenda mpaka alipokuwepo mtu yule, akasimama usawa wake huku akisali basi mtu yule alikuwa analala lakini shetani halali, anapumzika na shetani hapumziki, ndipo mtu yule alipomgeukia (shetani) huku akiwa anaona amali yake ni ndogo na nafsi yake imeshindwa, akamwambia: "Ewe mja wa Mwenyezi Mungu ni kupitia kitu gani umepata nguvu za kuswali swala hii?" Lakini shetani hakumjibu kitu. Akarudia tena na ndipo akamjibu kwa kusema: "Hakika mimi nilitenda dhambi nami hapa ninatubia, hivyo ninapoikumbuka dhambi hiyo napata nguvu za kuswali." Yule mtu akamwambia: "Niambie hiyo dhambi yako ili niitende na nitubie, kwani nikiifanya nitakuwa napata nguvu za kuswali." Akamwambia: Nenda mjini na muulizie malaya fulani, mpe dirhamu mbili na ujamiiane naye." Akasema: "Nitazipata wapi hizo dirhamu mbili na wala sijui ni nini dirhamu mbili?" Ndipo shetani akazitwaa toka chini ya unyayo wake na kumpa. Basi mtu yule akaingia mjini akiwa na joho lake huku akiuliza nyumba ya malaya fulani, basi watu wakamwelekeza ilipo wakidhani kuwa amekuja ili kumpa mawaidha, basi walipomwelekeza akamwendea na kumtupia ndowano ya dirhamu mbili, akamwambia simama, akasimama na kuingia nyumbani mwake. Mwanamke akamwambia: "Ingia lakini wewe umekuja katika namna ambayo huwa siijiwi kwa namna hiyo, nipe habari zako." Basi akampa habari na ndipo malaya yule akamwambia: "Ewe mja wa Mwenyezi Mungu! Kuacha dhambi ni rahisi kuliko kutafuta toba na wala si kila atafutaye toba huipata. Na ni lazima huyo alikuwa ni shetani aliye- jimithili kwako, ondoka hakika wewe hutoona kitu." Basi akaondoka na usiku uleule mwanamnke yule akafariki, basi walipoamka asubuhi watu wakakuta juu ya mlango wake kumeandikwa: "Hudhurieni msiba wa fulani kwani hakika yeye ni miongoni mwa watu wa peponi." Watu wakaingiwa na shaka wakakaa siku tatu bila kumzika wakiwa na shaka kuhusu jambo lake. Ndipo Mwenyezi Mungu akafunua ufunuo kwa Nabii miongoni mwa Manabii ambaye simjui ila Musa bin Imran akimwambia: "Nenda kwa fulani ukamsalie na waamuru watu wamsalie, kwani hakika Mimi nimeshamsamehe, na nimewajibisha apate pepo kwa kitendo cha kuzuia mja wangu fulani dhidi ya kuniasi."[1]

Inasemekana Mwenyezi Mungu alimfunulia Daudi wahyi kwamba: "**Ewe Daudi lau kama wanaonipa kisogo wangejua jinsi gani ninavyowangojea, ninavyowahurumia na jinsi nilivyo na shauku ya kuona wao wanaacha maasi yao, basi wangekufa kwa ajili ya shauku ya kutaka kuja kwangu, na viungo vyao vingekatikakatika kutokana na mapenzi yao Kwangu**."[2]

1. Al-Kafiy, Juz. 8, Uk. 384, hadithi ya 584.
2. Al-Muhujjat Al-Baydhai, Juz. 8, Uk. 62.

## NIDHAMU

Imam Ali (a.s) amesema alipokuwa akiwausia Hasan na Husein (a.s) baada ya kupigwa dhoruba ya upanga na Ibnu Muljim mlaanifu: "**Ninawausieni ninyi, wanangu wote, ahali zangu na yeyote atakayefikiwa na ujumbe wangu, nawausieni kumcha Mwenyezi Mungu na kunadhimu mambo yenu**."[1]

## KUHESHIMU HAKI ZA WAZAZI WAWILI

Mwenyezi Mungu amesema: "Na Mola wako Mlezi ameamuru kuwa msimwabudu (yeyote) ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema." (Surat Bani Israail: 23).

Akasema tena: "Basi akatabasamu akiichekea kauli yake na akasema: Ewe Mola wangu! Nipe nguvu nishukuru neema yako uliyonineemesha mimi na wazazi wangu na nipate kufanya vitendo vizuri uvipendavyo, na uniingize kwa rehema zako katika waja wako wema." (Surat Namlu: 19).

Akasema tena: "Na tumemuusia mwanadamu afanye wema kwa wazazi wake, mama yake amechukua mimba yake kwa taabu na amemzaa kwa taabu, na kumbeba na kumwachisha ziwa (kunyonya) ni miezi thelathini, hata anapofikia baleghe yake na akawa mwenye umri wa miaka arobaini, akasema: Ee Mola wangu Mlezi! Niwezeshe nishukuru neema zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na ili nifanye vitendo vizuri unavyovipenda, na unitengenezee watoto wangu, kwa hakika ninatubu kwako na hakika mimi ni miongoni mwa walionyenyekea." (Surat Ahqaf: 15).

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Dua ya mzazi kwa mwanae ni kama kuchukua kwa mkono**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "Watu watatu walitoka wakizunguka ardhini basi walipokuwa wakimwabudu Mwenyezi Mungu pangoni chini ya jabali ndipo jiwe kubwa lilipotoka juu ya mlima na kuziba mlango wa pango. Wakaanza kuambizana: Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, wallahi hatowaokoeni mpaka mumsadikishe Mwenyezi Mungu vilivyo, leteni yale mliyotenda kwa moyo mmoja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kwani mmepata mtihani huu kutokana na dhambi. Mmoja wao akasema: 'Ewe Mwenyezi Mungu ikiwa unajua kuwa mimi nilimtafuta mwanamke kwa ajili ya uzuri wake na urembo wake, nikampa mali nyingi, nilipompata na kumkalia mkao wa mwanaume kwa mwanamke nilikumbuka moto, ikiwa ni kwa kukuogapa wewe basi ewe Mwenyezi Mungu tuondolee jiwe hili.' Basi likajipasua hadi mwanya ukaonekana. Mwingine akasema: 'Ewe Mwenyezi Mungu ikiwa unajua kuwa mimi niliwaajiri watu wanilimie, kila mtu kati yao kwa nusu dirhamu, na walipomaliza niliwapa malipo yao. Mmoja wao akasema: 'Nimefanya kazi za watu wawili, wallahi sichukui ila dirham maja.' Akawa ameacha mali yake kwangu, nami nikaitumia hiyo nusu dirhamu kwenye ardhi, basi Mwenyezi Mungu akatoa riziki kutokana na nusu hiyo. Alipokuja mwenyewe na kuitaka nusu dirhamu yake nilimpa dirhamu kumi na nane elfu. Ikiwa unajua kuwa nilifanya hivyo kwa ajili ya kukuogopa basi tuondolee jiwe

---

1. Nahjul-Balagha, barua ya 47.
2. Al-Firdawsu, Juz. 2, Uk. 213, hadithi ya 3038.

hili.' Basi likaacha uwazi mpaka wakawa wanaweza kuonana. Akasema wa tatu wao: 'Ewe Mwenyezi Mungu ikiwa unajua kuwa baba yangu na mama yangu walikuwa wamelala nikawaletea bakuli la maziwa na nikahofia kuwa nikiyaweka chini wadudu watayaramba, na nikahofia kuwa nikiwaamsha nitakuwa nimewaudhi, basi nikaendelea kuwa katika hali hiyo mpaka wakaamka na wakayanywa. Ewe Mwenyezi Mungu ikiwa unajua kuwa mimi nilifanya hivyo ili kutafuta radhi Zako basi tuondolee jiwe hili.' Ndipo jiwe likapasuka kabisa mpaka njia ikawa nyepesi kwao."Kisha Mtume **(s.a.w.w)** akasema: '**Atakayemsadikisha Mwenyezi Mungu atafaulu**."[1]

Insafu katika muamala na watu: Imam Ali (a.s) amesema: "**Ni lipi neno lililokusanya yote? Ni uwapen- delee watu lile unalopenda kwa ajili ya nafsi yako, na uchukie kuwatendea lile unalochukia kwa ajili ya nafsi yako**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Inatosha kuwa ni ujinga kwa mtu kukataza watu wasitendewe yale yale anayowatendea yeye**."[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mtu mbaya zaidi kati ya watu ni yule anayefu- atilia aibu za watu huku akifumbia macho aibu zake**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema katika barua yake kwa Imam Hasan: "**Ewe mwanangu mpendwa! Ifanye nafsi yako kuwa ndio mizani ya yale yaliyopo kati yako na mwenzio, hivyo mpendelee mwenzako yale unayoyapenda kwa ajili ya nafsi yako, na chukia kumtendea yale unayochukia kwa ajili yako**."[5]

## KAZI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Kutafuta halali ni faradhi kwa kila mwislamu wa kiume na wa kike**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Afanyaye kazi huongeza nguvu, na anayepu- uzia kazi huzidi kulegea**."[7]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Jemedari wa waumini alikuwa akitoka huku akiwa na mizigo ya kokwa za tende kabeba. Anapoambiwa: 'Ewe Abul Hasan ni nini hiki ulichobeba?' Husema: 'Ni mitende atakapotaka Mwenyezi Mungu.' Basi anazipanda na hakuna hata moja inayomtoka**."[8]

Abu Amru As-Shaybaniy amesema: "**Nilimwona Abu Abdullah (a.s) na mikononi akiwa na koleo na kajifunika joho zito akifanya kazi bustanini kwake huku jasho likimtoka mgongoni. Nikamwambia: Mimi ni fidia kwako nipe nikufanyie. Akaniambia: 'Mimi napenda mtu apate adha ya ukali wa joto la jua akiwa anatafuta maisha**."[9]

Abdul-Aala mtumwa wa Ali Saam amesema: "Nilimkuta Abu Abdillah kwenye baadhi ya njia za Madina, siku yenye joto kali la kiangazi,

1. Al-Mahasin, Juz. 1, Uk. 394, hadithi ya 881.
2. Tuhaful-Uqul, Uk. 81.
3. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 7073.
4. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5739.
5. Nahjul-Balagha, barua ya 31.
6. Biharul-An'war, Juz. 103, Uk. 9, hadithi ya 35.
7. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 7990 na 7991.
8. Al-Kafiy, Juz.5, Uk. 75, hadithi ya 9.
9. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 76, hadithi ya 13.

nikamwambia: 'Mimi ni fidia kwako! Hali yako kwa Mwenyezi Mungu na ukuruba wako kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu bado unafanya juhudi mwenyewe katika siku kama hii?'Akasema: **'Ewe Abdul-Aala nimetoka ili kutafuta riziki ili nisiwahitajie watu mfano wako**."[1]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Ambaye haoni haya katika kutafuta maisha yake basi matumizi yake yatapungua na akili yake kupumzika na familia yake kuneemeka**."[2]

Ali bin Abu Hamza amesema: "Nilimwona Abul Hasan (a.s) akifanya kazi kwenye ardhi yake huku nyayo zake zikiwa zimelowa jasho, nikamwambia: 'Mimi ni fidia kwako, wako wapi watumishi?' Akasema: 'Ewe Ali, amefanya kazi kwa mkono wake katika ardhi yake yule aliyekuwa bora kuliko mimi na baba yangu.' Nikamwambia ni nani huyo? Akasema: 'Rasuli wa Mwenyezi Mungu, jemedari wa waumini na mababa zangu, wote walikuwa wakifanya kazi kwa mikono yao, nacho ni miongo- ni mwa vitendo vya Manabii na Mitume, Mawasii na watu wema."[3]

Ufanisi wa kazi: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu Mtukufu anapenda mmoja wenu anapofanya kazi yoyote aifanye kwa ufanisi**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Unapenda uwe miongoni mwa kundi la Mwenyezi Mungu lililoshinda? Mche Mwenyezi Mungu na fanya vizuri kwenye kila jambo lako, kwani hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wenye kumcha na wale ambao hufanya vizuri**."[5]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu alishuka kaburini mpaka akamweka Saad bin Mu'adh ndani ya mwanandani na akaweka sawa tofali juu yake, akawa anasema: 'Nipe jiwe, nipe udongo mbichi huku akiimarisha tofali. Alipomaliza na akaweka udongo juu na kusawazisha kaburi, akasema: 'Hakika mimi ninajua fika kuwa litakwishana litapatwa na mtihani, lakini Mwenyezi Mungu anapenda mja anapo- fanya amali yoyote basi aifanye kwa uimara**."[6]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Atakayejiajiri mwenyewe basi amejiletea riziki yake mwenyewe. Vipi isiwe hivyo ilihali alilolipata humo ni la Mola wake Mlezi ambaye alimwajiri?!**"[7]

## KUWAHUDUMIA WATU

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayeamka huku akiwa hajali mambo ya waislamu basi si mwislamu**."[8]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: "Na akanifanya ni mwenye kubarikiwa popote nitakapokuwa." (Surat Maryam: 31). "**Ni wenye kunufaisha**."[9]

---

1. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk.74, hadithi ya 3.
2. Thawabul-Aaamal, Uk. 200.
3. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 75, hadithi ya 10.
4. Kanzul-Ummal, Juz. 3 Uk. 907, hadithi ya 9128.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 2828.
6. Wasailus-Shia, Juz. 3, Uk. 230, hadithi ya 3484.
7. 238 Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 90, hadithi ya 1.
8. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 163, hadithi ya 1.
9. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 165, hadithi ya 11.

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu aliulizwa: 'Ni nani mtu apendwaye sana na Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Yule mtu awanufaishaye sana watu**."[1]

Jamil amesema: "Nilimsikia Imam As-Sadiq (a.s) akisema: **'Waumini ni wahudumu wa wenzi wao.' Nikamwambia vipi wanakuwa wahudumu wa wenzi wao? Akasema: 'Wanafaidishana wao kwa wao**."[2]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "Isa (a.s) alipita akawakuta watu wamevaa majalibibi akawaulizia, akaambiwa: Ni binti wa fulani anapelekwa nyumba ya fulani. Akasema: 'Rafiki yao wa kike atakufa usiku.' Basi

walipoamka asubuhi watu wakasema bado yuko hai. Ndipo (a.s) akaenda akifuatana na watu mpaka nyumbani kwa yule mwanamke, alipotoka mumewe akamwambia: 'Muulize mkeo ni kitu gani alichotenda jana usiku?' Mke akasema: 'Sikutenda kitu ila kuna ombaomba alikuwa akini- jia kila usiku wa siku ya Ijumaa kati ya Ijumaa zilizopita naye alikuja usiku uliyopita akaita na hakuna aliyemjibu, ndipo akasema: 'Imekuwa vigumu kwangu kwani yeye hasikii sauti yangu ilihali familia yangu wanabaki usiku huu wakiwa na njaa.' Ndipo nikaamka nikiwa nimekasirishwa nikampa kiasi ambacho nilikuwa nampa hapo awali.' Isa (a.s) akasema: 'Inuka hapo ulipoketi.' Alipoinuka ghafla akatokea nyoka mkubwa toka kwenye nguo zake (mwanamke) akiwa ameng'ata mkia wake. Isa (a.s) akasema: **'Kutokana na sadaka uliyotoa umeepushiwa nyoka huyo**."[3]

## UAMINIFU

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Uaminifu ni utajiri**."[4]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "Tazama hadhi aliyofikia Ali (a.s) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, nawe shikamana nayo, kwani hakika Ali (a.s) alifikia hadhi aliyofikia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwa ukweli na uaminifu."[5]

Abdur-Rahman bin Sayabah amesema: "Alipohiliki baba yangu alikuja kwangu mtu mmoja kati ya ndugu zake, akagonga nami nikatoka, akanipa pole na kuniambia: 'Je baba yako ameacha chochote?' nikamwambia hapana. Basi akanipa fuko likiwa na dirhamu elfu moja, na akaniambia: 'Lihifadhi vizuri na kula fadhila zake.' Ndipo nikaingia kwa mama yangu nami nikiwa na furaha nikampa habari. Basi usiku uilipoingia nilimwendea

rafiki wa baba yangu akaninunulia bidhaa na nikaanza kukaa dukani na Mwenyezi Mungu akaniruzuku kheri nyingi. Ulipofika msimu wa Hijja nikatamani kuhiji, nikamwendea mama yangu nikampa habari, nikamwambia: Mimi ninatamani niende Makka. Akaniambia: 'Mrudishie fulani dirhamu zake.' Nikamwendea na kumpa kana kwamba mimi nimempa zawadi. Yule mtu akaniambia: 'Huenda umeziona chache, nikuongeze nyingine?' Nikamwambia: La, lakini nimetamani kuhiji hivyo nimependa kitu chako nikikabidhi kabisa.' Kisha nikatoka na nikatekeleza

1. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 164, hadithi ya 2.
2. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 167, hadithi ya 9.
3. Biharul-An'war, Juz. 14, Uk. 324, hadithi ya 37.
4. Musnadus-Shihab, Juz. 14, Uk. 324, hadithi ya 37.
5. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 104, hadithi ya 5.

ibada yangu ya Hijja, kisha nikarejea Madina nikiwa na watu hadi nikaingia kwa Abu Abdillah (a.s), naye alikuwa anawapa idhini ya ujumla, basi nikakaa mwishoni mwa watu nami nilikuwa ni kijana mdogo, na hapo walikuwa wakimuuliza maswali naye anawajibu. Watu walipopungua kwake aliniashiria nisogee nikasogea, akaniambia: Una haja yoyote? Nikamwambia: Mimi ni fidia kwako mimi ni Abdur-Rahman mwana wa Sayabah. Akaniambia: Baba yako amefanya nini? Nikamwambia: Amehiliki. Basi akaumia na kumwombea rehema, kisha akaniambia: Je ameacha kitu? Nikamwambia: Hapana. - Akaniambia: Umehiji kutokana na nini? Nikaanza kumsimulia kisa cha mtu yule. Basi hakuniacha nimalize akawa ameniambia: Umefanya nini katika elfu hizo? Nikamwambia: Nimemrudishia mwenyewe. Akaniambia: Umefanya vizuri, je nikuusie? Nikaasema: Mimi ni fidia kwako, ndio. Akaniambia: Shikamana na ukweli na kuwa mwaminifu utashirikiana na watu katika mali zao hivi. Akawa amekusanya vidole vyake. Amesema: Nikahifadhi hilo, basi nikatoa Zaka dirhamu laki tatu."[1]

Imam Muhammad Al-Baqir (a.s) amesema: "**Vitu vitatu Mwenyezi Mungu hakumwekea yeyote ruhusa ya (kuvikiuka): Kuwa mwaminifu kwa mwema na muovu, kutekeleza ahadi kwa mwema na muovu na kuwatendea wema wazazi wawili, sawa wawe wema au waovu**."[2]

## KUJIPAMBA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika Mwenyezi Mungu ni Mzuri anapenda uzuri**".[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: "**Nywele nzuri ni zawa- di ya Mwenyezi Mungu Mtukufu basi iheshimuni**."[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayefuga nywele azitunze au azikate**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema kuwaambia wanaume: "**Kateni kucha zenu**." Akawaambia wanawake: "**Ziacheni kwani zenyewe ni mapambo yenu**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ni lazima mmoja wenu ajipambe kwa ajili ya ndugu yake mwislamu kama ajipambavyo kwa ajili ya mgeni ambaye anapenda amwone akiwa katika hali nzuri**."[7]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Vaa na jipambe, hakika Mwenyezi Mungu ni Jamilu anapenda jamali, lakini utokane na halali**."[8]

Imam Muhammad Al-Baqir (a.s) amesema: "**Haifai kwa mwanamke kuji- acha hali ya kutojipamba bali angalau aweke mkufu shingoni mwake**."[9]

1. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 134, hadithi ya 15.
2. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 162, hadithi ya 2.
3. Sahih Muslim, Juz. 1, Uk. 93, hadithi ya 147.
4. Man La Yahdhuruhul-Faqih, Juz. 1, Uk. 129, hadithi ya 327.
5. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 485, hadithi ya 2.
6. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 491, hadithi ya 15.
7. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 439, hadithi ya 10.
8. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 442, hadithi ya 7.
9. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 509, hadithi ya 2.

Al-Hakam bin Utaybah amesema: "Niliingia kwa Abu Jafar (a.s) naye akiwa ndani ya nyumba iliyopambwa kwa samani za ndani, naye akiwa na kanzu nyepesi na joho lenye rangi huku rangi ikiwa imeathiri shingo lake, nikawa natazama nyumba na ninamtazama. Akaniambia: 'Hakam! Unasemaje katika hili?' Nikamwambia: 'Siwezi kusema chochote hali mimi naliona juu yako, ama kwetu sisi hilo hufanywa na kijana barobaro.' Akaniambia: **'Ewe Hakam! Ni nani aliyeharamisha mapambo ya Mwenyezi Mungu aliyoyatoa kwa ajili ya waja wake, na vyakula vizuri miongoni mwa riziki. Na hili ni miongoni mwa aliyoyatoa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya waja wake. Ama nyumba hii ambayo unaiona ni nyum- ba ya mwanamke, nami ni karibu nitafanyanaye harusi. Na nyumba yangu ni ile unayoitambua**."[1]

## MAADILI MEMA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika nimetumwa ili nitimize maadili mema**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika nimetumwa ili nitimize tabia njema**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu amefanya tabia njema kuwa kiungo kati Yake na viumbe Wake. Basi mmoja wenu atosheke na kushikamana na tabia zilizoungana na Mwenyezi Mungu**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Fahamuni hakuna thawabu inayotarajiwa wala adhabu inayozuilika. Je mnazipa mgongo tabia njema?!**"[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Tabia njema ni dalili ya jadi njema**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Katika tabia njema kuna hazina za riziki**."[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mtu aridhiwaye sana ni yule ambaye tabia zake ni maridhawa**."[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwenye ukamilifu wa imani miongoni mwenu ni yule mwenye tabia njema**."[9]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Tabia njema ni dini nayo huongeza riziki**."[10]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Wasia wa Waraqah bin Nawfal kwa Khadija binti Khuwaylid (r.a) alipokuwa akiingia kwake ni: 'Fahamu kuwa ujana mzuri wenye tabia njema ni ufunguo wa kheri na kufuli la shari. Na ujana wenye tabia mbaya ni kufuli la kheri na ufunguo wa shari**."[11]

---

1. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 446, hadithi ya 1.
2. Asunanul-Kubra, Juz. 10, Uk. 323, hadithi ya 20782.
3. Musnad Ibnu Hanbal, Juz. 3, Uk. 323, hadithi ya 8961.
4. Tanbihul-Khawatir, Juz. 2, Uk. 122.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 6278.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4855.
7. Al-Kafiy, Juz. 8, Uk. 23.
8. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 3072.
9. Uyunul-Akhbar Ridhaa, Juz. 2, Uk. 38, hadithi ya 104.
10. Tuhufal-Uquul, Uk. 373.
11. Al-Amaal cha Tusiy Uk. 302, hadithi ya 598.

Husain bin Atiyyah amepokea kutoka kwa Imam As-Sadiq (a.s) kuwa amesema: "Tabia njema ni kumi, ukiweza kujitahidi ziwepo kwako basi na ziwepo, kwani zenyewe huwa kwa mzazi na wala haziwi kwa mtoto, na huwa kwa mtoto wala haziwi kwa baba yake na huwa kwa mtwana na wala haziwi kwa muungwana." Akaulizwa ni zipi hizo? Akasema: **'Ukweli wa ushujaa, ukweli wa maneno, uaminifu, kuunga udugu wa tumbo moja, kumkirimu mgeni, kumlisha ombaomba, kulipa wema kwa wema, kushutumiwa kwa ajili ya jirani yako, kushutumiwa kwa ajili ya rafiki yako, na kiongozi wao ni kuwa na haya**."[1]

Imepokewa kutoka kwa Hasan bin Muhammad kutoka kwa babu yake kutoka kwa sahaba zake zaidi ya mmoja, wamesema: "Mtu mmoja toka kizazi cha Umar bin Al-Khattab alikuwa akimuudhi Abu Hasan Musa (a.s) huko Madina, anamtukana amuonapo na kumshutumu Ali (a.s). Ndipo wafuasi wake wakamwambia siku moja: Tuache tumuuwe muovu huyu. Lakini akawakataza kufanya hivyo kwa kuwakemea sana. Akaulizia kuhusu mjukuu huyo wa Umar akaambiwa kuwa huwa analima huko kwenye viunga vya pembezoni mwa Madina, basi akarakibu hadi kwake akamkuta shambani kwake, ndipo akaingia shambani kwa punda wake, hapo mjukuu wa Umar akapiga kelele: 'Usikanyage mazao yetu.' Lakini akayakanyaga kwa punda wake mpaka akafika kwake, akashuka na akaketi kwake kwa furaha na cheko, na akamwambia:-Umegharamia kiasi gani kwenye shamaba lako hili? -Akasema: Dinari mia moja. - Akamwambia: Unataraji kupata kiasi gani?

Akajibu: Mimi sijui ghaibu. -Akamwambia: Nimekwambia Unataraji utajiwa na kiasi gani? -Akasema: Nataraji kujiwa na dinari mia mbili. Mpokezi anasema: Basi Abu Hasan (a.s) akamtolea fuko likiwa na dinari mia tatu na kumwambia: 'Shamba lako litabaki katika hali yake na Mwenyezi Mungu atakuruzuku unayotaraji.' Basi mjukuu wa Umar akasi- mama na kubusu kichwa chake na kumwomba amsamehe makosa yake. Imam akatabasamu na kuondoka. Alipoelekea msikitini akamkuta mjukuu wa Umar kakaa, alipomuona Imam akasema: 'Mwenyezi Mungu ajua jinsi anavyoweka risala yake.' Ndipo sahaba zake waliposhituka na kumuuliza: 'Ni ipi kadhia yako? Ulikuwa ukisema yasiyokuwa haya.' Akawaambia: Mmeshasikia niliyosema hivi sasa. Na akaanza kumwombea kheri Abul Hasan (a.s). Ndipo Abu Hasan aliporejea nyumbani kwake akawaambia wanabaraza wake waliomuomba wamuue mjukuu wa Umar: 'Ni lipi lililo bora, mlilotaka au nililotaka? Mimi nimemsawazisha kwa kiwango hiki mlichokijua, na shari yake imezuilika."[2]

## UTAWA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Enyi kundi la vijana wa kikuraishi! Hifadhini tupu zenu. Fahamuni kuwa atakaehifadhi utupu wake basi atapata pepo**."[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwenyezi Mungu anapomtakia mja kheri huli- hifadhi tumbo lake na utupu wake**."[1]

---

1. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 55, hadithi ya 1.
2. Biharul-An'war, Juz. 48 Uk. 102.
3. Al-Muujam Al-Awsat, Juz. 7, Uk. 61, hadithi ya 6850.

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwenye kupigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu si mwenye malipo makubwa kuliko aliye na uwezo wa kuzini lakini akafanya utawa. Mtawa amekaribia kuwa malaika miongoni mwa malaika**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Utawa hudhoofisha matamanio**."[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Zaka ya uzuri ni kuwa mtawa**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Utawa huilinda nafsi na huipamba dhidi ya mambo duni**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Utawa ni kiongozi wa kila kheri**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Kazi pamoja na utawa ni bora kuliko utajiri pamoja na ufuska**."[7]

## KUANGUSHA MACHO

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakuna mwislamu yeyote anayemtazama mwanamke mzuri mara ya kwanza, kisha akainamisha macho yake ila ni lazima Mwenyezi Mungu atamuwekea ibada atakayopata raha kwayo**."[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayehifadhi macho yake sifa zake zitakuwa nzuri**."[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Kuhifadhi macho ni miongoni mwa murua**."[10]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mambo matatu ni murua: Kuangusha macho, kupunguza sauti na kutembea kwa wastani**."[11]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayemuona mwanamke ampendezaye basi amwendee mke wake, kwani bila shaka naye anacho mfano wa kile ali- chokiona. Na wala asimpe shetani njia moyoni mwake, na ayaepushe macho yake kwake. Na kama hana mke basi aswali rakaa mbili na amuhimidi sana Mwenyezi Mungu, amswalie Mtukufu Mtume na Aali zake (a.s.), kisha amwombe Mwenyezi Mungu fadhila zake, basi hakika atamhalalishia kwa huruma yake lile litakalomtosheleza**."[12]

Imam Ali (a.s) alipokuwa ameketi na sahaba zake ghafla akapita mwanamke mzuri na watu wakamrushia macho yao, ndipo akasema: "**Amuonapo mmoja wenu mwanamke ampendezaye basi amtomasetomase mkewe, kwani hakika yeye ni mwanamke kama mke wake**."[13]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Mtazamo ni mshale miongoni mwa mishale ya Ibilisi ulio na sumu, atakayeuwacha kwa ajili ya Mwenyezi**

---

1. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4114.
2. Nahjul-Balagha, hekima ya 478.
3. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 2148.
4. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5449.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1989.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1168.
7. Nahjul-Balagha, barua ya 31.
8. Musnad Ibnu Hanbal, Juz. 8, Uk. 299, hadithi ya 22341.
9. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 9050.
10. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 6396.
11. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4660.
12. Al-Khiswal, Uk. 637, hadithi ya 10.
13. Nahjul-Balaghah, hekima ya 420.

**Mungu na si kwa ajili ya kingine basi Mwenyezi Mungu atamfatilizia imani ambayo atapata ladha yake**."[1]

1. Man La Yahdhuruhul-Faqih, Juz. 4, Uk. 18, hadithi ya 4969.

3

# JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA

# UDONDOZI KUTOKA KITABU: JAWAAHIRU AL-HIKMAH LI 'SH-SHABAAB

## 3 - HIJABU

Mwenyezi Mungu asema: "Ewe Nabii, waambie wake zako, na mabinti zako na wake wa wau- mini: Wateremshe juu yao shungi zao. Hivyo inaelekea zaidi waju- likane na wasiudhiwe, na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu." (Surat Ahzab: 59).

Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "Kijana mmoja wa kianswari alimgeukia mwanamke huko Madina na wanawake walikuwa wamevaa skafu zao nyuma ya masikio yao, basi akamtazama ilihali mwanamke yule akiwa mkabala naye, alipovuka mwanamke yule basi kijana akaingia mtaa uliokuwa ukiitwa Bani Fulani, akawa akimtazama kwa nyuma na hatimaye akaugonga uso wake kwenye ukuta na uso wake ukapasuka. Mwanamke alipotoweka akajitazama na kukuta damu zikishururuzika juu ya kifua chake na nguo yake, akasema: Wallahi ni lazima nimwendee Mtume wa Mwenyezi Mungu nikampe habari hii, basi akamwendea. Mtume wa Mwenyezi Mungu alipomuona akamwambia umefanya nini? Ndipo akampa habari ilivyokuwa, na ndipo Jibril akatelemka na Aya hii: "Waambie waumini wanaume wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao, bila shaka Mwenyezi Mungu anazo habari za yale wanayoyafanya." (Surat Nur: 30)."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu amewalaani wanaume wenye kujishabihisha na wanawake. Na Mwenyezi Mungu amewalaani wanawake wenye kujishabihisha na wanaume**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Nilikuwa nimeketi pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu huko Baqii siku yenye mvua na upepo, basi ghafla mwanamke akapita na punda na ghafla mkono wa punda ukaingia ndani ya shimo na hatimaye mwanamke akaanguka, basi Mtume akageuza uso. Wakamwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika yeye amevaa suruwali.' Akasema: 'Ewe Mwenyezi Mungu wasamehe wanawake wenye kuvaa suruwali (Mara tatu). Enyi watu tengenezeni suruwali hakika zenyewe ni miongoni mwa nguo zenu zenye sitara mno, na wahifadhini wake zenu kwazo pindi watokapo**."[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Zama za mwisho, na karibu na Kiyama kutadhihiri wanawake wenye kujiacha wazi uchi, wenye kujitoa katika dini, wenye kuingia katika fitina, wenye kuelemea kwenye matamanio, wenye kuharakishia starehe, wenye kuhalalisha haramu basi hao watadumu motoni**."[4]

1. Al-Kafiy, Juz. 5 Uk. 521, hadithi ya 5.
2. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 552, hadithi ya 4.
3. Mustadrakul-Wasail, Juz. 3, Uk. 244, hadithi ya 3490.
4. Man La Yahdhuruhul-Faqih, Juz. 3, Uk. 390, hadithi ya 4374.

# NDOA

## A: MKAZO WA KUOA UJANANI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakuna kijana anayeoa ujanani ila ni lazima shetani wake alie: 'Ole wangu, ole wangu! Amenizuilia theluthi ya dini yake.' Basi mja amche Mwenyezi Mungu kwenye theluthi mbili zilizobaki**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Enyi kundi la vijana! Ni juu yenu kuoa, na kama hamuwezi basi ni juu yenu kufunga, kwani kwenyewe ni kinga**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ewe kijana oa na jiepushe na zinaa, kwani yenyewe huondoa imani moyoni mwako**."[3]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Kijana wa kianswari alimwendea Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumlalamikia haja yake, basi akamshauri aowe. Kijana akasema: 'Mimi naona haya kurudi tena kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Basi akakutana na mtu kati ya maasnwari, akamwambia: 'Mimi nina binti mzuri, na hatimaye akamuoza. Basi Mwenyezi Mungu akam- panulia riziki, na kijana akamwendea Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumpa habari. Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: 'Enyi kundi la vijana! Ni juu yenu kuoa**."[4]

## B: MUME MARIDHAWA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakapowajieni mnayemridhia dini yake na tabia yake basi muozesheni na kama hamtofanya hivyo basi itakuwa ni uharibifu na ufisadi mkubwa aridhini**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Nilimuoza Mikdad na Zayd ili iwe mbora wenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule mwenye tabia njema kati yenu**."[6]

Alipoulizwa Imam Al-Baqir (a.s) kuhusu ndoa, alisema: "**Atakayeleta posa kwenu na mkaridhia dini yake na uaminifu wake basi muozeni, na kama hamtofanya basi itakuwa ni uharibifu na ufisadi mkubwa aridhini**."[7]

Alikuja mtu mmoja kwa Husein (a.s) akimtaka ushauri juu ya kumuoza binti yake. Akasema: "**Muoze kwa mwanamume mchamungu, kwani hakika yeye kama atampenda basi atamkirimu, na kama atamchukia basi hatomdhulumu.**"[8]

## C: MKE MARIDHAWA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Oeni mabinti vijana kwani hakika wao ndio wenye tabia njema.**"[9]

---

1. Biharul-An'war, Juz. 103, Uk. 221, hadithi ya 34.
2. Al-Kafiy, Juz. 4, Uk. 180, hadithi ya 2.
3. Makarimul-Akhlaq, Juz.1, Uk. 430, hadithi ya 1461.
4. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 330, hadithi ya 3.
5. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 347, hadithi ya 3.
6. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 20, hadihti ya 5248.
7. Al-Kafiy Juz. 5, Uk. 347, hadithi ya 1.
8. Al-Majazati An-Nabawiyyah, Uk. 312, hadithi ya 238.
9. Makarimul-Akhlaq, Juz. 1, Uk. 446, hadithi ya 1534.

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwanamke huolewa kwa sifa nne: Kwa mali yake, dini yake, uzuri wake na kwa nasaba yake na familia yake, basi ni juu yako kwa mwenye dini**."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayemuoa mwanamke kwa ajili ya uzuri wake basi hatopata kwake anachokipenda. Na atakaemuoa kwa ajili ya mali basi Mwenyezi Mungu atamtegemeza kwake. Basi ni juu yenu kwa mwenye dini**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayemuoa mwanamke kwa mali ya halali lakini akataka fahari na kujionyesha basi Mwenyzei Mungu hatomzidishia chochote ila udhalili na fedheha.**"[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Oeni kwenye matum- bo mema, kwani hakika damu hurithisha.**"[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Zichagulieni mbegu zenu sehemu yenye kheri, kwani hakika wanawake huzaa shabihi wa ndugu zao wa kiume na ndugu zao wa kike**."[5]

## D: KUOA AKRABA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Tafuteni wageni na wala msisababishe kuzaa wembamba**."[6]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Msioe akraba (ndugu wa karibu), kwani hakika mtoto huumbwa mwembamba."**[7]

## HAYA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Katika methali za Manabii haijabaki ila kauli ya watu: Ukiwa hauna haya basi fanya utakalo**."[8]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Kuwa na haya ndio kheri yote**."[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Haya ni sababu ya kuelekea kwenye kila jamali.**"[10]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Haya ni tabia njema.**"[11]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Haya ni ufunguo wa kila kheri**."[12]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Haya huzuia kutenda tendo baya**."[13]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Haya ina sehemu kumi: Tisa kwa wanawake na moja kwa wanaume.**"[14]

---

1. Kanzul-Ummal, Juz. 16, Uk. 303, hadihti ya ya 44602.
2. Biharul-An'war, Juz. 103, Uk. 235, hadithi ya 19.
3. Biharul-An'war, Juz. 76, Uk. 362, hadithi ya 30.
4. Makarimul-Akhlaq, Juz. 1, Uk. 432, hadithi ya 1474.
5. Kanzul-Ummal, Juz. 16, Uk. 295, hadihti ya 44557.
6. Al-Majazati An-Nabawiyyah, Uk. 92, hadithi ya 59.
7. Al-Muhujjat Al-Baydhai, Juz. 3, Uk. 94.
8. Uyunul-Akhbari Ridhaa, Juz. 2, Uk. 56, hadithi ya 207.
9. Maanil-Akhbari, Uk. 409, hadithi ya 92.
10. Biharul-An'war, Juz. 77, Uk. 211, hadithi ya 1.
11. Uyunul-Hikam Wal-Mawaidh, Uk. 40, hadithi ya 919.
12. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 340.
13. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1393.
14. Man La Yahdhuruhul-Faqih, Juz. 3 Uk. 468, hadithi ya 4630.

### HAYA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Haya ina namna mbili: Haya ya akili na haya ya ubaradhuli. Haya ya akili ni elimu na haya ya ubaradhuli ni ujinga**."[1]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Mambo matatu hayaonewi haya: Mtu kumhudumia mgeni wake. Kumsimamia baba yake na mwalimu wake toka alipokaa. Na kuitafuta haki hata kama ni ndogo**."[2]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Atakayeona haya kusema haki basi huyo ni baradhuli**."[3]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Haya zina wajihi mbili: Moja ni udhaifu na nyingine ni uimara nayo ndio Uislamu na imani**."[4]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Mwenye haya elimu yake ina manufaa**."[5]

### UNYENYEKEVU

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Aliye bora kati ya vijana wenu ni mwenye kujipamba kwa pambo la vikongwe wenu. Na aliye mbaya kati ya vikongwe wenu ni yule mwenye kujipamba kwa pambo la vijana wenu**."[6]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu anampenda mtoto wa miaka ishirini anaposhabihiana na mtu wa miaka the- manini. Na anamchukia mtu wa miaka sitini anaposhabihiana na mtoto wa miaka ishirini**."[7]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu huvutiwa na kijana asiyekuwa na kiburi**. "[8]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Aliye bora kati ya vijana wenu ni mwenye kujishabihisha na vikongwe wenu. Na aliye mbaya kati ya vikongwe wenu ni yule mwenye kujishabihisha na vijana wenu**."[9]

### MTAZAMO WA MBALI

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "Mtu mmoja alimjia Mtume **(s.a.w.w)** na kumwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu niusie.' Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia: **'Je utafuata usia iwapo mimi nitakuusia?'** akamuuliza hivyo mara tatu naye akijibu ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia: **'Hakika mimi nakuusia utakapoazimia jambo chunguza matokeo yake, ikiwa kuna mafanikio basi litekeleze na kama kuna kufeli basi liache**."[10]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Kufikiri kabla ya kutenda kunakusalimisha na majuto**."[11]

---

1. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 106, hadithi ya 6.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4666.
3. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8650.
4. Tuhaful-Uqual, Uk. 360.
5. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 106, hadithi ya 3.
6. Irshadul-Quluub, Uk. 41.
7. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 525, hadihti ya ya 7732.
8. Musnad Ibnu Hambal, Juz. 6, Uk. 134, hadithi ya 17376.
9. Maanil-Akhbar, Uk. 401, hadithi ya 63.
10. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 525, hadihti ya ya 7732.
11. Uyunul-Akhbari Ridhaa, Juz. 2, Uk. 54, hadithi ya 204.

Imam Ali (a.s) amesema: "**Fikiri kabla ya kutenda ili usiaibike kwa uliyotenda**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwenye akili sana kati ya watu ni yule mwenye kuchunguza sana matokeo ya baadaye**."[2]

Imam Hasan (a.s) alipoulizwa kuwa ufanisi ni nini? Alisema: "**Ni kusubiria fursa yako na kuharakisha yale uwezayo**."[3]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Simama kwenye kila jambo mpaka utakapojua mwanzo wake na mwisho wake, kabla hujaliingia ukaja kujuta**."[4]

Kuwataka ushauri wenye rai: Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu aliambiwa: Ufanisi ni nini? Akasema: 'Ni kuwataka ushauri wenye rai na kuwafuata**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hakuna ushindi imara kama kuomba ushauri**."[6]

Imam Al-Kadhim (a.s) amesema: "**Atakayeomba ushauri hatokosa kusifiwa iwapo atapatia, na hatokosa udhuru iwapo atakosea**."[7]

## UHURU

Imam Ali (a.s) amesema: "**Usiwe mtumwa wa mwenzako ilihali bila shaka Mwenyezi Mungu amekufanya huru**."[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayejiepusha na matamanio basi atakuwa huru**."[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hakika kuwa na haya na utawa ni miongoni mwa maumbile ya imani, nazo ni tabia za mtu huru na pambo la watu wema**."[10]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Sifa tano asiyekuwa nayo moja basi si mwenye kustarehe sana: Ya kwanza: ni utekelezaji wa ahadi. Pili: ni kupanga mipango. Tatu ni haya. Nne ni tabia njema. Tano ni uhuru, nayo ndiyo yenye kukusanya sifa zote hizi**."[11]

## KUKUBALI UDHURU

Imam Ali (a.s) amesema: "**Kubali msamaha wa ndugu yako, kama hana udhuru basi muombee udhuru**."[12]

Imam Ali (a.s) alipokuwa akimuusia mwanae Muhammad bin Al-Hanafiyah alisema: "**Usimlazimishe ndugu yako kwa kufuata shaka, na wala usijitenge naye bila kumuomba akuelezee, kwani huenda ana udhuru nawe wamlaumu bure**."[13]

---

1. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5442.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 3367.
3. Maanil-Akhbari, Uk. 401.
4. Tuhaful-Uquul, Uk. 304.
5. Al-Mahasin, Juz. 2, Uk. 435, hadithi ya 2508.
6. Al-Kafiy, Juz. 8, Uk. 20, hadithi ya 4.
7. Ad-Durrat Al-Bahirah, Uk. 34.
8. Nahjul-Balagha, barua ya 31.
9. Tuhaful-Uquul, Uk. 99.
10. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 3605.
11. Al-Khiswal, Uk. 284, hadithi ya 33.
12. Tuhaful-Uquul, Uk. 112.
13. Man La Yahdhuruhul-Faqih, Juz. 4, Uk. 391, hadithi ya 5834

Imam Al-Kadhim (a.s) amesema: "Baba yangu alinishika mkono kisha akasema: 'Ewe mwanangu mpendwa! Hakika baba yangu Muhammad bin Ali alinishika mkono kama nilivyokushika na akaniambia: Hakika baba yangu mpendwa Ali bin Husain (a.s) alinishika mkono kama nilivyokushika na akaniambia: **Ewe mwanangu mpendwa! Mfanyie kheri kila aliyeitafuta kutoka kwako, ikiwa ni anayestahiki basi utakuwa umepatia sehemu yake, na ikiwa si anayestahiki basi wewe utakuwa ni unayestahiki. Hata kama mtu atakushutumu kuliani mwako kisha akageuka kushotoni mwako na akakuomba msamaha basi kubali msamaha wake**."[1]

1. Al-Kafiy, Juz. 8, Uk. 152, hadithi ya 141.

# JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA

## 3 - SEHEMU YA TATU

## VIZUIZI VINAVYOZUWIA USTAWI WA VIJANA

### KUTOJISHUGHULISHA

### KUTOKUJISHUGHULISHA KWAKEMEWA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika Mwenyezi Mungu anamchukia mwenye siha asiyejishughulisha, hayupo katika kujishughulisha na dunia wala katika kujishughulisha na akhera**."[1]335

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Ikiwa kujishughulisha ni taabu basi kuendelea na kutojishughulisha ni uharibifu**."[2]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Moyo usiyojishughulisha hutafuta mabaya. Na mkono usiojishughulisha hupelekea kwenye ubaya**."[3]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Atakayefanya uvivu kwenye tohara yake na Swala yake basi hana kheri na jamabo la akhera yake. Na atakayefanya uvivu kwenye jambo litakalotengeneza maisha yake basi hana kheri na jambo la dunia yake**."[4]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Mwenyezi Mungu anachukia kuendekeza kulala na kuendekeza kukaa bila kujishughulisha**."[5]

Imepokewa kutoka kwa Umar bin Yazid amesema: "Nilimwambia Abu Abdillah [(a.s)]: Mtu anayesema: 'Nitakaa nyumbani kwangu, nitaswali, nitafunga na kumwabudu Mola wangu Mlezi. Ama riziki yangu itaniijia yenyewe.' Abu Abdillah [(a.s)] akasema: **'Huyu ni mmoja kati ya watu watatu ambao dua zao hazijibiwi**."[6]

Asbatu bin Salim amesema: "Niliingia kwa Abu Abdillah [(a.s)] akatuuliza kuhusu Umar bin Muslim amefanya nini? Nikasema: Ni mwema lakini yeye ameacha biashara. Abu Abdillah [(a.s)] akasema: 'Kazi ya shetani.' Mara tatu. Kisha akasema: **'Hivi hajui kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alinunua bidhaa kutoka Shamu ndipo akajipatia riziki ambayo alilipia deni lake na kuwagawia karaba zake**."[7]

Zararah amesema: "Mtu mmoja alimjia Abu Abdillah [(a.s)] na kumwambia: 'Mimi siwezi kufanya kazi vizuri kwa mkono wangu, na wala siwezi kufanya vizuri biashara, nami ni muhitaji mwenye haja.' Akamwambia: **'Fanya kazi, beba juu ya kichwa chako, na usiwahitajie watu**."[8]

Imepokewa kutoka kwa Al-Mufadhal bin Umar amesema: "Tafuteni msaada kupitia sehemu ya dunia kwa ajili ya akhera, kwani hakika mimi

---

1. Sharhu Nahjul-Balagha, Juz. 17, Uk. 146.
2. Al-Irshad, Juz. 1, Uk. 298.
3. Sharhu Nahjul-Balagha, Juz. 20, Uk. 303, hadithi ya 473.
4. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 85, hadithi ya 3.
5. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 84, hadithi ya 3.
6. Al-Kafiy, Juz. 5 Uk. 77, hadithi ya 1.
7. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 75, hadithi ya 8.
8. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 76, hadithi ya 14.

nimemsikia Abu Abdillah (a.s) akisema: **'Tafuteni msaaada kupitia sehemu ya hii ili mpate hii. Na wala msiwe wategemezi kwa watu**."[1]

Imam Al-Kadhim (a.s) amesema: "**Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anamchukia mja mwenye kulalalala asiyejishughulisha**."[2]

### MADHARA YA KUTOJISHUGHULISHA

Ibnu Abbas amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa amuonapo mtu na akavutiwa naye husema: 'Je ana kazi?' Wakimwambia hana, basi husema: 'Hana nafasi tena kwangu.' Huambiwa: Vipi hilo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Husema: **'Kwa sababu muumini akiwa hana kazi ataishi kwa dini yake**."[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ujinga hutokana na kutojishughulisha**."[4]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "Huko Madina kulikuwa na mtu asiyejishughulisha ambaye watu walikuwa wakimcheka. Akasema: 'Huyu mtu -Yaani Ali bin Husein - amenishinda kumchekesha. Basi akapita Ali (a.s) akiwa na vijana wake wawili, ndipo mtu yule akaja na kumnyang'anya joho lake toka shingoni, kisha akaondoka na wala Ali (a.s) hakumgeukia. Wakamwendea na kumnyanganya joho, wakalileta kwake na kumtupia. Umam (a.s) akawauliza ni nani huyu? Wakamwambia: Huyu ni mwanaume asiyejishughulisha huwa anawachekesha watu wa Madina. Basi akasema: 'Mwambieni: **Hakika Mwenyezi Mungu ana siku ambayo wasiyojishughulisha watapa hasara humo**."[5]

Luqman (a.s) alisema: "**Wenye hesabu kali siku ya Kiyama ni aliyetoshelezwa asiyejishughulisha, kwani ikiwa kujishughulisha ni taabu basi kutokujishughulisha ni uharibifu**."[6]

## ULEVI

### KILA KILEVI KIMEHARAMISHWA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Fahamuni kila kilevi ni haramu, na kila kilegezacho ni haramu. Kila kileweshacho kwa wingi ni haramu hata kwa uchache. Na kila kichanganyacho akili ni haramu**."[7]

Ummnu Salamah amesema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alikataza kila kilevi na kila kilegezacho nguvu**."[8]

Imam Al-Kadhim (a.s) amesema: "**Hakika Mwenyezi Mungu hajakataza pombe kwa ajili ya jina lake, lakini aliikataza kutokana na matokeo yake. Basi kila ambacho matokeo yake ni sawa na pombe nacho ni haramu**."[9]

---

1. Tuhaful-Uquul, Uk. 513.
2. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 84, hadithi ya 2.
3. Jamiul-Akhbar, Juz. 5, Uk. 84, hadithi ya 1084.
4. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 9251.
5. Biharul-An'war, Juz. 46, Uk. 68, hadithi ya 39.
6. Tanbihul-Khawatir, Juz. 1, Uk. 60.
7. Kanzul-Ummal, Juz. 5, Uk. 368, hadithi ya 13273.
8. Sunan Abu Daud, Juz. 3, Uk. 329, hadithi ya 3686.
9. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 412, hadithi ya 2.

### TAHADHARI DHIDI YA MADAWA YA KULEVYA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Umma wangu utafikiwa na zama watakuwa wanakula kitu jina lake ni Banji** [1].**Mimi najitenga nao na wao wako mbali na mimi**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mtoleeni salamu Myahudi na Mnasara, lakini msimtolee salamu mlaji wa Banji**."[3]

(Nasema: Huenda kwa sasa ni aina moja ya madawa ya kuilevya ya kisasa. Na huenda ikawa ni jamii fulani ya milungi, japo maumbile yanatofautiana, kwani hata hii huliwa kama iliwavyo milungi.) - Mfasiri.

## RAFIKI MBAYA

### MADHARA YA RAFIKI MBAYA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mfano wa mwenza aliye mwema ni mfano wa muuza manukato, ikiwa hatakupa manukato yake basi harufu yake itakupata. Na mfano wa mwenza muovu ni mfano wa muhunzi, ikiwa hatakuunguza nguo yako basi harufu yake itakusibu**."[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi najikinga kwako na sahiba mwenye mghafala na rafiki mbaya**."[5]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Kuandamana na watu waovu kunaleta uovu, ni kama upepo upitapo kwenye harufu mbaya huleta harufu mbaya**."[6]

Musa [(a.s)] amesema: "**Atakayejiepusha na rafiki mbaya ni kana kwamba ameifanyia kazi Taurati**."[7]

Luqman [(a.s)] alimwambia mwanawe: "**Anayefanya urafiki na mtu mbaya basi hatosalimika**."[8]

Ali bin Asbati amepokea kutoka kwa Maimamu [(a.s)] kuwa: "**Miongoni mwa mawaidha ya Mwenyezi Mungu kwa Isa (a.s) ni: Ewe Isa! Jua kuwa rafiki mbaya ananifanyia uadui, na rafiki mbaya ananipinga. Na jua ni nani unayefanya naye urafiki. Na jichagulie ndugu miongoni mwa Waumini**."[9]

Imepokewa kutoka kwa Sufyan At-Thawriy amesema: "Nilikutana na mkweli mwana wa mkweli Jafar bin Muhammad [(a.s)], nikamwambia: Ewe mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, naomba uniusie. Akaniambia: 'Ewe Sufyan! Mzazi wangu aliniamuru mambo matatu na akanikataza mambo matatu, na miongoni mwa hayo aliyoniambia ni: **'Ewe mwanangu mpendwa! Atakayeandamana na rafiki mbaya hatosalimika**."[10]

---

1. Ni jina la kiarabu ambalo linamaanisha aina fulani ya mti ambao hutoa mbegu zenye kulewesha. Tazama Majmaul-Bahrain Juz. 1, Uk. 191.
2. Mustadrakul-Wasail, Juz. 17, Uk. 85, hadithi ya 20815.
3. Mustadrakul-Wasa'il, Juz. 17, Uk. 86, hadithi ya 20815.
4. Kanzul-Ummal, Juz. 9 Uk.22, hadithi ya 24736.
5. Az-Zuhdu cha Ibnu Mubarak Uk. 303, hadithi ya 875.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5839.
7. Jamiul-Akhbar, Uk. 508, hadithi ya 1413.
8. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 642, hadithi ya 9.
9. Al-Kafiy, Juz. 8 Uk. 134, hadithi ya 103.
10. Al-Khiswal, Uk. 169, hadithi ya 222.

Alama za rafiki mbaya: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya mwisho basi asifanye undugu na kafiri na wala asiandamane na muovu. Atakayefanya undugu na kafiri au akaan- damana na muovu atakuwa kafiri au muovu**."[1]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Atakayekusitiri aibu yako na akakuaibisha uwapo haupo basi ni adui, jihadhari naye**."[2]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Jiepusheni na wale ambao nyoyo zenu zinawachukia**."[3]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Ambaye mapenzi yake si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu basi jihadhari naye. Kwani hakika mapenzi yake ni mabaya na usuhuba wake ni hatari**."[4]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Inafaa kwa anayetaka kuitengeneza nafsi yake na kuihifadhi dini yake ajiepushe kuandamana na watu wa dunia**."[5]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Tazama kila asiyekuwa na manufaa na wewe katika dini yako basi usiwe na mazoea naye, na wala usiwe na ragh- ba ya kusuhubiana naye, kwani hakika kila asiyekuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu matokeo yake ni mabaya yenye kudhuru**."[6]

Adam [(a.s)] alimuusia mwanae Shi'ithi: "**Nyoyo zenu zikikataa kitu basi jiepusheni nacho, kwani hakika mimi niliposogea kwenye mti ili nichume moyo wangu ulikataa, hivyo lau kama ningelijizuia kula basi yasingelinis- ibu yaliyonisibu**."[7]

Marafiki wabaya

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Msiandamane na waovu**."[8]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Msifanye urafiki na mlevi wa pombe, kwani kufanya naye urafiki huleta majuto**."[9]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Jizuieni kufanya urafiki na kila mwenye kheri ndogo, mwenye shari nyingi, khabithi wa nafsi. Anapokhofu hujikunyata na anapopata amani hufanya ujabari**."[10]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Aliye mbaya kati ya ndugu zako ni yule anayekuridhisha kwa batili**."[11]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Aliye mbaya kati ya ndugu zako ni anayekupaka mafuta ndani ya nafsi yako na kukuficha aibu zako**."[12]

---

1. Biharul-An'war, Juz. 74, Uk. 197, hadithi ya 31.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8745.
3. Biharul-An'war, Juz. 74 Uk. 198, hadithi ya 34.
4. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8978.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 10951.
6. Biharul-An'war, Juz. 74, Uk. 191, hadithi ya 5.
7. 368 Biharul-An'war Juz. 78, Uk. 452, hadithi ya 19.
8. Irshadul-Quluub, Uk. 20.
9. Jamiul-Akhbar, Uk. 428, hadithi ya 1198.
10. Tanbihul-Khawatir, Juz. 2, Uk. 121.
11. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5690.
12. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5725.

Imam Ali (a.s) amesema: "**Jiepushe kuwapenda maadui wa Mwenyezi Mungu, au kuonyesha mapenzi yako ya dhati kwa wasiokuwa mawalii wa Mwenyezi Mungu, kwani hakika atakayeipenda kaumu fulani atafufuliwa pamoja nao**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwenye kusuhubiana na watu wabaya ni sawa na alierakibu merkebu baharini**."[2]

Imam Jawad (a.s) amesema: "**Jiepushe kusuhubiana na mtu muovu, kwani hakika yeye ni sawa na upanga wenye sumu, ukiutazama wavutia lakini athari zake ni mbaya**."[3]

### ULEVI WA UJANA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ujana ni matawi ya uendawazimu**."[4]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Aina za ulevi ni nne: Ulevi wa ujana, ulevi wa mali, ulevu wa kulala na ulevi wa ufalme**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Inapasa kwa mwenye akili ajiepushe na ulevi wa mali, ulevi wa uwezo, ulevi wa elimu, ulevi wa sifa, na ulevi wa ujana,kwani hakika hayo yote yana riha mbaya inayoondoa akili na kupunguza unyenyekevu**."[6]

Imepokewa kuwa Imam Ali na Maimamu (a.s) walikuwa wakiomba ndani ya mwezi wa Shabani: "**Ewe Mungu wangu nimemaliza umri wangu kwenye shari ya kukusahau Wewe. Na nimeumaliza ujana wangu katika ulevi wa kujitenga na Wewe. Ewe Mungu wangu ni siku nyingi sijaamka kwa ajili ya kukufanyia ujeuri, na kurakibu nikielekea njia ya ghadhabu Yako**."[7]

## MATAMANIO YA KIJINSIA

### MTEGO WA SHETANI

Mwenyezi Mungu amesema: "Waambie waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao, bila shaka Mwenyezi Mungu anazo khabari za yale wanayoyafanya. Na waambie waumini wanawake wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao isipokuwa unaodhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, na wasionyeshe uzuri wao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba za waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au watoto wa kaka zao, au watoto wa dada zao, au wanawake wenzao, au wale waliomilikiwa na mikono yao au wafuasi wanaume wasio na matamanio (kwa wanawake), au watoto ambao hawajajua siri za wanawake. Wala wasipige chini miguu yao ili yajulikane mapambo waliyoyaficha. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu enyi wenye kuamini ili mpate kufaulu." (Surat Nuur: 30 -31).

---

1. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 2703.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 9835.
3. Ad-Duratu Al-Bahirah, Uk. 40.
4. Man Layahdhuruhul-Faqiih, Juz. 4, Uk. 377, hadithi ya 5774.
5. Tuhaful-Uquul, Uk. 124.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 10948.
7. Biharul-An'war, Juz. 94, Uk. 98, hadithi ya 13.

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mtazamo wa kwanza ni bahati mbaya, wa pili ni makusudi na wa tatu huangamiza**."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu imeongezeka juu ya mwanamke mwenye mume aliejipodoa macho yake kwa ajili ya asiyekuwa mumewe au asiyekuwa maharimu wake. Kwani hakika yeye iwapo atafanya hivyo Mwenyezi Mungu humporomoshea kila amali aliyoitenda**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Jiepusheni na mitazamo ya ziada, kwani yenyewe hupanda matamanio, na huzalisha mghafiliko**."[3]

Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Abbas amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuweka Fadhlu bin Abbas nyuma ya kipando chake

siku ya kuchinja (Siku ya Iddi kubwa), na Fadhlu alikuwa ni mwanaume mwenye mvuto, basi Mtume akasimama mbele ya watu akiwapa fatwa, ndipo akatokea mwanamke kutoka Khath'am naye akawa anamuuliza maswali Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, basi Fadhlu akawa akimkodolea macho mwanamke yule na akapendezwa na uzuri wake. Mtume akageuka ilihali Fadhlu akiwa bado anamkodolea macho, ndipo **(s.a.w.w)** akakishika kidevu cha Fadhlu na kuuondoa uso wake kwa mwanamke yule."[4]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Macho ni mitego ya shetani**."[5]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Jicho lionapo tamanio basi moyo hufumbia ambacho ni matokeo ya baadaye**."[6]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Ni dhambi ngapi hupatikana kwa kufumba na kufumbua?**"[7]

Imam Al-Baqir [(a.s)] amesema: "**Mwanamke malaya alitoka kuwafuata vijana wa kibani Israil na akawafanyia fitina. Baadhi yao wakasema: Mfanya ibada fulani angemuona angemfitini. Basi akasikia kauli zao, akasema: 'Wallahi siendi nyumbani kwangu mpaka nimfitini. Ndipo akamwendea usiku akamgongea mlango, akasema: 'Nimekimbilia kwako.' Akamkatalia. Akasema: 'Baadhi ya vijana wa kibani Israil wamenitamani wao wenyewe hivyo niingize kwako la sivyo watanikuta hapa na kunifedhehesha.' Basi aliposikia kauli yake hiyo akamfungulia mlango. Alipoingia akavua nguo zake, basi alipoona uzuri wake na umbile lake akamtamani, na hatimaye akaweka mkono wake juu yake, kisha nafsi yake ikarejea, wakati huo alikuwa amewasha moto ambao ametenga chungu, basi akaweka mkono wake juu ya moto. Mwanamke akasema: 'Unafanya nini?' Akasema: "Nauunguza kwa sababu wenyewe umefanya kitendo." Basi mwanamke akatoka akaliendea kundi la kibani Israil, akawaambia: 'Muokoeni fulani ameweka mkono**

---

1. Kanzul-Ummal, Juz. 5, Uk. 329, hadithi ya 13073.
2. Thawabul-Aaamal, Uk. 338.
3. Biharul-An'war, Juz. 72, Uk. 199, hadithi ya 29.
4. Sahih Bukhar, Juz. 5, Uk. 2300, hadithi ya 5874.
5. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 950.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4063.
7. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 6939.

**wake juu ya moto.' Basi wakamwen- dea wakamkuta mkono wake umeshaungua**."[1]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Mtazamo ni mshale miongoni mwa mishale ya Ibilisi wenye sumu, ni mitizamo mingapi ya muda mfupi imeleta hasara ya muda mrefu**."[2]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akiwasalimu wanawake na wanamjibu. Na jemedari wa waumini alikuwa akiwasalimu wanawake na alikuwa hapendi kuwasalimu mabinti miongoni mwao, na akisema: Nahofia sauti yake isinivutie nikaingiwa na mengi kuliko malipo niyatafutayo**."[3]

Masihi (a.s) amesema: "**Usiwe na macho makali ya kukodolea kisicho cha kwako, kwani utupu wako hautazini madamu macho yako umeyahifadhi. Ukiweza kutoitazama nguo ya mwanamke ambaye si halali kwako fanya hivyo**."[4]

Masihi aliwaambia wanafunzi wake: "**Jiepusheni kuwatazama wanawake ajnabiya (asiye maharim wako), kwani kwenyewe ni kupanda matamanio na ni miche ya ufuska**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ashki huenda ikapatikana kwa sekunde chache**."[6]

Imam As-Sadiq (a.s) alipoulizwa kuhusu ashki alisema: "**Nyoyo zilizojie- pusha na utajo wa Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu akazionjesha mapenzi ya kumpenda asiyekuwa Yeye**."[7]

Maangamio ya wafuata matamanio:

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ambaye hima yake kubwa ni kupata matamanio basi moyo wake hunyang'anywa utamu wa imani**."[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ni mara ngapi starehe za muda mfupi hurithisha huzuni ya muda mrefu?**"[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Jiepusheni matamanio yasizishinde nyoyo zenu, kwani hakika mwanzo wake ni nguvu na mwisho wake ni maangamizi**."[10]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwanzo wa matamanio ni burudani na mwisho wake ni karaha**."[11]

Madhara ya kujichanganya na wasiokuwa maharimu: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho halali sehemu ambayo mwanamke asiyekuwa maharimu wake anaisikia nafsi yake**."[12]

---

1. Biharul-An'war, Juz. 14, Uk. 492, hadithi ya 11.
2. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 559, hadithi ya 12.
3. Al-Kafiy, Juz. 2 Uk. 648, hadithi ya 1.
4. Tanbihul-Khawatir, Juz. 1, Uk. 62.
5. Biharul-An'war, Juz. 104, Uk. 42, hadithi ya 52.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5314.
7. Biharul-An'war, Juz. 73, Uk. 158, hadithi ya 1.
8. Tanbihul-Khawatir, Juz. 2, Uk. 116.
9. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 451, hadithi ya 1.
10. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 2746.
11. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 3133.
12. Biharul-An'war, Juz. 104, Uk. 50, hadithi ya 16.

Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "**Nuh (a.s) alipomuomba Mola wake Mlezi kuwaombea kaumu yake, Ibilisi aliyelaaniwa na Mwenyezi Mungu alimjia na kumwambia: 'Ewe Nuh! Nikumbuke sehemu tatu, sehemu niwapo karibu mno na mja na awapo moja ya sehemu hizo: Nikumbuke unapoghadhibika. Nikumbuke uhukumupo kati ya watu wawili. Na nikumbuke uwapo pamoja na mwanamke faraghani mkiwa hamna yeyote pamoja nanyi**."[1]

Muhammad Tayar amesema: "Niliingia Madina na nikatafuta nyumba nikodishe, basi nikaingia nyumba ambayo ndani yake mna nyumba mbili, kati yake kuna mlango na humo mna mwanamke, akasema: 'Unakodi nyumba hii?' Nikasema: Kati yake kuna mlango nami ni kijana. Akasema: 'Mimi nitafunga mlango kati yangu na wewe.' Basi nikahamishia mizigo yangu humo na nikamwambia: Funga mlango. Akaniambia: 'Uache upepo unaingia kwangu kupitia hapo.' Nikamwambia: Hapana, mimi ni kijana na wewe ni binti, mimi naufunga. Akasema: 'Kaa wewe nyumbani kwako mimi sikuijii na wala sikukaribii.' Basi akakataa kufunga mlango, ndipo nikamwendea Abu Abdillah (a.s) nikamuuliza kuhusu hilo. Akasema: **'Hama humo, kwani hakika mwanamke na mwanaume wanapokuwa faraghani ndani ya nyumba moja shetani huwa wa tatu wao**."[2]

## MALIPO YA UTAWA WA JINSIA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayekuwa na uwezo juu ya kitendo cha haramu juu ya mwanamke au kijakazi lakini akamwacha kwa ajili ya kumuogopa Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu ataharamisha moto juu yake na Mwenyezi Mungu Mtukufu atam- pa amani dhidi ya mshituko mkubwa (Kiyama)**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayetokewa na ufuska au matamanio kisha akajiepusha kwa ajili ya kumuogopa Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu atamuharamishia moto na atampa amani dhidi ya mshituko mkubwa na atamtimizia alichomwahidi ndani ya Kitabu chake katika kauli yake: 'Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake atapata Bustani mbili**."[4]

Imam Zainul-Abidina (a.s) amesema: "Mwanaume mmoja alirakibu baharini akiwa na mkewe basi jahazi likawapasukia, hakuna aliyeokoka miongoni mwa waliokuwa ndani ya jahazi ila mke wa mwanaume yule. Yeye aliokoka kwa kutumia mbao za jahazi ambazo zilimpeleka hadi kwenye kisiwa miongoni mwa visiwa vya bahari. Ndani ya kisiwa hicho kulikuwa na mwanaume mmoja ambaye alikuwa akisafiri na hakuacha heshima yoyote kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ila aliivunja. Basi hakujua lolote ila mwanamke aliyekuwa amesimama juu ya kichwa chake, akainua kichwa chake kumtazama, akasema: 'Ni binadamu au jini?' mwanamke akajibu: 'Mwanadamu.' Basi hakumzungumzisha neno lingine mpaka akawa amekaa kwake mkao wa mwanaume kwa mkewe. Alipoanza kumkusudia yule mwanamke akatetemeka, akamwambia: 'Kitu gani kinakutetemesha?'

1. Al-Khiswal Uk. 132, hadithi ya 140.
2. Man Layahdhuruhul-Faqiih Juz. 3 Uk. 252, hadithi ya 3913.
3. Thawabul-Aaamal Uk. 334.
4. Man Layahdhuruhul-Faqiih Juz. 3 Uk. 14, hadithi ya 4968.

Akajibu: 'Namkimbia huyu.' Akaashiria mkono wake mbinguni. Akasema: 'Umemfanya huyu chochote?' Akasema: 'Hapana bali nguvu zake.'Akasema: 'Wewe unamkimbia huyu mbio zote hizi ilihali hujamfanya huyu chochote, basi mimi nakuchukia mno, wallahi mimi ndiye ninayefaa zaidi kukimbia huku na kukhofu kuliko wewe.' Basi mwanaume akasimama bila ya kufanya chochote, ndipo akarudi kwa mkewe akiwa hana hima yoyote ila kutubu na kurejea Kwake. Alipokuwa akitembea njiani ghafla akasadifiana na padri, basi jua likawa kali juu yao, ndipo padri akamwambia kijana: 'Muombe Mwenyezi Mungu atufunike kwa kivuli cha mawingu kwani hakika jua limekuwa kali juu yetu.' Kijana akasema: 'Mimi sijui kama nina jema mbele ya Mola wangu Mlezi hata nipate ujasiri wa kumuomba chochote.' Akamwambia: 'Mimi nitakuwa naomba nawe unaitikia.' Akasema: 'Ndio.' Basi padri akaanza kuomba na kijana akiitikia, basi haraka sana kivuli cha wingu kikawa kimewafunika. Wakatembea chini yake mchana kidogo, kisha wakaachana njiani. Kijana akachukua njia yake na padri njia yake, ndipo ghafla mawingu yakawa pamoja na kijana. Padri akasema: 'Wewe ni bora kuliko mimi, kwa ajili yako dua imejibiwa na wala haijajibiwa kwa ajili yangu. Nipe habari ni kipi kisa chako?' Ndipo akampa habari za yule mwanamke. Akasema: 'Umesamehewa yaliyopita kutokana na kuingiwa na khofu, na angalia mustakbali wako jinsi gani utakuwa."[1]

## MALIPO YA MWENYE ASHKI ALIYE MTAWA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayekuwa na ashki akaficha na akajizuia na hatimaye akafariki basi yeye ni shahidi**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ashki pasipo na matamanio ni kafara ya dhambi**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakayekuwa na ashki akaficha na akavuta subira, Mwenyezi Mungu atamghufiria na kumwingiza Peponi.**"[4]

Imepokewa kutoka kwa Ibnu Abbas kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kuwa amesema: "**Watu bora katika umma wangu ni wale ambao hufanya utawa pindi Mwenyezi Mungu anapowapelekea balaa ya kitu." Wakamwambia: Ni balaa ipi? Akasema: 'Ashki**."[5]

## MITEGO YA SHETANI

Imam Ridhaa (a.s) amepokea kutoka kwa baba zake kuwa: "Hakika Ibilisi alikuwa akiwajia Manabii (a.s) kuanzia kwa Adam (a.s) mpaka Mwenyezi Mungu alipomleta Masih (a.s), alikuwa akiongea nao na kuwadadisi, na hakuna aliyekuwa akizungumza naye mara kwa mara kama Yahya bin Zakariya (a.s). Yahya akamwambia: 'Ewe Abu Marah mimi nina haja kwako.' Akamwambia: 'Wewe una uwezo zaidi siwezi kukukatalia ombi basi niulize ulitakalo, hakika mimi si mwenye kukukhalifu katika jambo ulitakalo.'

1. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 69, hadithi ya 8.
2. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 372, hadithi ya 7000.
3. Al-Firdawsu, Juz. 3, Uk. 94, hadithi ya 4266.
4. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 373, hadithi ya 7002.
5. 408 Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 373, hadithi ya 7001 na Uk. 779, hadithi ya 8732, zote zimenukuliwa kutoka kwa Daylamiy. Al-Firdawsu, Juz. 2, Uk. 174, hadithi ya 2867.

Yahya akasema: 'Ewe Abu Marah napenda unionyeshe mitego yako na mbinu zako ambazo kwazo huwanasa wanaadamu.' Ibilisi akasema: 'Kwa ukarimu wako na mapenzi yako, ninakuahidi hadi kesho.' Yahya alipoamka alikaa nyumbani kwake akisubiri ahadi na akamfungia mlango kabisa, ghafla akamhisi yuko usawa wake kutokana na mtego uliokuwa ndani ya nyumba yake, na hatimaye akaona sura ya uso wa kima na mwili wake ukiwa katika sura ya nguruwe, na macho yake yamepasuka kwa urefu. Kinywa chake kimepasuka kwa urefu na meno yake na kinywa chake ni mfupa mmoja bila kidevu wala ndevu, akiwa na mikono minne: Mikono miwili ikiwa kifuani mwake na miwili kwenye mabega yake. Mshipa wa kisigino ukiwa mbele na vidole vyake vikiwa nyuma na juu yake kukiwa na kuba na katikati yake kuna eneo lenye nyuzi zilizo kati ya rangi nyekundu, kijani njano na rangi zote, na mkononi mwake akiwa na kengele kubwa na juu ya kichwa chake kukiwa na yai na ndani ya yai kuna chuma kilichotungikwa kinashabihiana na koleo. Yahya alipotaamali akamwambia: 'Ni eneo gani hili ambalo liko katikati yako?' akajibu: 'Huu ni umajusi, mimi ndiye niliyeuanzisha na kuupamba kwa ajili yao.' Akamuuliza: 'Vipi hizi nyuzi zenye rangi?' akajibu: 'Hizi zote ni rangi za wanawake, mwanamke anaendelea kupaka rangi mpaka ananasa kwa rangi zake na kwazo nawatia watu kwenye fitina.' Akamuuliza: 'Vipi hii kengele iliyoko mikononi mwako?' Akasema: 'Huu ni mjumuiko wa ladha zote, kuanzia ngoma, zumali, gita, filimbi na ala. Na watu wanakaa kwenye vinywaji vyao wakiwa hawaburudiki kwa ladha basi hapo ndipo naitikisa kengele kati yao na hatimaye wanapoisikia basi mvuto wake huwavuta na hapo hupatikana anaecheza, mwenye kutikisa vidole vyake na hadi mwenye kuchana nguo yake.' Akamuuliza: 'Ni mambo gani ambayo yanakuridhisha sana?' Akasema: 'Wanawake, wao ndio mtego wangu, na kwa hakika wanapokusanyika walinganizi wema na watoa laana basi huenda kwa wanawake na wao huniridhisha.' Yahya akamwambia: 'Vipi hili yai lililopo juu ya kichwa chako?' Akasema: 'Kwalo najikinga na dua ya waumini.' Akamuuliza: 'Vipi hiki chuma nikionacho ndani yake?' Akajibu: 'Kwacho nazigeuza nyoyo za waumini.' Yahya akasema: 'Je kuna wakati wowote ulinishinda hata kido- go?' Akasema: 'Hapana, lakini kwako kuna sifa inivutiayo.' Yahya akamwambia: 'Ni ipi hiyo?' Akasema: 'Wewe ni mtu mlaji mno, unapofu- turu huendelea kula na kuvimbiwa na hilo hukukataza kutekeleza baadhi ya Swala na kisimamo chako cha usiku.' Yahya akamwambia: 'Hakika mimi nampa Mwenyezi Mungu ahadi kuwa sintoshiba chakula mpaka nitakapokutana naye.' Ibilisi akasema: 'Nami nampa Mwenyezi Mungu ahadi kuwa mimi sintomnasihi mwislamu mpaka nitakapokutana naye.' Kisha akatoka na hakurudi tena kwake baada ya hapo."[1]

1. Al-Amaal, cha Tus Uk. 339, hadithi ya 692.

5

# JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA

## MADHARA YA KIELIMU NA KISIASA

### WAJIBU WA KUJIKINGA DHIDI YA MADHARA YA KIELIMU

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Wahadharisheni watoto wenu na maghu- lati ili wasiwaharibu, kwani hakika maghulati ni viumbe wabaya mno kati ya viunbe vya Mwenyezi Mungu. Wanadharau utukufu wa Mwenyezi Mungu na wanadai uungu kwa waja wa Mwenyezi Mungu**."[1]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Harakisheni kuwafunza wanenu hadithi kabla murjiina hawajawatangulia kwao**."[2]

Tahadhari dhidi ya kuwafuata mbumbumbu: Mwenyezi Mungu amesema: "**Wala usifuate usiyo na elimu nayo, hakika masikio na macho na moyo, hivyo vyote vitaulizwa**." (Surat Banii Israil: 36).

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Msiwe mabubusa, mnasema: 'Watu wakifanya wema nasi tunafanya, wakidhulumu nasi tunadhulumu. Lakini zipeni mamlaka nafsi zenu, watu wakifanya wema nanyi fanyeni wema, wakifanya ubaya basi nyinyi msidhulumu**."[3]

Kumayl bin Ziyad amesema: "Jemedari wa waumini Ali bin Abu Talib alinishika mkono akanitoa hadi jangwani, basi alipoligusa tu jangwa alivuta pumzi kidogo na kisha akasema: **'Ewe Kumayl bin Ziyad! Hizi nyoyo ni vyombo na kilicho bora zaidi ni kile chenye kuzingatia. Basi hifadhi kutoka kwangu yale nikwambiayo: Watu ni wa aina tatu: Yupo alimu mtiifu kwa Mola, mwenye kujifunza katika njia ya uokovu. Na mawimbi wafuata upepo wenye kumfuata kila mpiga kelele, wanafuata kila upepo, hawajaangaziwa kwa nuru ya elimu na wala hawajakimbilia kwenye nguzo imara.**"[4]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Msiwe mabubusa, mnasema: Mimi niko pamoja na watu nami ni kama mmoja kati ya watu**."[5]

Abu Hamza Thumali amesema: Abu Abdillah (a.s) aliniambia: 'Jiepushe na uraisi na jiepushe usiwe mfuata nyayo za watu." Nikamwambia: 'Mimi ni fidia kwako. Ama urais tunaujua, ama kufuata nyayo za watu ni kuwa theluthi ya niliyonayo ni kutokana na kufuata nyayo za watu.' Akaniambia: **'Si kama unavyodhani, ni kuwa jiepushe kumpa mtu utawala bila kuwa na hoja, ukaja kumsadikisha kwa kila alisemalo**."[6]

Imam Al-Kadhim (a.s) alimwambia Fadhlu bin Yunus: "Fikisha kheri na sema kheri na wala usiwe bubusa." Nikamwambia: 'Bubusa ni nani?' akasema: 'Usiseme: Mimi ni kama mmoja miongoni mwa watu, kwani hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: '**Enyi watu!**

1. Al-Amaaliy cha Tusiy Uk. 650, hadithi ya 1349.
2. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 47, hadithi ya 5.
3. Sunan Tirmidhiy, Juz. 4, Uk. 374, hadithi ya 2007.
4. Nahjul-Balagha, hekima ya 147.
5. Maanil-Akhbar Uk. 266, hadithi ya 1.
6. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 298, hadithi ya 5.

**Hakika njia ni mbili: Njia ya kheri na njia ya shari. Hivyo njia ya shari isiwe ipendwayo kwenu kuliko njia ya kheri**."[1]

### WAJIBU WA KUWAKHALIFU VIONGOZI WAOVU

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Enyi kundi la vijana mcheni Mwenyezi Mungu na wala msiwafuate viongozi, waacheni mpaka wawe wafuasi. Msiwafanye watu marafiki wa moyo mkamwacha**[2] **Mwenyezi Mungu. Hakika sisi wallahi ni bora kwenu kuliko wao.' Kisha akapiga mkono wake juu ya kifua chake**."[3]

## MAAFA YA KITABIA NA KIMATENDO

### KUTOTIMIZA HAKI ZA WAZAZI WAWILI

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Lau kama Mwenyezi Mungu angefahamu kilicho chini zaidi ya (kusema kumwambia mzazi) Akh! katika kutotimiza haki za wazazi wawili basi angekiharamisha. Mwenye kushindwa kutimiza haki za wazazi afanye afanyavyo hatoingia Peponi**."[4]

Imam Al-Baqir [(a.s)] amesema: "**Baba yangu alimwona mwanaume akiwa na mwanaye akitembea kwa miguu huku mtoto akiwa kaegemea kwenye dhiraa ya baba. Akasema: Basi baba yangu hakumsemesha kwa ajili ya kuchukizwa naye mpaka anaiacha dunia**."[5]

Imam Al-Baqir [(a.s)] amesema: "**Baba mbaya ni yule ambaye wema unam- peleka kwenye uvukaji mipaka. Na mtoto mbaya ni yule ambaye kupuuzia humpelekea kutotimiza haki za wazazi**."[6]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Kiwango cha chini kabisa cha kutotimiza haki za wazazi ni neno Akh. Na lau kama Mwenyezi Mungu angejua kitu chepesi zaidi ya hilo basi angekikataza**."[7]

Imam Al-Askar [(a.s)] amesema: "**Ujasiri wa mtoto dhidi ya baba yake utotoni mwake hupelekea kumnyima haki zake ukubwani mwake**."[8]

### TABIA MBAYA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Tabia mbaya ni dham- bi isiyoghufiriwa**."[9]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alipoambiwa: "**Fulani anafunga mchana na kuswali usiku lakini yeye ana tabia mbaya anamuudhi**

---

1. Tuhaful-Uquul, Uk. 413.
2. Anaashiria kauli ya Mwenyezi Mungu: "Je mnadhani kuwa mtaacha na hali Mwenyezi Mungu hakuwabainisha wale waliopigania dini miongoni mwenu wala hawakumfanya rafiki wa moyo isipokuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Waumini? Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayofanya." (Surat Twba: 16).
3. Tafsirul-Ayyash, Juz. 2, Uk 82, hadithi ya 32. Biharul-An'war, Juz. 24, Uk. 246, hadithi ya 5.
4. Al-Firsawsu, Juz. 3, Uk. 353, hadithi ya 5063.
5. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 349, hadithi ya 8.
6. Tarikhul-Yaaqubiy, Juz. 2, Uk. 320.
7. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 48, hadithi ya 1.
8. Tuhaful-Uquul, Uk. 489.
9. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 443, hadithi ya 7363.

**jirani yake kwa ulimi wake.'Akasema: 'Hana kheri, naye ni miongoni mwa watu wa motoni**."[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ambaye tabia zake zitakuwa mbaya basi riziki yake itabana**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ambaye tabia yake itakuwa mbaya atatengwa na rafiki**."[3]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Ambaye tabia yake itakuwa mbaya basi ameiadhibu nafsi yake**."[4]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "Luqman (a.s) alisema: **'Ewe mwanangu mpendwa! Jiepushe na ghadhabu, tabia mbaya na uchache wa subira, haku- na mtu anayekuwa sawa juu ya sifa hizi. Ilazimishe nafsi yako ridhaa kati- ka mambo yako, na ivumilishe nafsi yako katika matumizi ya jamaa na wafanyie watu wote tabia njema**."[5]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Ambaye ulimi wake utaogopwa na watu basi huyo ni mtu wa motoni**."[6]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Maafa ya uzuri ni mawazo hewa (yatokanayo na kiburi)**."[7]

## KUJIONA/ KUJIKWEZA

Imam Ali (a.s) amesema: "**Lililo baya mno kati ya mambo ni mtu kujikweza mwenyewe**."[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayejiona adhimu ndani ya nafsi yake basi mbele ya Mwenyezi Mungu atakuwa duni**."[9]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "Mcheni Mwenyezi Mungu wala msihusudiane nyinyi kwa nyinyi, hakika miongoni mwa sheria za Isa bin Maryam ilikuwa ni kutembea mjini, ndipo siku moja akatoka katika

matembezi yake akiwa na mwanaume mbilikimo miongoni mwa sahaba zake, naye alikuwa ni mwandama mno wa Isa bin Maryam (a.s).

Isa (a.s) alipofika baharini alisema: 'Bismillahi' kwa usahihi akiwa na yakini nayo, akatembea juu ya maji. Basi mtu yule mbilikimo alipomtazama Isa (a.s) alimuiga kwa usahihi akiwa na yakini nayo, naye akapita juu ya maji na kuungana na Isa (a.s). Hilo likamfanya ajikweze, akasema: 'Huyu Isa (a.s) Ruhullah anatembea juu ya maji nami pia natembea juu ya maji, basi ana ubora gani juu yangu.' Hapo hapo akazamishwa ndani ya maji na ndipo akaanza kuomba msaada toka kwa Isa (a.s), akamshika mkono na kumwopoa toka ndani ya maji, kisha akamwambia: 'Ulisema nini ewe mbilikimo?' Akasema: 'Nilisema: Anatembea juu ya maji nami natembea juu ya maji, basi hilo likanifanya nijione.' Isa (a.s) akamwambia: 'Umeiweka nafsi yako sehemu isiyokuwa ile aliyokuweka Mwenyezi Mungu, ndipo Mwenyezi Mungu akakuchukia kwa uliyosema, hivyo tubu kwa Mwenyezi Mungu

---

1. Biharul-An'war, Juz.81, Uk. 394, hadithi ya 63.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8023.
3. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 9187.
4. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 321, hadithi ya 4.
5. Biharul-An'war, Juz. 13, Uk. 419, hadithi ya 14.
6. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 327, hadithi ya 3.
7. Man Layahdhuruhul-Faqiih, Juz. 4, Uk. 373, hadithi ya 5762.
8. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5723.
9. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8609.

kutokana na uliyose- ma.' Basi mbilikimo yule akatubu na akarejea kwenye daraja lake ambalo Mwenyezi Mungu alimweka. Mcheni Mwenyezi Mungu msihusudiane nyinyi kwa nyinyi."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Jiepusheni na kiburi, kwani hakika kiburi huwa kwa mtu hata kama ana joho**."[2]

## PUPA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika mwanaadamu ni mwenye pupa juu ya yale aliyonyimwa**."[3]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwenye pupa ni fakiri hata kama ataimiliki dunia kwa mikono yake**."[4]

## HUSUDA

Imam Ali (a.s) amesema: "**Husuda ni matokeo ya kuchoka**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Husuda huzuia raha**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Husuda haileti ila madhara na hasira. Hudhoofisha moyo wako na kuuguza mwili wako. Na shari ambayo inayohisiwa na moyo wa mtu ni husuda**."[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hasidi milele ni mgonjwa (alilu)**."[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hasidi daima ni mgonjwa hata kama ni mwenye mwili wenye siha**."[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hasidi hafanikiwi**."[10]

Imam Ali (a.s) amesema: "**La ajabu ni mghafiliko wa mahasidi kunako usalama wa miili**."[11]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hasidi hudhihirisha mapenzi yake kwenye kauli zake na huficha chuki yake kwenye vitendo vyake. Ana jina la rafiki na sifa ya adui**."[12]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Matunda ya husuda ni mahangaiko ya dunia na akhera.**"[13]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "Luqman (a.s) alimwambia mwanae: **'Hasidi ana alama tatu: Anasengenya anapokuwa hayupo. Huonesha mapenzi ya uongo anaposhuhudia na hufurahia msiba**."[14]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Hasidi ni mwenye kujidhuru yeye mwenyewe kabla hajamdhuru mhusudiwa, kama ambavyo Ibilisi kwa**

---

1. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 306, hadithi ya 3.
2. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 526, hadithi ya 7735.
3. Kanzul-Ummal, Juz. 16, Uk. 113, hadithi ya 44095.
4. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1753.
5. Biharul-An'war, Juz. 78, Uk. 13, hadithi ya 71.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 372.
7. Biharul-An'war, Juz. 73, Uk. 256, hadithi ya 29.
8. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 782.
9. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1963.
10. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1017.
11. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1803.
12. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 2105.
13. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4632.
14. Al-Khiswal, Uk. 121, hadithi ya 113.

**husuda yake alirithisha laana ndani ya nafsi yake, na akarithisha kwa Adam (a.s) kujielekeza (kwa Mola wake)**."[1]

## CHUKI YA NDANI (HIKDI)

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hikdi huumiza nafsi na huongeza maumivu ya moyo**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayetoa chuki basi moyo wake na akili yake hustarehe**."[3]

## HASIRA

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hasira ni sehemu ya uwendawazimu kwa sababu mwenye nayo hujuta, na ikiwa hajuti basi uwendawazimu wake huendelea**."[4]

## UBISHI

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ubishi hunyakua rai**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ubishi huharibu rai**."[6]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Matunda ya ubishi ni kuangamia**."[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mbishi hukumbana na balaa.**"[8]

Imam Zainul-Abidiin (a.s) amesema: "**Ubishi huambatana na ujinga, na ushabiki huletwa na msiba, na sababu ya heshima ni unyenyekevu.**"[9]

## UVIVU

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimwambia Ali (a.s): "**Jiepushe na sifa mbili: Hasira na uvivu, kwani hakika wewe ukikasirika hutosubiri juu ya haki, na ukifanya uvivu hutotekeleza haki**."[10]

Imam Al-Baqir (a.s) amesema: "**Hakika mimi nachukia sana mtu kufanya uvivu kunako jambo la dunia yake. Na atakayefanya uvivu juu ya jambo la dunia yake basi ni mvivu kunako jambo la akhera yake**."[11]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hakika mambo yalipochanganyikana, uvivu na kushindwa vilijichanganya pamoja na hatimaye vikazaa ufakiri**."[12]

Imam Ali (a.s) amesema katika sifa za muumini: "**Utamuona uvivu wake uko mbali; na uchangamfu wake ni wa daima**."[13]

Imam Zainul-Abidiin (a.s) amesema katika dua zake: "**Ewe Mola wetu Mlezi tupe neema ya uchangamfu na utukinge na kufeli na uvivu**."[14]

---

1. Biharul-An'war, Juz. 73, Uk. 255, hadithi ya 23.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1962.
3. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8584.
4. Nahjul-Balagha, hekima ya 255.
5. Nahjul-Balagha, hekima ya 179.
6. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 1078.
7. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 4596.
8. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 5389.
9. Nuzhatun-Nadhir, Uk. 91, hadithi ya 14.
10. Man Layahdhuruhul-Faqiih, Juz. 4 Uk. 355, hadithi ya 5762.
11. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 230, hadithi ya 1.
12. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 86, hadithi ya 8.
13. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 230, hadithi ya 1.
14. Biharul-An'war, Juz. 94, Uk. 125.

## KUVUKA MIPAKA KATIKA IBADA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Jiepusheni kuifanya nzito dini, kwani hakika Mwenyezi Mungu ameifanya nyepesi, ichukueni kadri muwezavyo, kwani hakika Mwenyezi Mungu hupenda maadamu tu ni katika amali njema hata kama ni ndogo.**"[1]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Atakayeifanya nzito dini basi hatafika kwenye haki**."[2]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Hutomuona mjinga ila ni mwenye kupuuza au mwenye kupituka**."[3]

## KUJIPAMBA KULIKOKEMEWA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Si miongoni mwetu wale wanawake wenye kujishabihisha na wanaume. Na wala wanaume wenye kujishabihisha na wanawake**."[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Makundi ya aina mbili ni ya motoni na sitoyaona: Kaumu wenye mijeledi kama mikia ya ng'ombe wanaitumia kuwapiga watu. Na wanawake wenye kujiachia wenye kubaki uchi, wenye kushawishi wenye kuringa.hawatoingia peponi na wala hawatoipata harufu yake**."[5]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Mwenye kushabihiana na kaumu hukaribia kuwa miongoni mwao**."[6]

## KUENDEKEZA KUFIKIRIA STAREHE

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ambaye fikara zake zitazama kwenye starehe basi zitamshinda**."[7]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ambaye fikara zake zitazama kwenye maasi yatamwita ayaendee**."[8]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "Wanafunzi wa Isa (a.s) walijikusanya kwake na kumwambia: 'Ewe mwalimu wa kheri tuongoze.' Akawaambia: 'Hakika Musa Kalimullah aliwaamuru msiape kwa Mwenyezi Mungu ilihali ni waongo. Na mimi nawaamuru kuwa msiape kwa Mwenyezi Mungu ilihali ni waongo na si wakweli.' Wakasema: 'Ewe Ruhullah tuzidishie.' Akasema: **'Musa Nabii wa Mwenyezi Mungu aliwaamuru msizini nami nawaamuru msizisimulie nafsi zenu zinaa achia mbali kuitekeleza. Kwani hakika mwenye kuisimulia nafsi yake zinaa anakuwa kama mtu aliyewasha moto ndani ya nyumba iliyorembwa, na hatimaye moshi ukaharibu marembo hata kama nyumba haikuungua**."[9]

1. Kanzul-Ummal, Juz. 3, Uk. 35, hadithi ya 5348.
2. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8852.
3. Nahjul-Balagha, hekima ya 70.
4. Kanzul-Ummal, Juz. 15, Uk. 324, hadithi ya 41237.
5. Sahih Muslim, Juz. 3, Uk. 1689, hadithi ya 125.
6. Nahjul-Balagha, hekima ya 207.
7. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8564.
8. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 8561.
9. Al-Kafiy, Juz. 5, Uk. 542, hadithi ya 7.

## KUNYWA POMBE

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Pombe ni mama wa maovu na maasi**."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Pombe ni mama wa mabaya.**"[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Shari yote imekusany- wa ndani ya nyumba, na kunywa pombe kukafanywa ndio ufunguo wake**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Atakaelala amelewa basi huwa amelala akiwa biharusi wa shetani**."[4]

Imam Ali [(a.s)] amesema: "**Mwenyezi Mungu alifaradhisha kuacha pombe ili kuilinda akili**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Hakika maasi akiyatenda mja kwa siri hayamdhuru ila mtendaji wake. Na akiyatenda waziwazi bila kukemewa hudhuru jamii nzima**."[6]

---

1. Kanzul-Ummal, Juz. 5, Uk. 349, hadithi ya 13181.
2. Kanzul-Ummal, Juz. 5, Uk. 349, hadithi ya 13183.
3. Biharul-An'war, Juz. 79, Uk. 148.
4. Biharul-An'war, Juz. 79, Uk. 148, hadithi ya 58.
5. Nahjul-Balagha, hekima ya 252.
6. Biharul-An'war, Juz. 100, Uk. 74, hadithi ya 15.

# JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA

## SEHEMU YA NNE

## HAKI ZA VIJANA

### HAKI ZA VIJANA JUU YA WAZAZI WAO

### UMUHIMU WA HAKI ZA MTOTO

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mzazi hupatwa kutokana na haki za mtoto wake yale ambayo humpata mtoto kutokana na haki za mzazi wake**."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Wazazi hupatwa kutokana na kutomtimizia haki mtoto wao yale ambayo humpata mtoto wao kutokana na kutowatimizia haki zao**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Wazazi hupatwa kutokana na kutomtimizia haki mtoto wao iwapo ni mwema yale ambayo humpata mtoto**."[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mtoto ni bwana miaka saba, ni mtumwa miaka saba na ni waziri miaka saba**."[4]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Mwache mwanao acheze miaka saba, na huadabishwa miaka saba na mfuatilie miaka saba**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ambaye mwanae atafikia umri wa kuoa na akawa ana mali anayoweza kumuozesha lakini hakumuozesha kisha (mtoto) akizua la kuzua madhambi ni juu yake (mzazi)**."[6]

### UADILIFU

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Fanyeni uadilifu baina ya wanenu. Fanyeni uadilifu baina ya wanenu**."[7]

Nu'man Bin Bashir amesema: "Baba yangu alinipa kipawa basi Amrat bint Rawaha akasema: 'Siridhii mpaka umshuhudishe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akamjia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na kumwambia: 'Hakika mimi nimempa mwanangu toka kwa Amrat binti Rawaha kipawa, akaniamuru (Amrat) nikushuhudishe wewe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akamuuliza: 'Je umewapa wanao wengine kama hivyo?' akasema 'La.' Akamwambia: 'Mcheni Mwenyezi Mungu na fanyeni uadilifu baina ya wanenu.' Anasema: Basi akarejea na kumnyang'anya kipawa kile."[8]

Imam As-Sadiq [(a.s)] amesema: "**Uadilifu ni mtamu kuliko maji ayanywayo mwenye kiu. Ni upana ulioje wa uadilifu pindi mtu akifanyiwa hata kama ni mdogo**."[9]

---

1. Kanzul-UImmal, Juz. 16, Uk. 444, hadithi ya 45344.
2. Al-Kafiy, Juz. 6, Uk. 48, hadithi ya 5.
3. Al-Khiswal, Uk. 55, hadithi ya 77.
4. Makarimul-Akhalq, Juz. 1, Uk. 478, hadithi ya 1649.
5. Man Layahdhuruhul-Faqiih, Juz. 3, Uk. 492, hadithi ya 4743.
6. Kanzul-Ummal, Juz. 16, Uk. 442, hadithi ya 45337.
7. As-Sunanu Al-Kubra, Juz. 6, Uk. 293, hadithi ya 11999.
8. Sahih Bukhar, Juz. 2, Uk. 914, hadithi ya 2447.
9. Al-Kafiy, Juz. 2, Uk. 146, hadithi ya 11.

## DUA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Dua njema ya mzazi kwa mwanae ni sawa na dua njema ya Nabii kwa umma wake**."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Dua njema ya mzazi kwa mwanae ni sawa na maji kwenye mmea kwa manufaa yake**."[2]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mwenyezi Mungu humrehemu anayemsaidia mwanae kumfanyia mema, nako ni kumsamehe makosa yake na kumuombea mema katika yale yaliyopo kati yake na Mwenyezi Mungu**."[3]

## KUACHA KUMUOMBEA MABAYA

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Msiwaombee mabaya wanenu ikaja kuwa mwafaka kwa jibu kutoka kwa Mwenyezi Mungu**."[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Msijiombee mabaya na wala msiwaombee mabaya wanenu, wala msiiombee mabaya mali yenu, msifanye iwe mwafaka na saa ambayo humo huombwa kipawa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na hatimaye akawajibu**."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Msitamani kuhiliki kwa vijana wenu hata kama wana madhara, kwani hakika wao pamoja na hivyo walivyo bado wana vipindi (vya manufaa): Ima watubu na Mwenyezi Mungu awakubalie toba yao, na ima madhara yawapate. Na ima adui aje wamuue, ima janga la moto walizime, na ima maji wayazuie**."[6]

Imam As-Sadiq (a.s) amesema: "**Mtu yeyote atakayemuombea mwanae mabaya basi Mwenyezi Mungu humrithisha ufakiri (mtu huyo)**."[7]

Alama ya kuvuka mipaka katika kumlaumu: Imam Ali (a.s) amesema: "**Utakapomkemea kijana basi mwachie nafasi katika kosa lake ili kumkemea kusimpelekee kuwa na jeuri**."[8]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Kuzidisha kukemea huwasha moto wa ubishi (upinzani)**."[9]

Imam Ali (a.s) amesema: "**Unapokemea kemea kwa wastani**."[10]

---

1. Mishkatul-An'war, Uk. 282, hadithi ya 853.
2. Al-Firdawsu, Juz. 2, Uk. 213, hadithi ya 3038.
3. Biharul-An'war, Juz. 104, Uk. 98, hadithi ya 3038.
4. Tarikh Isbihan, Juz. 2, Uk. 296, hadithi ya 1784.
5. Sahih Muslim, Juz. 4, Uk. 2304, hadithi ya 3009.
6. Hilyatul-Awliyai, Juz. 5, Uk. 119.
7. Iddatud-Dai, Uk. 80.
8. Sharhu Nahjul-Balagha, Juz. 20, Uk. 333, hadithi ya 819.
9. Uyunul-Hikam Wal-mawaidh, Uk. 333, hadithi ya 819.
10. Ghurarul-Hikam, hadithi ya 3977.

## HAKI ZA KIJANA KIJAMII

### KUWAKIRIMU

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Wapeni nafasi vijana katika mabaraza, waelewesheni hadithi, kwani hakika wao ni warithi na watu wa hadithi**."[1]

Sahlu bin Sa'ad amesema: "Mtume **(s.a.w.w)** aliletewa bilauri akanywa kilichomo, kuliani mwake kulikuwa na kijana mdogo kuliko wote waliokuwepo, na kushotoni mwake **(s.a.w.w)** kulikuwa na wazee, basi akamwambia: 'Ewe kijana unaniridhia niwape wazee kilichomo?' akasema: **'Siwezi kumrithisha yeyote fadhila yangu kutoka kwako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Basi akawa amempa**."[2]

Kuwaomba ushauri

Imam Ali (a.s) amesema: "**Ukihitaji ushauri wa jambo lililokutokea basi lidhihirishe kwa kuwaanza vijana kwani hakika wao ni moja ya akili na wepesi wa kutafakari, kisha baada ya hapo lirejeshe kwenye rai ya wazee na vikongwe ili walipitie tena, na wafanye uteuzi wa maamuzi mazuri, kwani hakika uzoefu wao ni mwingi**."[3]

Kutilia umuhimu mahitaji yao maalumu

Ima Al-Baqir (a.s) amesema: "Hakika Ali (a.s) aliwaendea mabazazi na kumwambia aliye mtu mzima: 'Niuzie nguo mbili.' Mwanaume yule akasema: 'Ewe Jemedari wa waumini, kwangu kuna haja yako.' Alipojua kusudio lake akamwacha na akaenda kwa kijana, akachukua nguo mbili, moja kwa dirhamu tatu na nyingine kwa dirhamu mbili, akasema: 'Ewe Qanbar chukua ya dirhamu tatu.' Akasema: **'Wewe ndiye aula kwayo kwani unapanda mimbari na kuhutubia watu.' Akamjibu: 'Nawe ni kijana na bado una mvuto wa ujana, nami naona haya mbele ya Mola wangu Mlezi kuwa mbora juu yako**."[4]

Na mwisho wa dua yetu ni kumshukuru Allah Bwana Mlezi wa walimwengu.

### SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

### MWISHO WA KITABU

1. Al-Firdawsu, Juz. 1, Uk. 98, hadithi ya 320.
2. Sahih Bukhari, Juz. 2, Uk. 829, hadithi ya 2224.
3. Sharhu Nahjul-Balagha, Juz. 20, Uk. 337, hadithi ya 866.
4. Biharul-An'war, Juz. 40, Uk. 324, hadithi ya 6.

## YALIYOMO


**1 ................................. JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA**
UDONDOZI KUTOKA KITABU: JAWAAHIRU AL-HIKMAH LI 'SH-
1 ............................................................ SHABAAB
1 ................. KIMEANDIKWA NA: MUHAMMAD REYSHAHRI
1 .......... KIMETARJUMIWA: HEMEDI LUBUMBA SELEMANI
1 ......................................... NENO LA MCHAPISHAJI
2 ................................................................ DIBAJI
**4 ................................. JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA**
**4 ................................................ SEHEMU YA KWANZA**
4 ............. NAFASI YA KIPINDI CHA UJANA KATIKA USTAWI
4 ............................. 1- KIPINDI CHA USTAWI WA MAISHA
4 ............................. KUNUFAIKA NA FURSA YA UJANA
6 ................................................. HAZINA YA SIKU
6 ........... JUHUDI ZA DHATI KATIKA NJIA YA MAENDELEO
7 .................................... 2- USTAWI KATIKA KUJIJENGA
8 .................. NAFASI YA VIJANA KATIKA KUJIELIMISHA
9 ........................................... MAFUNZO YA KIROHO
9 ................ MANABII (A.S) WALITUMWA WAKIWA VIJANA
10 ................. 3 - NAFASI YA VIJANA KATIKA SERIKALI YA
10 .... BALOZI WA KWANZA WA MTUME (s.a.w.w) NI KIJANA
GAVANA WA KWANZA WA MAKKA NI KIJANA WA MIAKA
11 ............................................. ISHIRINI NA MOJA
NAFASI YA VIJANA KATIKA SERIKALI YA IMAM WA ZAMA
12 ............................................................ ZETU
**13 ............................... JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA**
**13 ................................................... SEHEMU YA PILI**
13 ............... SABABU ZINAZOPELEKEA USTAWI WA VIJANA
13 ........................................................ 1- MAARIFA
13 ................................................... KUJIELIMISHA
13 ................................................... KUJITAMBUA
14 ..................................... KUIJUA QUR'ANI TUKUFU
15 ............................................. KUJIFUNZA DINI
16 ........................................ UMUHIMU WA UDADISI
17 ........................................................ 2 - AZMA
17 ...................................................... KUJITUMA
18 ............................................. MALENGO YA JUU

18 ........................................ KUJIHESHIMU
19 ........................................ MSIMAMO
19 ........................ KUMTAWAKALI MWENYEZI MUNGU
**20 ............................... JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA**
20 ........................ 3 - UHUSIANO NA MWENYEZI MUNGU
20 ........ THAMANI YA IBADA KATIKA KIPINDI CHA UJANA
21 ............................ BARAKA ZA IBADA YA UJANANI
21 ............................................. MAANA YA IBADA
22 .................................... WASTANI KATIKA IBADA
22 ............................................. 4 - RAFIKI MWEMA
22 ................................. NAFASI YA RAFIKI MAISHANI
22 ........................................... KUMJARIBU RAFIKI
23 ............................................. AINA ZA MARAFIKI
23 ............................................. MARAFIKI BORA
25 ..................................... HAKI YA MWENZI WAKO
25 ........... 5 - MAHITAJI YA HALALI NA NGUVU ZA MWILI
25 ................................. NGUVU ZA MWILI ZASIFIWA
26 ........................................... SABABU ZA MVUTO
26 ........................................ BURUDANI
27 ........................................ MATEMBEZI
27 ........................................ MIZAHA
28 ........................... KUOGELEA NA KUTUPA MSHALE
29 ........................................ MIELEKA
29 ........................................ MASHINDANO
30 ....... 6 - THAMANI YA TABIA NJEMA NA MATENDO MEMA
30 ............................................. KUACHA MAASI
31 ........................................ TOBA
34 ........................................ NIDHAMU
34 ..................... KUHESHIMU HAKI ZA WAZAZI WAWILI
35 ........................................ KAZI
36 ...................................... KUWAHUDUMIA WATU
37 ........................................ UAMINIFU
38 ........................................ KUJIPAMBA
39 ............................................. MAADILI MEMA
40 ........................................ UTAWA
41 ........................................ KUANGUSHA MACHO

**43** ................................ **JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA**
**UDONDOZI KUTOKA KITABU: JAWAAHIRU AL-HIKMAH LI**
**43** ...................................................... **'SH-SHABAAB**
43 ...................................................... 3 - HIJABU
44 ............................................................ NDOA
44 ................................ A: MKAZO WA KUOA UJANANI
44 ......................................... B: MUME MARIDHAWA
44 ........................................... C: MKE MARIDHAWA
45 ............................................... D: KUOA AKRABA
45 ........................................................ HAYA
46 ........................................................ HAYA
46 ................................................ UNYENYEKEVU
46 .......................................... MTAZAMO WA MBALI
47 ...................................................... UHURU
47 ........................................... KUKUBALI UDHURU
**49** ................................ **JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA**
49 ......................................... 3 - SEHEMU YA TATU
49 .............VIZUIZI VINAVYOZUWIA USTAWI WA VIJANA
49 ................... KUTOKUJISHUGHULISHA KWAKEMEWA
50 ....................... MADHARA YA KUTOJISHUGHULISHA
50 ............................................................ ULEVI
50 ............................ KILA KILEVI KIMEHARAMISHWA
51 ........... TAHADHARI DHIDI YA MADAWA YA KULEVYA
51 ................................................... RAFIKI MBAYA
51 ................................ MADHARA YA RAFIKI MBAYA
53 ............................................... ULEVI WA UJANA
53 ....................................... MATAMANIO YA KIJINSIA
53 ........................................... MTEGO WA SHETANI
56 ............................... MALIPO YA UTAWA WA JINSIA
57 ............... MALIPO YA MWENYE ASHKI ALIYE MTAWA
57 ........................................... MITEGO YA SHETANI
**59** ................................ **JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA**
59 ........................... MADHARA YA KIELIMU NA KISIASA
WAJIBU WA KUJIKINGA DHIDI YA MADHARA YA KIELIMU
59 .............................................................
60 .......... WAJIBU WA KUWAKHALIFU VIONGOZI WAOVU
60 .......................... MAAFA YA KITABIA NA KIMATENDO

60 ..................... KUTOTIMIZA HAKI ZA WAZAZI WAWILI
60 ..................................................... TABIA MBAYA
61 ........................................ KUJIONA/ KUJIKWEZA
62 ............................................................. PUPA
62 .......................................................... HUSUDA
63 ...................................... CHUKI YA NDANI (HIKDI)
63 ........................................................... HASIRA
63 ............................................................ UBISHI
63 ............................................................. UVIVU
64 ............................. KUVUKA MIPAKA KATIKA IBADA
64 ................................. KUJIPAMBA KULIKOKEMEWA
64 ........................... KUENDEKEZA KUFIKIRIA STAREHE
65 ................................................ KUNYWA POMBE
**66 ................................ JOHARI ZA HEKIMA KWA VIJANA**
66 .................................................... SEHEMU YA NNE
66 ................................................. HAKI ZA VIJANA
66 .............................. UMUHIMU WA HAKI ZA MTOTO
66 ....................................................... UADILIFU
67 ............................................................... DUA
67 ............................ KUACHA KUMUOMBEA MABAYA
68 ......................................... HAKI ZA KIJANA KIJAMII
68 .................................................... KUWAKIRIMU
68 ............................................. SHARTI YA KUCHAPA
68 ........................................... MWISHO WA KITABU
69 ....................................................... YALIYOMO